ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	- Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Pili – Tarehe 20 Januari, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Moh'd Shein aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Nane la Wawakilishi Zanzibar tarehe 11 Novemba, 2010 ahsante.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 21

Gharama za Uchaguzi

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Serikali kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar hutengeneza karatasi za kupigia kura (*Ballot Papers*) nje ya Zanzibar kwaajili ya chaguzi mbali mbali za Kiserikali. Kwa kuwa mara nyengine hutokea kutokufanyika kwa uchaguzi ama wa Jimbo au Wadi kutokana na kasoro za karatasi za kupigia kura.

(a) Je, Mhe. Waziri, kasoro kama hizi zinasababishwa na nini.

(b) Zinapotokea kasoro kwenye karatasi za kupigia kura nani anawajibika kulipia gharama hizo.

(c) Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwaajili ya utengenezaji wa karatasi za Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Kasoro za karatasi za kura husababishwa na mambo mengi ikiwemo haya yafuatayo:

   i) Sababu za kiufundi wakati wa kuchapishwa na kufungwa kwa karatasi;

   ii) Karatasi za kura kuwa na taarifa zisizo sahihi za mgombea/ wagombea;

   iii) Karatasi za kura kutokezea kuwa pungufu kuliko idadi ya wapiga kura wanaostahiki kupiga kura hizo;

   iv) Kukosekana kabisa kwa karatasi za kura katika jimbo /wadi husika ; na

   v) Muingiliano wa karatasi za kura kimipaka na majina ya mitaa.

b) Inapotokezea kasoro za karatasi za kura, Serikali kupitia Tume ya Uchaguzi ndiyo inayolipia gharama za uchapishaji wa karatasi za kura kwa kufanya uchaguzi wa marejeo.

c) Jumla ya TShs. 495,321,368/= zimetumika kwa uchapishaji wa karatasi za kura katika uchaguzi Mkuu uliopita. Kati ya hizo T Shs. 422,521,128/= zilitumika kwa uchapishaji wa karatasi za kura kwa uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani na T.Shs. 72,800,240/= zilitumika kwa gharama mbali mbali za uendeshaji wa uchaguzi huo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa *ballot paper* kwa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar zinakuwa zinachapishwa za rangi, kwa kuwa *ballot paper* kwa ajili ya uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani huwa zinakuwa hazina rangi yaani *black and white*, na kwa kuwa tofauti ya uchapishaji wa *ballot paper* zile za rangi na zisizo za rangi inakuwa sio kubwa sana.

a) Je, Mhe. Waziri serikali imejipanga vipi kuona kwamba uchaguzi ujao *ballot papers* kwa ajili ya chaguzi zote zinakuwa za rangi kama vile *ballot* za chaguzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika uchaguzi uliopita?

b) Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa *ballot papers* zinazokuwa za rangi zinawarahisishia wapiga kura kuchagua vyama vyao ambavyo tayari rangi za vyama vyao zinakuwa zinaonekana, kuliko ilivyo hivi sasa?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nia yetu ni kufanya uchaguzi vizuri na kuhakikisha kwamba wanaopiga kura wananchi wanapata karatasi zinazofaa,

Mhe. Spika: Tuzifunge simu zetu kwa sababu zinaingiliana na mawasiliano humu ndani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Kuhakikisha kwamba wanaopiga kura wananchi wanapata karatasi zinazofaa kwa ajili ya kupigia kura. Kama ushauri wake utatufaa baada ya kupitiwa na Tume ya Uchaguzi, tutauchukua ushauri huo na kuufanyia kazi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa uchaguzi ni kila baada ya miaka mitano na kwa hivyo Tume ya Uchaguzi ilikuwepo na inajua kwamba kuna uchaguzi.

a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kura za *sample* kwa wawakilishi hazikupatikana mpaka uchaguzi ukafika?

b) Kwa kuwa wagombea wawakilishi wote na madiwani waliitwa katika Tume ya Uchaguzi kuthibitisha karatasi za mwanzo kabla ya kuchapichwa ni sababu gani za msingi zilizofanya kukakosekana usahihi wa karatasi za kura kwa baadhi ya diwani?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sababu za msingi zilizocheleweshe *sample* kuja kwa wakati ni sababu za kiufundi ambazo zimetokana wakati wa uchapishaji. Vile vile hizo *sample* zilikosewa, kwa msingi huo ilipidi litokee tatizo hilo.

Suala la pili kuwa ni sababu gain za msingi zinazotokea na kusababisha kuchelewa au kutokea makosa ya katika kura zetu. Mhe. Spika, katizo kubwa kama nilivyosema awali, linatokana na masuala ya kiufundi. Pia wakati mwengine husababishwa na yule msimamiaji ambaye hutoka katika Tume ya Uchaguzi, anapokwenda pale kwa mchapishaji kutokuwa makini zaidi kwa kuhakikisha kwamba kura zile zinazochapishwa zinakuwa ni zile zile zilizokubalika.

Inapotokea kasoro yoyote msimamizi huyu kuwa na mapungufu ya aina moja au nyengine pale katika kiwanda, basi tatizo hilo hujitokeza. Kwa sasa na kupitia Tume ya Uchaguzi, tutahakikisha mtu anayekwenda pale kusimamia kura zetu ni aliye makini zaidi, awe na uwezo wa kutosha kuhakikisha kwamba kura hazipatikani na makosa na zifike hapa kwa wakati.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na ninaomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa wamekiri kwamba makosa yanayofanyika pengine husababishwa na kutokuwa makini kwa wafuatiliaji.

(a) Sasa hilo likitokezea kwa nini msimamizi huyo yeye halipii gharama hizo na baadae serikali iendelee kulipia gharama wakati ni uzembe wake msimamizi.

(b) Kwa kuwa mwanasiasa huyo aliathirika ambapo jimbo lake au wadi yake imeaghirishwa na kwa sababu amejipanga kwa ajili ya uchaguzi wa siku ile, kwa hivyo hatuoni kwamba serikali imesababisha watu wale kushindwa?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, juu ya jitihada yanagu ya kusikiliza katika spika yako hii, bado swali la pili sikulisikia vizuri. Mhe. Spika, bado tuna matatizo ya *echo*, kwa kweli ni tatizo kubwa ambalo linatusumbua. Kwa hivyo ningeomba Mhe. Mjumbe arudie swali lake la (b).

Mhe. Spika: Mhe. Hija Hassan Hija rejea swali lako la (b).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la (b) ni kwamba kwa sababu uchaguzi akuwa siku moja na wanasiasa wote wanajipanga kwa ajili ya siku hiyo, ikitokezeauchaguzi ukaahirika katika wadi fulani. Je, hatuoni kwamba serikali inasababisha watu wale kushindwa siku ya uchaguzi, kwa sababu tayari siku ambayo ni ya kujipanga imeahirishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba baadhi ya matatizo yanatokana pia na msimamizi wetu anayepelekwa kusimamia uchapishaji pale kiwandani. Wakati mwengine pengine shughuli zimemzidi akazidiwa kusimamia vizuri na matokeo yake yakawa hayo yanayotokea. Kwa sasa tutakachokifanya tutahakikisha kwamba tunampeleka msimamizi makini au ikiwezekana hata zaidi ya mmoja ili kuhakikisha makosa haya hayatokei.

Mhe. Spika, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi wote wa Zanzibar kwamba uchaguzi wowote utakaokuja kufanyika tena, basi tutahakikisha kuwa mapungufu haya yanaondoka na tufanye uchaguzi uliomzuri na wenye utulivu mkubwa, ahsante sana.

Nam. 24

Uchimbaji wa Mchanga Makaburini

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Mhe. Spika, swali langu Nam. 24 nililielekeza katika Afisi ya Waziri Anayehusika na Tawala za Mikoa, lakini kwa bahati mbaya limeletwa katika afisi inayohusiana na masuala ya mazingira, na kwa sababu linagusa mazingira. Kwa hivyo, kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anayehusika na mazingira anijibu. Lakini ikiwezekana kama Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa anaweza kutusaidia basi ningemuomba atusaidie ahsante.

Mhe. Spika: Ni kweli, ni utaratibu wa kawaida. Kama kuna swali limeingia huku na huku basi mawaziri wanaweza kusaidiana. Ni jana tu tulimuona Mhe. Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo akimsaidia Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa hivyo, ni jambo la kawaida, waziri akiona hivyo basi anaweza akasaidia.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, sasa naomba swali langu nambari 24 lijibiwe. Hivi sasa kumejitokeza tabia mbaya ya vijana kuchimba mchanga katika maeneo ya makaburi ya Mwanakwerekwe wakati wa usiku kwa njia ya kuchukuwa mchanga huo na kuuza. Kwa kuwa kitendo hicho kinasababisha kuyaacha mabaki ya miili ya maiti waliozikwa kuwepo nje na kuzagaa ovyo; na kwa kuwa kitendo kama hicho sio kizuri wala si cha kiungwana.

Je, Mhe. Waziri Serikali imechukuwa hatua zipi katika kukabiliana na vitendo hivyo viovu, hasa tukizingatia kuwa mara kadhaa vyombo vyetu vya Habari vimekuwa vikilisemea suala hili la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 naomba nikubaliane naye kuwa hivi sasa kumejitokeza tabia mbaya ya vijana kuchimba

mchanga katika maeneo ya makaburi ya Mwanakwerekwe wakati wa usiku kwa nia ya kuchukua mchanga huo na kuuza. Vitendo vyengine viovu ni kwa wananchi kujenga nyumba za kuishi katika maeneo hayo.

Aidha, naomba nilijuilishe Baraza lako Tukufu kuwa suala la uhifadhi wa uchukuaji wa maliasili zisizorejesheka (*None Renewable Resources*) kama vile mchanga na mawe unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mashirikiano ya karibu na Serikali za Halmashauri za wilaya ambao hutoa vibali vya uchukuaji na kukusanya mapato kutokana na maliasili hizo.

Hata hivyo, sheria Nam. 2 ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 1996 kifungu Nam. 98 imetoa adhabu kwa mtu yeyote atakayopatikana na hatia ya kuchukua maliasili hizo kuwa ni faini ya Shs. Milioni mbili (2,000,000/=) au kifungo kwa muda usiopungua miezi sita (6) pamoja na kutaifisha vifaa vyote vilivyotumika kufanya uhalifu huo vikiwemo gari au gari ya ng'ombe, ng'ombe mwenyewe, jembe, na pauro. Ili kuwakamata wahalifu hao ambao hufanya uhalifu huo nyakati za usiku, doria za pamoja zenye ulinzi madhubuti zinahitajika kwani wahalifu hao wanakuwa tayari kwa mapambano.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, inaendelea kushirikiana na Taasisi nyengine zikiwemo za Wizara ya Kilimo na Maliasili; Halmashuri ya Wilaya Magharibi, Jeshi la Polisi, Afisi za Kadhi Mkuu na Mufti wa Zanzibar na Kamisheni ya Wakfu ili kukabiliana na vitendo hivyo viovu vinavyoidhalilisha Nchi yetu.

Tarehe 20/12/2010, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira ilikutana na wadau hao kwa lengo la kujadili na kulitafutia ufumbuzi suala hilo. Mikakati iliyowejkwa kupitia kikao hicho, kwanza ni pamoja na kulitambua eneo hilo na baadae kulijengea kwa kulizungushia ukuta kwa ajili ya kulihifadhi. Vile vile kwa wale ambao wamelivamia eneo hilo kwa kujenga nyumba, mkakati uliowekwa ulikuwa ni pamoja na kuzibomoa nyumba hizo ambazo zimejengwa ndani ya eneo hilo la Mwanakwerekwe. Pia ni kutoa elimu kwa jamii juu ya ubaya wa vitendo hivyo.

Hata hivyo Mhe. Spika, ili tuweze kufanikiwa juu ya mikakati hiyo, mashirikiano ya dhati kutoka kwa kila raia wema, wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu yanahitajika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu

swali langu la msingi, alivitaja baadhi ya vifungu vya sheria, ambapo kama sheria inayohusiana na mazingira itavunjwa basi sheria itachukua mkondo wake. Swali langu liko hapa.

Je, Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kwamba kitendo cha kutokutekelezwa kwa sheria zilizowekwa, ambazo zimepitishwa na Baraza la Wawakilishi, kunasababisha vitendo hivi vya uharibifu wa mazingira viendelee?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kutokuwajibika kwa kusimamia utekelezaji wa sheria ambazo zinapitishwa ndani ya chombo chako hiki kitukufu ndiko kunakosababisha kuendelea kwa kufanyika vitendo hivi viovu ambavyo vinaizalilisha nchi yetu, sio hivi tu. Lakini tatizo hili tumeliona katika maeneo mengi, sheria zipo lakini hazifuatwi.

Mhe. Spika, wito wa afisi yangu ni kwamba taasisi zote zinazohusika na kusimamia sheria, tafadhali sana tunaomba sheria zisimamiwe, kwa sababu zipo na ni nzuri, ili tuweze kupata maendeleo na usimamizi mzuri wa rasilimali zetu.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, kwa kuwa uharibifu wa mazingira ni suala moja nyeti sana katika nchi yetu, naomba nikuulize swali moja kama ifuatavyo. Je, watu wangapi katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2011 wametiwa hatiani kwa kosa la uharibifu wa mazingira?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, data hiyo nitamletea kwa maandishi kwa sababu ipo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, baada ya maelekezo mazuri tuliyoyapata kutoka kwa Mhe. Waziri, mimi nina swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika eneo la Mwanakwerekwe ambalo watu wanaendelea kuzikwa, ni eneo ambalo inawezekana kwamba tuligaiwa siku moja, kwa upande wa dini ya wenzetu na dini yetu. Lakini eneo letu limekwisha kujaa kwa hivi sasa na imekuwa tunajirudia rudia na kuna ule utaratibu wa kuvamia lile eneo na ikawa lile eneo halitutoshi kwa hivi sasa.

Je, serikali kwa kupitia wizara yako, ina mpango gani wa kuongeza eneo kwa ajili ya kuzikana sisi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa kweli serikali imeona umuhimu wa kwamba sasa tayari eneo hilo lina tatizo na kutafuta eneo jengine mbadala kwa ajili ya shughuli ya kuzikia.

Mhe. Spika, kama tutakumbuka kwa wajumbe ambao walikuwemo humu, tuliwahi kuarifiwa kwamba serikali ya awamu ya sita iliunda kamati maalum kwa ajili ya kutafuta eneo la kuzikia ambapo ilikuwa chini ya Mwenyekiti wake waziri wa wakati ule Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili.

Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba serikali hii italiendeleza hilo kwa ajili ya kupata eneo mbadala.

Nam. 7

Utoaji wa Mikopo kwa Wanafunzi wa vyuo Vikuu

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Kwa kuzingatia kuwa kwa sasa kuna utaratibu wa kuwasaidia vijana wasio na uwezo kwa kuwapa mikopo ili waweze kumudu gharama za masomo hasa katika ngazi ya vyuo vikuu kwa masharti ya kujaza fomu na kuzilipia fomu hizo shilingi elfu thelathini.

(a) Je, wale ambao hawakubahatika kupata mikopo hiyo, hurejeshewa fedha hizo.

(b) Kwa mwaka 2009/2010, ni wanafunzi wangapi walijaza fomu za maombi ya mkopo na wanafunzi wangapi walibahatika kupata mikopo hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mhe. Spika, Mwanafunzi anaeomba mikopo kwa ajili ya kusoma katika Vyuo vya Elimu ya Juu hutakiwa kuwasilisha barua ya maombi wala sio kujaza fomu; akiambatanisha na vyeti vya kumalizia masomo, kitambulisho cha Mzanzibar na barua ya udahili kutoka chuo alichoomba. Kwa mfanyakazi anapaswa pia kuambatanisha na kitambulisho cha ZSSF na barua yake ya maombi ipitie kwa mwajiri wake.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na baada ya maelezo haya ninaomba kumjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna fedha wanazotozwa waombaji wakati wanapowasilisha barua zao za maombi ya mikopo. Gharama za 30,000/= zinatozwa kwa waombaji ambao maombi yao yamekubaliwa, ikiwa ni gharama za mkataba kati yake na Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu. Kwa maneno mengine malipo ya shs. 30,000/= hutozwa kwa wale ambao maombi yao ya udhamini yamekubaliwa.

b) Kwa mwaka 2009/10 jumla ya waombaji 976 waliwasilisha maombi yao, kati yao waombaji 625 walikubaliwa wakiwemo wanawake 215 na wanaume 410 na kupatiwa mikopo baada ya kuingia Mkataba na Bodi ya Mfuko na Elimu ya Juu. Ahsante sana

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize.

(a) Je, katika kila muhula mmoja serikali inatenga kiasi gani cha fedha ili kuwahudumia wanafunzi hao wanaosoma elimu ya juu.

(b) Je, mwanafunzi anayepata mkopo anapewa masharti gani, kulipa au anasamehewa?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Mhe. Spika, idadi ya fedha ambayo tunalipa kwa muhula mmoja, kwa hivi sasa nitakuwa sina nitamletea kwa maandishi.

(b) Mwanafunzi anayeomba mkopo ni wajibu wake baada ya kumaliza masomo, basi mkopo huo aurudishe. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuongeza majibu ya ziada kwa Mhe. Ali Abdalla Ali. Ni kwamba kikawaida fedha zinazotengwa ni kwa ajili ya kumlipia mwanafunzi kwa mwaka mzima. Kwa hivyo, inategemea kuna wanafunzi wangapi katika muhula ule, hivyo idadi ya fedha huwa zinatofautiana. Kutokana na hali hiyo, wizara inachofanya huwa inaomba bajeti

kwa ajili ya kugharamia masomo kwa mwaka ule, yaani inakisia wanafunzi watakaokwenda katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Kwa hivyo, pale inapofika wakati wa kuruhusiwa basi fedha zile huwa zinatolewa na kila mwanafunzi analipwa fedha zake za mwaka mzima na tunasubiri mwaka wa pili ili tuendelee kumlipa. Sasa akitaka hesabu ya mwaka gani na tumetumia kiasi gani basi hiyo anaweza kuipata.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza, pamoja na utaratibu huu wa kuwapatia mikopo kwa taarifa ambazo tunazoletewa na wanafunzi wengi wanaosoma vyuo vya juu ambao wanapewa mikopo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hivi sasa ni muda mrefu sana na wengine wanasema inafika miaka miwili, yaani *semesters* nne bado hawajalipiwa au hawajaingiziwa fedha hizi za mikopo ambazo waliruhusiwa. Matokeo yake wameshinda hata kupewa matokeo ya mitihani yao.

Kutokana na hali hiyo uongozi mpya wa wizara unachukua hatua gani kwa ajili ya kurekebisha kasoro hii kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wanafunzi wetu ambao wanasoma katika vyombo mbali mbali ndani na nje ya Tanzania.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli wanafunzi wetu ambao wanaomba mikopo na tayari wamejaza mikataba walikuwa na matatizo hayo wakiwemo wa ndani na nje ya Tanzania.

Lakini nataka kulifahamisha kwamba tayari matatizo hayo tumeyafuatilia na tumeshaanza kuyatatua. Kwa upande wa wanafunzi ambao wako nje ya nchi kama vile China, Ukraine na Uganda tayari tumeshaanza kuwalipia kwa awamu ya kwanza na kwa wale ambao wako ndani ya nchi tumeshazungumza na vyuo ambavyo wanasoma na baada ya muda mfupi malipo yao yafatuata.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, swali hili limechukua muda mrefu kidogo, kwa hivyo ninawaomba turidhike na hayo na tuendelee na swali linalofuata. *(Makofi)*

Nam. 16

Ongezeko la Maradhi ya Figo

Mhe. Salmin Awadhi Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa maradhi ya figo yamekuwa yakiongezeka hapa nchini na kupelekea wagonjwa wa maradhi hayo kufanyiwa upasuaji kwa kutolewa figo na kuingizwa figo nyengine.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa nini kumekuwa na ongezeko kubwa la ugonjwa huo.

(b) Hivi sasa kuna wagonjwa wangapi waliofanyiwa upasuaji na kuingizwa mafigo mengine pamoja na wale ambao wanaendelea kutumia dawa.

(c) Je, Mhe. Waziri mgonjwa aliefanyiwa upasuaji na kuendelea kutumia dawa hulazimika kutumia kiasi gani cha fedha kwa mwezi ili kununua dawa hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye vifungu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwa vile hakuna utafiti wa maradhi ya figo ulofanyika hapa Zanzibar ni vigumu kueleza moja kwa moja sababu za ongezeko la maradhi haya. Hata hivyo miongoni mwa sababu zinazopelekea kuathirika kwa mafigo ni matatizo ya moyo, matumizi ya baadhi ya madawa ya hospitali na za kienyeji, magonjwa ya kisukari na *pressure*.

Pia sababu nyengine ni maradhi ya njia za haja ndogo ikiwemo kuziba mkojo, vijiwe na kansa.

Kuanzia Juali 2009 hadi Juni 2010 jumla ya wagonjwa 119 wenye maradhi ya figo (*renal failure*) walitibiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wagonjwa watatu wamefanyiwa upasuaji wa kuekewa figo nchini India kupitia Wizara ya Afya. Inawezekana wapo wengine waliofanyiwa uwekaji figo kwa gharama zao.

Kwa wastani baada ya upasuaji huo gharama za dawa kwa mgonjwa ni shilingi milioni 30 kwa mwaka. Inaweza kubadilika kulingana na idadi na aina ya dawa zitakazohitajika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuwa wagonjwa hao waliofanyiwa upasuaji hutumia dawa kila siku katika uhai wao na kwa kuwa dawa zao wanazotumia ni ghali mno. Je, serikali inawasaidia vipi wagonjwa hawa.

(b) Kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yake ya Afya inao utaratibu wa kuwasaidia wagonjwa wa aina hizi na hata wale wagonjwa ambao wametokea Zanzibar. Hivi sasa wagonjwa wale wanazuiliwa kuchukua dawa kule Hospitali za Tanzania Bara na wala hawajui hatima ya maisha yao. Je, Mhe. Waziri wizara yako haiwaoneni huruma wagonjwa hawa na kuwafanya wajue hatima ya maisha yao.

(c) Serikali inampango gani wa kuanzisha Clinic ya Wagonjwa wa Figo kama vile ilivyo kwa Wagonjwa wa Kisukari.

(d) Tathmini ya maradhi hayo itafanyika lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Serikali kwa wale wagonjwa wanaopitia Wizara ya Afya na kama nilivyosema kwamba ni watatu, pia upo utaratibu wa kupitia wizara hiyo kwa ajili ya kufuatia matibabu yao na wakati wanaporudi wanaandikiwa na tunapeleka maombi yetu Wizara ya Fedha.

Sasa kama Wizara ya Fedha inazo fedha kwa kipindi kile itatupa na sisi tutampa, lakini kama hawana basi itakuwa hatuna la kufanya. Kwa hivyo, tunamueleza hali halisi na wakati zinapopatikana basi tunamjuilisha na kupewa fedha hizo za matibabu.

Kuhusu suali la Serikali ya Muungano kuwapatia madawa, Wizara ya Afya Zanzibar na Wizara ya Afya Bara ni wizara mbili tofauti pamoja na mipango tofauti. Isipokuwa kwa wale wagonjwa wanaoihusu Serikali ya Muungano wale wanakuwa na bima, kwa hivyo ikiwa maradhi yale yameshindikana kutibika hapa basi mgonjwa yule anapewa rufaa na kwenda bara na bima yake inamhudumia.

Wizara inayo mipango ya hivi sasa ya kutengeneza kitengo kinachohusiana na mambo hayo. Kitengo hiki kinahitaji wataalamu pamoja na vifaa vingi vya gharama kubwa. Lakini kwa vile Hospitali ya Mnazimmoja inatakiwa kuwa Hospitali ya Rufaa, basi hayo ni lazima yawepo.

Kwa hivyo, katika mipango ya kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja kuwa ya Rufaa, tunategemea kwamba Kitengo kinachohusiana na mafigo kitakuwepo na tathmini inaweza kufanyika mara tu baada ya kuwa na kitengo hicho, lakini kwa hivi sasa hatuna uwezo huo kwa sababu bado hatujaweza kufanya hiyo shughuli.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Spika, kunipa fursa hii kwa ajili ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa gharama za matumizi ya dawa kwa mgonjwa kama alivyosema takribani ni shilingi milioni 30. Je, mgonjwa humlazimu kuwa na kiwango gani cha fedha kwa shughuli yote kuanzia tangu kufanyiwa vipimo mpaka kupasuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mgonjwa mwenye maradhi ya figo kwanza inabidi itafutwe sababu na kama nilivyoeleza kwamba sababu zipo nyingi na kila sababu ina vipimo tofauti. Kwa hivyo, inatokana na sababu ipi iliyomfanya mgonjwa huyo kuwa na tatizo hilo. Nadhani hapo ndipo unapoweza kusema gharama ni ipi, kutokana na vipimo vipi vitakavyotumika, ili kuweza kujua hilo tatizo lenyewe pamoja na kufahamu hali halisi ya gharama.

Nam. 34

Upigaji Vita Uvuvi Haramu

Mhe. Hassan Hamad Omar - Alijibu:-

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na mpango wa kupiga vita uvuvi haramu katika maeneo ya bahari ya Zanzibar.

(a) Je, Wizara imejiwekea malengo gani katika vita hivi.

(b) Jitihada hizi zimefanikiwa kwa kiasi gani.

(c) Kwa kiwango gani, wavuvi wameelimishwa ili waweze kujiepusha na uvuvi huo haramu.

(d) Kuna mpango gani wa kuwatafutia wavuvi zana zinazofaa ili waweze kujiepusha na uvuvi usioruhusiwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, niwasifu sana wananchi wake wa Jimbo la Kojani kwa kuwa na umahiri mkubwa sana katika shughuli za uvuvi hapa Zanzibar.

Vile vile napenda niwapongeze sana wananchi wa jimbo hilo kwa kuwa na muamko mzuri katika shughuli za uhifadhi wa mazingira ya bahari yetu.

Sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejiwekea malengo yafuatayo katika kupiga vita uvuvi haramu katika maeneo ya bahari ya Zanzibar.

- Kuendelea kuishirikisha jamii katika ulinzi na usimaizi wa rasilimali za baharini.
- Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii ya ukanda wa pwani.
- Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010.

(b) Kupitia Kamati za Uvuvi katika shehia jamii zinashiriki kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali hizo, ikiwa ni pamoja na kufanya doria mbali mbali, na uhalifu umepungua kwa zaidi ya asilimia 80.

(c) Wavuvi wameelimishwa kwa kupitia njia mbali mbali, zikiwemo semina, mikutano, ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi, vipindi vya radio na televisheni, sanaa na mashindano ya vijana katika maskuli.

(d) Kupitia mradi wa *MACEMP*, wizara yangu imewapatia zana bora na endelevu wavuvi katika vikundi mbali mbali, ili waweze kujiepusha na uvuvi usioruhusiwa. Pia wizara imeweza kubadilisha mitego haramu kwa kuwapatia wavuvi mitego bora yaani "*gear exchange*" na ina mpango wa kubuni njia za kuweza kuendelea na programu kama hizi.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wavuvi wa Kojani katika masuala ya hifadhi ya mazingira wizara imewaandalia nini na imewaahidi nini.

(b) Hivi hapa Zanzibar wapo wavuvi ambao tayari wameshawahi kubadilishiwa vyavu zao na wizara.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kama nilivyosema awali kwamba wavuvi wa Kojani pamoja na wananchi wa Kojani kwa jumla katika siku za karibuni wameonekana kuwa na mwamko mkubwa katika shughuli za uhifadhi wa bahari yetu.

Vile vile wizara yangu inampango wa kuanzisha Hifadhi ya Eneo la Kojani kama vile ambapo tumeanzisha Hifadhi za Minai na Memka na Peka. Kwa hivyo, hivi sasa tunao mpango wa kuanzisha Hifadhi ya Eneo la Kojani na tayari tunafanya mazungumzo mazuri na yenye kuelekea kupata mafanikio baina ya wizara yangu na wananchi wa jamii ya Kojani katika suala hili.

Kutokana na hali hiyo, wakati wowote mazungumzo hayo yatakapokamilika na kwa msaada wake Mhe. Mwakilishi pamoja na viongozi wengine, basi suala la uhifadhi wa Eneo la Kojani litakamilika baada ya muda mfupi unaokuja.

Kuhusu mitego yoyote ambayo imebadilishwa. Kwa kweli kuna maeneo mbali mbali katika nchi yetu ya Zanzibar ambapo wizara yangu imeweza kuwabadilishia vyavu wavuvi baada ya kupata muamko wao wenyewe. Kwa mfano, katika Jimbo la Tumbe kuna nahodha Sharif Ali Sharif amepatiwa nyavu tano, Omar Said nyavu tano, Said Omar nyavu tano, Bakari Jabu nyavu tano, Mtumwa Hassan nyavu tano na Kibaya nyavu tano.

Vile vile kwa upande wa Jimbo la Kojani ambalo Mhe. Mwakilishi ndilo jimbo lake nahodha Hamad Dume amepatiwa nyavu tano, katika eneo la Mkoani nahodha Mussa Mahmoud amepatiwa vipande vinane.

Mhe. Spika, kwa upande wa Unguja eneo la Minai Kizimkazi Mkunguni vipande 18, Chukwani vipande 26, Memka jumla ya vipande 77 walipatiwa baada ya kubadilishana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kweli Mhe. Waziri amekiri kwamba uhalifu umepungua kwa asilimia zaidi ya 80. Lakini inaonekana kwamba uhalifu uliopungua ni kuwadhibiti wavuvi wadogo wadogo ndani ya nchi wa Unguja na Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza kutuambia uhalifu wa bahari kuu umepungua kwa asilimia ngapi hadi hivi sasa.

(b) Jitihada kubwa imefanywa na Idara ya Uvuvi ndani ya wizara yake, yakupeleka vifaa vya uvuvi kama vile maboti na mashine. Je, anaweza kutuambia jitihada hizo zimefanikiwa kwa kiasi gani na boti zile bado zipo au zimeuzwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba tumeweza kwa kiasi kikubwa kama nilivyosema katika jibu langu la swali mama, katika kudhibiti uharibifu wa mazingira katika bahari ya ndani. Lakini nikiri kwamba bado tunalo tatizo kubwa katika suala la bahari kuu.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumo mbioni kwa ajili ya kuandaa kikosi kikubwa sana cha doria ya bahari kuu, kuona kwamba suala hilo nalo tunalifanyiakazi na kuweza kulidhibiti kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Spika, wiki iliyopita wizara yangu ilikuwa na kikao na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa lengo la kulizungumza suala hili. Kwa kweli tumejenga mikakati kwa niaba ya serikali kuona kwamba rasilimali zetu zilizoko katika bahari kuu nazo zinalindwa ili ziweze kuhakikisha kwamba zinachangia ipasavyo katika uchumi wa nchi yetu.

Kuhusu swali la bodi ambazo wamepewa wananchi jinsi gani zimesaidia. Mhe. Spika, kwa kiwango kikubwa vifaa pamoja na boti ambazo wamepewa wavuvi wetu, kwa kweli zimesaidia sana kwanza ni kukwamua umasikini, vile vile kuongeza mapato yao binafsi na pia kuona sasa samaki wengi wanakamatwa baada ya kupewa vifaa hivi.

Kweli yapo baadhi ya maeneo machache vifaa hivi vimetumika visivyo. Lakini wizara yangu hivi sasa imo mbioni kufanya tathmini ya jumla kuona kwamba zana au vifaa vyote ambavyo wamepewa vikundi basi vinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa hivyo, kwa wale ambao ama wameviuza au wanavitumia kinyume na utaratibu basi sheria itachukua mkono wake.

Mhe. Thubeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba Zanzibar tunao wavuvi wengi ambao wamezunguka katika nchi yetu kama vile Kojani na sehemu nyengine.

Kutokana na nchi yetu kuzungukwa na bahari ambao ndani yake wamo samaki wengi na hasa bahari kuu na mpaka leo hii bado hatujaweza kuitumia na Mhe.

Waziri mwenyewe amekiri kwamba wapo watu ambao wanahujumu uchumi wetu kupitia bahari kuu, yaani mali au rasilimali zetu wanazichukua na sisi wenyewe tumekaa tu.

Kwa hivyo, ni lini hasa serikali itafanya mkakati makusudi wa kupata zana za kileo, ili wale samaki walioko bahari kuu tuweze kuwatumia na wananchi wafaidike kwa rasilimali zao kwa lengo la kupunguza umasikini.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kweli naomba nikiri kwamba nchi yetu ni kisiwa ambayo imezungukwa na bahari yenye utajiri mkubwa ambapo serikali bado haijaweza kuvuna rasilimali zilizomo baharini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako Mhe. Spika waniamini kwamba tunayo mipango madhubuti ya kuvutia wawekezaji katika eneo hilo.

Vile vile kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha na mwenyewe yupo na ananisikia kwamba tumeanza kuzungumza na wawekezaji kutoka nje ambao tayari wameshakuja na baadaye watakuja tena. Kutokana na hali hiyo, hivi karibuni tunayo imani kubwa sana watafanya uwekezaji mkubwa katika eneo la uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hapo basi wananchi wa Zanzibar wataanza hasa kufaidika na neema ya bahari kuu ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia. Kwa hiyo, naomba mtupe muda kidogo na tumo katika kujipanga na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafanikiwa. *(Makofi).*

Nam. 30

Serikali Kuvifuta Viwanja

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali kupitia Idara ya Upimaji na Mipango Miji hupima viwanja katika maeneo mbali mbali kwa mujibu wa *"Master Plan"* ya mji na baadaye serikali huwagawia wananchi kwa ajili ya kuviendeleza.

(a) Je, Mhe. Waziri, inakuwaje serikali kuamua kuvifuta viwanja hivyo baada ya muda mfupi tu, wakati baadhi ya wananchi wakiwa tayari wameshaanza kuviendeleza.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea kufutwa kwa kiwanja ambacho tayari kimeshatolewa na serikali kwa mwananchi ambaye ameshakiendeleza.

(c) Je, serikali hutakiwa ifanye nini kwa mwananchi kama huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vifuangu (a), (b) na (c) ikama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inaweza kufuta viwanja wakati wowote ule ikiona kuna sababu za kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 kifungu 55 na 56.

(b) Mhe. Spika, sababu zinazopelekea kufutwa kwa kiwanja ambacho kimeshatolewa na serikali kwa mwananchi ambaye amekwisha kiendeleza ni kutokana na eneo la kiwanja hicho kutakiwa itumike kwa matumizi ya kijamii au kiserikali.

(c) Mhe. Spika, kumlipa fidia mwananchi anayeathirika na kadhia hio kwa mujibu wa thamani ya soko (*market value*) pamoja na gharama alizotumia iwapo kiwanja hicho amekwisha kiendeleza.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Hivi Mhe. Waziri atakubaliana nami kama wizara yake imevamia na taasisi mbali mbali katika ujenzi wa holela hasa Mkoa wa Mjini Magharibi.

(b) Je, anao mpango gani wa kuhakikisha kwamba Mkoa huu ndio mama wenye kuleta nuru katika Zanzibar hii, ili kuhakikisha zile sehemu zilizobakishwa ndogo ndogo kuzilinda.

(c) Je, anaelewa kwamba kuna sehemu mbali mbali ambazo tayari zimeshamegwa kwa ajili ya kutolewa viwanja na hasa zile sehemu ambazo zimeachwa makusudi kwa lengo la michezo au watoto kujiburudisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi arejee tena sikulifahamu vizuri swali lake.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ameuliza kwamba wizara inajua kama imevamiwa na taasisi mbali mbali, jibu tunajua.

Swali jengine ameuliza kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi ni mkoa mama na huu wamevamia viwanja au maeneo mengi sana ninajua, nasema serikali kupitia Wizara yangu iko mbioni kuangalia uvamizi huu uliotokea na uvamizi huu sio kwa Mkoa wa Mjini Magharibi peke yake, uvamizi huu unafanywa Unguja na Pemba au Zanzibar nzima. Kufuatia agizo la Makamo wa Pili wa Rais kwamba hili suala tuliangalie na aliyenyang'anywa na aliyedhulumiwa tumpe haki yake.

Lakini pia tuna utaratibu wa kuendelea kuvifuta baadhi ya viwanja vilivyotolewa hilolela na kivamizi na viwanja hivyo tuviplani tena na tuwape wanyonge wanaohitaji kupata viwanja kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Mhe. Spika, ninaelewa kwamba yapo maeneo yaliyotengengwa kisheria kwamba ni maeneo ya wazi na kwamba wapo wananchi wanaovamia baadhi yao kwa kushirikiana na wafanyakazi wa wizara yangu, kuyapima maeneo hayo na kuyagawa kwa wananchi kiholela nasema jitihada tumeanza kuzichukua. Kufuta baadhi ya maeneo na tutaendelea kufanya hivyo kila tutakapogundua viwanja hivyo vimetolewa kiholela na hata kama kuna nyaraka zimetolewa lakini bado kwa mujibu wa sheria waziri wakati wowote anaweza kuvifuta viwanja hivyo, kama viwanja vimeendelezwa basi wizara au serikali itawalipa wananchi watakaofutiwa viwanja vyao fidia.

Lakini vile viwanja vinavyopimwa usiku usiku na kuendelezwa kujengwa usiku usiku hivyo vitafutwa na serikali haitalipa fidia *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja dogo tu la nyongeza.

Hivi Mhe. Waziri anaweza kutupa kwa maandishi maeneo au orodha ya maeneo hayo ambayo hayakutolewa kihalali au wanahisi yanahitaji kufutwa viwanja vyake, ili na sisi tukajua tusije tukajiingiza humo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati: Viwanja vilivyotolewa kwa namna hiyo ya ajabu ajabu ni vingi, kama anasisitiza nivilete kwa maandishi itachukua muda mrefu lakini tunafanya utafiti wa kupitia maeneo hayo. Hatutosubiri mpaka tumalize utafiti tutakachokigundua tutakichukulia hatua haraka hapo hapo, baada ya kumaliza shughuli hizi kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nitaleta taarifa hiyo barazani kwa faida ya wananchi waelewe yale matatizo yalivyotokea na vile yalivyoshughulikiwa.

Kwa hivyo namuomba aniachie niendelee na utaratibu niliupanga na utakapomalizika nitaleta taarifa hiyo barazani kwa maandishi.

Mhe. Spika: mimi nafikiri hili suala limechukua muda kidogo na nadhani kwa sababu bado maswali yamebakia mengi na muda mwenyewe unakimbia mno tuendelee na masuala mengine.

Nam. 22

Fedha za Mifuko ya Maendeleo Kupatiwa Wananchi Wote

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Kwakuwa lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwawezesha wananchi wake kiuchumi kupitia njia mbali mbali kama vile mfuko wa AK na JK; na kwa kuwa lengo la mfuko huo halikufanikiwa vizuri kwasababu baadhi ya majimbo kama vile Jimbo la Magomeni hakuna hata mwananchi mmoja aliyefaidika na mfuko huo.

Je, Serikali hii mpya ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa ina mipango ipi mizuri ilikuhakikisha kuwa wananchi wa majimbo yote ya Zanzibar, bila ya ubaguzi wanafaidika na mipango ya Serikali yao pindi inapoanzishwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu wa Saba imetoa kipaumbele katika suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lengo ni kuhakikisha kwamba shughuli za wananchi za kiuchumi katika majimbo yote ya Zanzibar zinaleta tija, kipato chao kinanyanyuka na maisha yao yanakuwa bora zaidi kwa kuweza kumudu mahitaji yao ya kila siku. Kuundwa kwa Wizara Maalum ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni kigezo kimojawapo kinachoonesha dhamira ya Serikali kwenye suala hilo.

Wizara hii ina jukumu la kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa kuhakikisha kuwepo kwa mazingira yatakayopelekea fursa zaidi za ajira, shughuli endelevu za kiiuchumi na kuimarika kwa kipato cha wananchi. Aidha, ina jukumu la kubuni, kupanga, kusimamia, kufuatilia na kutathmini programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Pia ina jukumu la

kutafuta rasilimali fedha na nyenginezo pamoja na mifuko maalum kwa ajili ya programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Miongoni mwa mipango ambayo imepangwa kutekelezwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ajira na Programu ya Kazi ambazo kwa pamoja zinalenga katika kukuza fursa za ajira rasmi na zisizo rasmi kwa lengo la kukuza kipato na kuimarisha hali ya maisha miongoni mwa wananchi.;

(b) Kuzifanyia mapitio Sheria za Kazi na kutengeneza Kanuni ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hizo;

(c) Kuandaa Sera na Mpango Mkakati itakayosaidia kutoa miongozo na kubainisha programu za uwezeshaji.

(d) Kuimarisha usimamizi wa mifuko ya mikopo ili iweze kutoa huduma bora zaidi na kuhakikisha urejeshwaji wa mikopo kwa wakati ili wananchi wengi zaidi waweze kufaidika;

(e) Kuwasiliana na washirika wa maendeleo ili kutafuta nyenzo kwa ajili ya programu za uwezeshaji ambazo, pamoja na mambo mengine, zitajihusisha na utoaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali hususan wadogo wadogo, kuanzisha vituo vya kutoa taaluma ya ujasiriamali na uanzishwaji wa maeneo ya biashara kwa wajasiriamali wadogo wadogo;

(f) Kuviimarisha vyama vya ushirika ili viweze kuwa chachu ya kuwainua wananchi kiuchumi; na

(g) Kuimarisha uratibu wa programu za uwezeshaji ili kuhakikisha watu wengi zaidi wanfaidika na programu hizi na kuondoa uwezekano wa programu hizo kugongana na hivyo kufaidisha wachache.

Mhe. Salmin Awadha Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, serikali ya awamu ya sita ambayo imeanzisha mfuko wa JK na AK wananchi walifarijika na walikuwa na matumaini makubwa juu ya mfuko huo, lakini jinsi muda unapokwenda inaonekana matumaini ya wananchi yanaendelea kufifia katika mfuko huo.

Je, Mhe. Waziri Wizara yake itayafufua vipi matumaini ya wananchi kupitia mfuko wa JK na AK.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:

Kwanza na taka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba lengo na adhma ya serikali hii ya awamu ya saba ambapo Mhe. Rais ameiunda wizara hii ni kuweza kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la kuwawezesha wananchi, kwa hivyo tayari tumeshajipanga kiwizara katika suala zima la mifuko ya JK na AK na pia kuandaa utaratibu mzuri zidi ambao wananchi utawapunguzia bughudha na uchereweshwaji wa kupata mikopo hiyo.

Lakini pia naomba Mheshimiwa aelewe pamoja na weheshimiwa wengine waelewe kwamba kulijitokeza matatizo katika mifuko hii, baadhi ya wananchi wengi wao walishindwa kulipa mikopo hii kwa wakati na wengine hadi hii leo hawajalipa kiwango chochote kile ambacho walihitajiwa kulipa kwa mujibu wa walivyokubaliana.
Kwa maana hiyo sasa hivi benki imezuia kwana hadi hapo utaratibu maalum utakapoandaliwa na tayari tunaanzisha mazungumza na benki ili kuweza kufanya utaratibu ambao utarahisisha zaidi wananchi kupata mikopo hiyo.

Kwa hivyo nawaombwa waheshimiwa wa Majimbo yote ya kuchaguliwa na kuteuliwa pamoja na wale wa viti maalum kuwatota wasi wasi kwa wananchi wao kwamba ishaala katika miaka mitano ijayo basi tutahakikisha kwamba tunawawezesha kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika pesa hizi za AK na JK wananchi ambao wamepata pesa hizi walikuwa na tatizo ambalo limewafanya wengi wao kushindwa kulipa pesa hizi na kuwafanya wale wengine kukosa nafasi ya kupata pesa hizi.

Je. Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha pesa zile zinalipwa ili wale wengine waliokuwa hawajapata waweze kupata.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu: -

HIli ndilo jambo ambalo sasa hivi tunaliandalia utaratibu kuhakikisha kwamba kwanza kuwapatia nyenzo, kwa sababu suala la ufuatiliaji ni tatizo kubwa sana ambalo limejitokeza kwenye wizara hii. Nimegundua kwamba tatizo sio kwamba wananchi hawana uwezo wa kulipa lakini ufuatiliaji ulikuwa ni hafifu na hii inatokana na kwamba wamekosa nyenzo za kuwafikia wananchi kwenda kuwafuatilia na kulipa mikopo hiyo.

Kwa hivyo tunajiandaa ili kuhakikisha tuna utaratibu mzuri wa kufuatilia na kuwafikia wale wananchi ambao walipata mikopo hiyo ili wazirejeshe fedha hizo na ziwanufaishe wengine, lakini pia nataka nimuhakikishie kwamba tumefanya mazungumzo na taasisi mbali mbali za kimataifa na nyenginezo za hapa nchini ili kuweza kupata fedha za kutusaidi, pamoja na serikali kuu tuna mufko ule wa uwezeshaji wananchi tutaomba kwa kushirikiana na Wizara ya fedha ili kuimarisha mfuko ule na wale waliokuwa hawajabahatika basi waweze kubahatika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa fedha hizi za JK na AK zililetwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kujiondolea au kujipunguzia kidogo umasikini, lakini fedha hizi zilikuwa na urasimu mkubwa kuzipata ndio sababu ya majimbo mengine fedha hizi wananchi wakakosa kuzipata.

a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama kunahitaji kupunguza urasimu ili hawa wananchi hizi fedha wazipate.

b) Fedha hizi kwa sababu zimeshaanza kutumika ni kiasi gani zimeshatumika na kiasi gani bado zipo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:

Katika jibu langu nilieleza kwamba tutahakikisha kwamba tunarahisisha utaratibu wa upatikanaji wa pesa zile za mikopo ya mifuko ile ya JK na AK.

Katika suala lililopita nilijibu kwamba tutafanya mazungumzo na benki ili kuona kwa kiwango gani tunaweza kukaa na kuwarahisishia wananchi mikopo ile ikapatikana kwa hakika.

Fedha kamili ambazo zimetolewa kwenye mifuko hii mpaka sasa hivi nitamletea kwa maandishi rafiki yangu.

Nam. 55

Marekebisho ya Katiba

Mhe. Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 yameitaja Zanzibar kuwa ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kifungu cha 2 na kifungu cha 2A cha Katiba hiyo kinampa uwezo Rais wa Zanzibar kuigawa Zanzibar katika mikoa ambapo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 Ibara ya Kwanza inasema Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano na Ibara ya Pili (Kifungu kidogo cha pili) kinasema kuwa Rais wa Jamhuri atashauriana na Rais wa Zanzibar kabla ya kuigawa Tanzania Zanzibar katika mikoa, Wilaya au maeneo mengine.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa Katiba hizi zinagongana.

(b) Kwa msingi huo wananchi wetu wafuate maelezo ya Katiba ipi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, yamezingatia zaidi maamuzi ya Wananchi wa Zanzibar kuhusu Mfumo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao kwa sasa ni wa Umoja wa Kitaifa; na utendaji wa Serikali hiyo utafanywa katika utaratibu utakao hakikisha kuendelezwa kwa Umoja Nchini na lengo la kufikia Demokrasia. Pia marekebisho hayo yamewekwa bayana hadi ya Zanzibar katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo historia inaeleza wazi kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeundwa na Nchi mbili zilizokuwa huru wakati huo ambazo ni Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika.

Mhe Spika, ni kweli kwamba kifungu cha Katiba ya Zanzibar kinampa uwezo Rais wa Zanzibar kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Ni kweli pia, Ibara ya 2(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, inampa uwezo Rais wa Jamhuri ya Muungano kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengineyo, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa upande wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kabla ya kuigawa Zanzibar katika Mikoa, Wilaya au maeneo mengineyo, alilazimika kushauriana kwanza na Rais wa Zanzibar..

Mhe. Spika, ni vyema tukafahamu kwamba, lengo kuuu ya Serikali ya Nchi yeyote duniani kwa kuigawa Nchi hiyo katika Mikoa, Wilaya au maeneo mengineyo ni kuweka utaratibu kwa kuratibu na kurahisisha utendaji wa Serikali kuu ya Nchi husika katika Mikoa, Wilaya au maeneo mengineyo kama itakavyoamua. Hivyo, kwa upande wa Zanzibar, majukumu yanayotekelezwa na Wakuu wa Mikoa au Wilaya ni yale yanayotokana na majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, katika utekelezaji wa Ibara ya 2 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wakati wote huo jukumu hilo likitekelezwa na Rais wa Zanzibar. Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kipindi hicho pia haijawahi kugharamia utekelezaji wa majukumu ya Mikoa au Wilaya za Zanzibar ikieleweka kwamba, Wakuu wa Mikoa au Wilaya wanatekeleza majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano hana mamlaka nayo.

Kwa mantiki hiyo ni dhahiri kuwa Rais wa Zanzibar ndie mwenye mamlaka ya kiutawala kwa upande wa Zanzibar na gharama zote za kiutawala zinagharimikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, kwa maelezo hayo yaliyotangulia naomba nimjibu Mhe Mwakilishi swali Nam. 55 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Katiba hizi mbili zinagongana kiuandishi, na hivyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano inapaswa kuangaliwa upya kwa lengo la kuondosha utata unaojitokeza hasa kwa kuainisha historia ya Nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kuainisha mamlaka na majukumu ya Serikali hizi mbili kulingana na Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa kila upande wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Kwa upande wa Mambo ya Muungano, Katiba inayopaswa kufuatwa ni ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; na mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar, katiba inayopaswa kufuatwa ni ile ya Zanzibar ya Mwaka, 1984 kama ilivyorekebishwa nyakati mbali mbali.

Kwa sababu suala la Tawala za Mikoa yaani shughuli za Mikoa na Wilaya kwa Zanzibar si mambo ya Muungano basi katiba ya Zanzibar ndio inayopaswa kufuatwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kama alivyouliza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kwamba kifungu cha 2(a) cha katiba ya Zanzibar kinampa uwezo Mhe. Rais kuweza kugawa Mikoa ya Zanzibar, lakini vile vile ibara ya kwanza ya katiba ya Jamhuri ya Muungano inampa uwezo Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar kuigawa mikapa ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hii inaonyesha kweli kuna mgongano wa kikatiba na sio vifungu hivi tu viwili katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katiba ya Zanzibar kuna baadhi ya vifungu vingi ambavyo vinagongana, lakini ukiacha hivyo hata hiyo katiba yenyewe ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna baadhi ya mambo ya Zanzibar hayatekelezwi kimuungano ambayo ni mambo ya Muungano.

Je, hivi sasa kuna mdahalo mkubwa ambao wenzetu vyuo vikuu bara wameanza kwa ajili ya mchakato wa kuanzishwa katiba mpya ya Tanzania. Je, kwa upande wa Zanzibar tuko kimya katika hili Serikali inawaambia nini wananchi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Kwanza ni vyema tukafahamu kwamba maamuzi ya wananchi ndio yanayopasa kutekelezwa na marekebisho haya ambayo yanamtaka Rais wa Zanzibar kugawa Mikoa ni maamuzi ya wananchi kwa kupitia kura ya maoni.

Lakini nataka nimueleze kwamba mambo mema yanapaswa kufuatwa ukitizama Katiba ya Zanzibar ya 1979 kabla ya marekebisho kifungu cha 2. Kilisema wazi kwamba Rais wa Zanzibar ndiye atakayegawa Mikoa na Wilaya katiba ya 79 ninayo na naweza kumpa *reference* hiyo, kwa hivyo maamuzi haya mazuri baadae yalibadilishwa na katika utendaji tukaona kwamba hayafuatwi kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano hafanyi zile shughuli zilizomo kwenye katiba yaani kushauriana na Rais wa Zanzibar, alikuwa ni Rais wa Zanzibar ambaye anafanya utaratibu huu.

Kwa maana hiyo wakati tunabadilisha katiba katika marekebisho ya 10 tukahisi kwamba ni vizuri yale mambo mazuri yaliyokuwemo katika katiba yetu ya mwanzo ya mwaka 1979 tuyarejeshe na wananchi wakakubali ndio maana tukakubali.

Lakini la pili ni kwamba hivi sasa kweli kuna mdahalo unaozungumzia marekebisho au kuanzishwa kwa katiba mpya ya Tanzania ni jambo zuri kwa sababu mbili.

Kwanza mdahalo huu utasaidia kuyaweka wazi yale matatizo yote ambayo yanaleta mgongano baina ya katiba ya Zanzibar na katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa hivyo ni vyema kwa Wazanzibar na sisi tukaanza mapema kujaribu kuainisha yale matatizo ambayo yanaleta mgongano huu kwa hivyo tukishakuanza mjadala huo na tukawa nayo tayari pale inapofika hatua ya kubadilisha katiba hiyo sisi Wazanzibar tutakuwa tuko tayari kwa yale mambo ambayo tunahisi yangeweza kuingizwa katika katiba ya jamhuri ya Muungano.

Kwa upande wa Wizara yetu tumeshaanza kazi hiyo tunajaribu kutizama ni maeneo yapi ambayo kwa Zanzibar yanaleta matatizo katika katiba ya Jamhuri ya Muungano, hivi sasa tumeshafanya kamati ndogo ambayo tunashughulikia kuyaainisha na tunakaribisha maoni kwa mtu yoyote kutuletea ili tuweze kuyaweka pamoja ili baadae tutapohitajika kuyafanyia kazi tutakuwa tunakwenda kwa kauli moja ya Wazanzibar.

Kwa hivyo ni wito wangu kwa ujumla kwamba utaratibu huu tuufanye ili tuweze kupiga hatua kidogo.

Nam. 27

Taasisi Kushindwa Kuhudhuria Kwenye Vikao

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo kuu la *ZIPA* ni kuifikisha nchi yetu katika mustakbali mzuri wa dhana ya kituo kimoja cha uwekezaji *One Stop Center* na kwa kuwa dhana hii imekuwa ngumu kufikia lengo lililokusudiwa kutokana na wakuu wa taasisi au vitengo husika kushindwa kushiriki katika vikao ambavyo huhitaji maamuzi yao; na kwa kuwa kutoshiriki kwao kunazorotesha au kuyumbisha kwa baadhi ya maamuzi, jambo ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya nchi.

(a) Ni sababu zipi zinazopelekea Taasisi au Vitengo husika kushindwa kuhudhuria kwenye vikao mbali mbali vinavyoitishwa.

(b) Je, Mhe. Waziri, utakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika wa kuwawajibisha wale wote wanaoshindwa kushiriki katika vikao hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu**:-**

Mhe. Spika**,** kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwanza napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, dhana ya kituo kimoja cha uwekezaji *One Stop Centre* inalenga katika kuharakisha utoaji wa huduma mbali mbali zinazohitajiwa na Mwekezaji, ili shughuli zinzokusudiwa kufanywa zipatiwe maamuzi ya haraka bila ya kuathiri taratibu za kisheria za nchi.

Mhe. Spika, katika kufanikisha dhana hii, Serikali iliamua kuwa taasisi zote zinazohusika moja kwa moja na maamuzi yanayohusu uwekezaji, kuweka maafisa wake katika ofisi ya Mamlaka ya Uwekezaji *ZIPA.* Lengo la uamuzi huu ni kuona kwamba shughuli zote zinazohitaji maamuzi kutoka taasisi mbali mbali za Serikali, zinapatiwa uamuzi ya haraka, bila ya usumbufu na kwa muda mfupi iwezekanavyo.

Mhe. Spika**,** ili dhana ya *One Stop Centre* iweze kutekelezeka, ni dhahiri kwamba maafisa wanao wakilisha taasisi zao katika Kituo cha Uwekezaji *ZIPA,* wanahitaji kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi kwa mujibu wa utaratibu wa taasisi wanazoziwakilisha.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi , kwa ruhusa yako , sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, maafisa wanaoziwakilisha taasisi za Serikali kama vile, Idara ya Ardhi, Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi, Kamisheni ya Utalii n.k. wanafanya kazi ndani ya *ZIPA.* Maafisa hao hushiriki vikao vinvyohusika. Kinachokosekana kwa baadhi ya mambo ni uwezo wa kufanya maamuzi kwa maafisa hao. Upungufu huo wa uwezo wa kufanya maamuzi hupelekea maofisa hao kuwa na kazi ya kukusanya matatizo ya wawekezaji na kuyawasilisha katika Taasisi zao kwa maamuzi. Utaratibu huu unapelekea ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi badala ya urahisishaji. Hivyo, kupelekea malalamiko na kupotea kwa dhana nzima ya *One Stop Centre.*

b) Mhe. Spika, kutokana na maelezo yangu niliyoyatoa, hakujitokezi haja ya kuwawajibisha maafisa kwa kushindwa kushiriki vikao. Kinachotakiwa na ambacho ofisi yangu itakisimamia ni kuona kuwa maofisa wote wanaopelekwa kuwakilisha taasisi zao wanapewa uwezo na kufanya maamuzi yanayohitajika, ili dhana ya *One Stop Centre* ifanye kazi kama inavyotarajiwa.

Mhe. Spika: kabla ya kuuliza swali hebu nitoe ushauri mmoja kwa sababu muda umemalizika zimebakia dakika kama mbili tu ambazo pengine tukishamaliza kuuliza swali muda utakuwa umekwisha na Waziri atakuwa hana nafasi.

Jana tuliacha maswali kama matano (5) kufuatana na ukubwa wa maswali na wingi wa maswali ambayo Waheshimiwa Wajumbe waliyauliza. Leo baada ya suala suala hili ambalo hata swali la nyongeza halijaulizwa muda umeshamalizika. Ningeshauri Waziri atoe hoja tuyamalize maswali haya ili mwisho wa kikao chetu iwe maswali tumeyamaliza au kuyapunguza kwa kiasi kikubwa. Nimuombe Mhe. Waziri wa nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais atoe hoja ya kutenga Kanuni kando, Kanuni ya 40 kifungu kidogo cha (3) cha Kanuni hiyo ili kuweza kuongeza muda wakuuliza maswali, tupate kuyauliza maswali haya na tuone kama wajumbe wanakubali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu iweke kando Kanuni ya muda wa maswali ili maswali yaliyokuwemo katika Order paper ya leo yaweze kuendelea na tuweze kumaliza.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mhe. Salmini sasa tuendelee na swali la nyongeza.

Mhe: Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa lengo la serikali la kuanzisha kituo kimoja cha uekezaji yaani *One Stop Center* ni kuharikisha maamuzi juu ya masuala mazima ya uekezaji. Na kwa kuwa Mheshimiwa amekiri kwamba maafisa wanaofika katika kituo kile ni maafisa ambao hawana maamuzi. Inaonekana ni dhahiri ni kwenda kinyume na lengo la Serikali lilivyokusudiwa katika kuleta maendeleo ya nchi.

Je, Mhe. Waziri kwa kuwa lengo la serikali katika kutoa maamuzi hara halifikiwi wizara yake ina mtazamo gani juu ya jambo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa lengo la kunzishwa hichi kituo ni pamoja na kuwapa uwezo maafisa hawa kuweza kufanya maamuzi na kutekeleza kwa haraka iwezekanavyo. Kilichojitokeza ni kwamba maafisa wanaopelekwa pale hawana uwezo wa kufanya maamuzi hayo. Kinachoonekana ni ku-*compile* matatizo na kuyawasilisha katika taasisi zao, baadae taasisi ndio zinazotoa maelekezo.

Wizara yangu inachokiangalia kwa hivi sasa ni kuzipitia sheria hizi, ambao maafisa wao wapo pale *ZIPA* na kuzifanyia marekebisho kwa kushirikiana na wizara husika ili maafisa hawa wawe na uwezo wa maamuzi au mapendekezo watakayoyatoa pale *ZIPA*.

Nataka niseme Mhe. Spika, na vile vile nataka niwapongeze sana Wizara ya Ardhi tayari afisa wa ardhi aliyekuwepo pale mapendekezo anayoyatoa yanafanyiwa kazi hana haja tena kurudi wizarani. Tutafanya hivyo hivyo na kwa Wizara ya Kazi, Uhamiaji na taasisi nyengine. Naomba vile vile Waheshimiwa Mawaziri waliyokuwepo hapa wakubaliane nami ili tuweze kufanikisha ile dhana nzima ya *one stop center.*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kama alivyokiri kwamba *ZIPA* ndio kitengo ambacho kingewakaribisha wawekezaji lakini usumbufu wanaoupata wawekezaji unatokana na kuchelewa kwa maamuzi.

(a) Je, kwa kuwa kitengo hiki kimerejeshwa tena Wizara ya Fedha na yeye ndiye alichonacho. Umeipanga vipi Wizara ya Fedha kuondoa usumbufu huu kwa wawekezaji.

(b) Ardhi na ruhusa ya *ZIPA* kipi kinachofuata mwanzo, kuna baadhi ya wawekezaji hupewa ardhi mwanzo na hawajapata ruhusa ya *ZIPA* na kuna usumbufu huu. Je, usumbufu huu au tatizo hili limekabiliwa vipi na wizara yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:

(a) Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie kwamba maamuzi yatatoka na yatapatikana kwa haraka zaidi pale tutakapoweza kuzifanyia marekebisho sheria zinazohusiana na maeneo yote ambayo

muwekezaji anayahitajia, ikiwa ni pamoja na sheria ya *ZIPA*. Hivi sasa sheria ya *ZIPA* tunaipitia upya na tunatarajia tutaiwasilisha katika kikao hiki.

(b) Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hivi sasa kuna utata kidogo kwamba. Muwekezaji ananza kwenda kutafuta ardhi, anaingia mitaani, haelewi mipango ya ardhi ile ikoje. Anapokuja *ZIPA* anasema tayari ninayo ardhi. *ZIPA* inapowasiliana na vitengo vya ardhi inaonesha kwamba mipango ya ardhi ile sio ile ambayo muwekeza anataka kuwekeza.

Tunachokisema sisi muwekezaji kwanza apate taratibu, apate *certaficate* ya *ZIPA* halafu baadaye *ZIPA* ndio itamsaidia katika hatua za kupata ardhi. Sisi ndio tunaoelewa ardhi hii imetengwa kwa ajili ya shughuli gani.

Nam. 1

Uchakavu wa Meli ya MV Maendeleo

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Kufuatia tukio la kuharibika kwa meli ya MV. Maendeleo hivi karibuni wakati ikifanya safari ya kutoka Unguja kwenda Pemba na hatimaye Mhe. Waziri Kuchukua hatua thabiti ya kuzuia meli hiyo kuendelea na safari ya kurudi Unguja.

(a) Je, wizara haioni haja ya kuiuza kabisa meli hiyo isiendelee kutoa hduma kutokana na ukweli kwamba imechakaa sana na kuendelea kutoa huduma za usafiri ni hatari kwa abiria na mali zao.

(b) Kwa kuzingatia ukweli kuwa Shirika la Meli lipo katika hali mbaya kifedha na kuwa limekuwa mzigo mkubwa kwa serikali, kwa nini Shirika hilo lisivunjwe na kuipa sekta binafsi fursa zaidi ya kuendelea na utoaji wa huduma hizo za usafiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 lenye lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kwali kwamba meli yetu ya MV. Maendeleo imechakaa lakini kwa muda huu bado haijawa muda muwafaka wa

kuiyuza meli hii hadi hapo serikali itakapoweza kununua meli nyengine ya kuweza kuwahudumia wananchi wa Zanzibar.

Ni kweli kuwa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alichukua hatua ya kuizuia meli hiyo wakati ikifanya safari ya kwenda Pemba kutokana na hitilafu zilizojitokeza kwa wakati huo. Napenda kulitaarifu Baraza lako tukufu kwamba meli hiyo imerejea nchini ikitoka Mombasa kwenye matengenezo na ipo nangani kwa kusubiri hatua za kwanza za safari zake za kawaida.

(c) Mhe. Spika, Shirika la Meli lipo katika hali mbaya kifedha na kuwa limekuwa mzigo kwa serikali yetu. Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwa hivi sasa linajiendesha wenyewe kwa ushahidi kama ifuatavyo:-

(i) Shirika kwa hivi sasa linaendesha shughuli zake zote bila ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

(ii) Shirika linamudu kulipa madeni yake yote ya Chelezo na ununuzi wa vipuri na matumizi mengine ya uendeshaji bila ya kuathiri kazi nyengine za utendaji na uendeshaji wa shirika hilo. Aidha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendelea kumiliki meli zake inapelekea kuwadhibiti wafanyabiashara wa vyombo vya baharini pamoja na huduma za usafiri na kuwajenga imani raia wa Zanzibar kwa serikali yao.

Zanzibar tokea asili serikali yetu ilikuwa ikimiliki meli zake, hivyo serikali kupitia wizara yangu haina budi kuendeleza utaratibu huu mzuri na wenye tija kwa maslahi ya wazanzibari.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo:-

Shirika la Meli tayari limeshakwisha uza meli ya Mapinduzi pamoja na meli moja ya mafuta kwa kipindi kirefu na waliahidi huko nyuma kwamba wakishakuuza meli hizo wataongeza na fedha walizonazo wanunue meli za kisasa ili ziweze kuingia kwenye ushindani wa kibiashara.

(a) Je, wazo hilo lingalipo au limeondoka.
(b) Kama limeondoka ni kwa sababu zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeweza kuuza meli yake ya MV. Mapinduzi kutokana na uchakavu kwa wakati huo. Madhumuni ya kuuza meli hiyo ilikuwa kwa mnasaba wa kutengeneza *Phase***.** Kwa hivi sasa meli ya MV. Ukombozi haijauzwa nayo imekodishwa kwa Shirika la *OPEC* kwa ajili ya kuleta mafuta nchini. Kukodishwa huko kunaisaidia serikali kupata mapato ya kodi ya kuendeshea shirika.

Madhumuni na Mipango ya Wizara yetu ni kuhakikisha fedha zilizouzwa MV.Mapinduzi kushirikiana na wadau wahisani, mpango wa kununua meli ya kisasa upo pale pale.

Mhe. Salum Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni muda mrefu sasa Shirika la Meli ukiangalia shughuli zake tumeshuhudia hasa kuwa imekuwa inafanya shughuli zake chini ya uwezo na tulikuwa tukipendekeza ama livunjwe au kufanywe mabadiliko ya aina yoyote.

Shirika hili kwa kadiri ninavyoelewa moja katika mambo ambayo yanachangia upatikana wa fedha na Katika Mamlaka yao ni meli mbili hizi za serikali zilizokuwepo pamoja na ya mafuta. MV. Mapinduzi imeshauzwa na MV. Maendeleo toke mwaka 2003 nilipokuja hapa inatengenezwa akirudi inatia hasara, mpaka inakodishwa ikirudi lakini serikali inashindwa kuiendesha wenyewe.

(a) Shirika hili limefanya miujiza gani ya kiutendaji mpaka sasa linajipata matumaini wakati ilipokuwa na vyombo vizuri vilivyokuwa vipya ilikuwa halijiendeshi vizuri.

(b) Mhe. Spika, tumo katika hali mbaya ya usafiri kutokana na kutokuwa na meli za kutosha. Ushauri ni kuwa wasafiri wanatoka Pemba Bandari ya Wete kuja Unguja huwa wanajazana kiasi ambacho wanafika hapa kwa kadiri ya uwezo wa Mwenyezi Mungu tu lakini hali ile sio hali ya kuvumilia.

Shirika kama kweli limeshajipanga na lina uwezo wa kujiendesha. Linafanya utaratibu gani wa kutafuta meli ambayo itarahisisha na kufanya usafiri wa salama baina ya Unguja na Pemba ambapo hivi sasa hali ni mbaya sana.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kweli hakuna miujiza iliyofanyika hadi shirika la meli kubadilika kuwa lilikuwa halina uwezo na hadi sasa kuwa na uwezo isipokuwa ni kujipanga upya.

Wametambua makosa yao ni yapi wamejirekebisha na hapa ninaushahidi kwamba kweli watajirekebisha kutokana na meli ya MV. Maendeleo peke yake faida inayoingiza kuanzia Juni 2010 mpaka Disemba 2010 na kwamba walikuwa na faida ya milioni 108.

Jengine ni kwamba Mhe. Salim alitaka kujua kuna mpango gani wa usafiri wa abiria hasa kutoka Wete kuja Zanzibar kwa namna ambavyo wanajazana kwenye vyombo.

Mhe. Spika, kwanza serikali ina sera maalum ya kushajihisha wawekezaji binafsi moja katika nyanja mbali mbali moja ikiwa ni usafiri wa baharini. Hivi sasa tuna meli zaidi ya nane (8) za wawekezaji binafsi ambao wanafanya safari zao Pemba/ Unguja, Unguja /Pemba. Tatizo la kujazana katika meli watu wengi sana ni utaratibu ambao mimi naona ni donda ndugu.

Mhe. Spika, ni mashahidi nyote kwamba kwa usafiri wa Unguja Pemba, Pemba Unguja zinakatishwa tiket kwa mujibu wa uwezo, uwezo ambao kila chombo kinapewa. Mfano meli ya MV. Maendeleo inatakiwa ichukue abiria 750, mwenye meli atakatisha tiketi ya watu 750. Mwenye meli atakatisha tiketi ya watu 750 lakini anayekata tiketi kwa utaratibu wa Unguja /Pemba, Pemba/ Unguja anakwenda na watoto wake watatu kawakamata mkono. Sasa hiyo sio idadi ya 750 tena. Na ukimwambia hawa watoto wasiende anakwambia basi na mimi siendi. Sasa hili ni tatizo lete wenyewe.

Kwa hivyo kujazana kwa meli kwa watu wengi sio suala kwamba meli wanakata tiketi za ziada, lakini ni utaratibu tuliouzoea miaka nenda miaka rudi huu unataka uamuzi wa serikali kwamba hata watoto wadogo na wao watoleshwe tiketi ili ionekane kabisa kwamba wanaokata tiketi ndio wanaoingia melini peke yao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, atakubaliana na mimi kuwa kuna muwekezaji au kuna tajiri ambae alikubaliana kutengeneza meli nyengine katika nchi ya South Afrika. Je, wamefikiana vipi katika kutengeneza meli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli serikali ilikuwa ina utaratibu wa kujenga meli mpya, lakini baada ya kutafakari vizuri serikali imeona ni vyema tukafanya uchambuzi yakinifu na kuanza kutafuta utaratibu mwengine utakaoweza kujenga meli nyengine yenye gharama nafuu, yenye tija na uwezo wa kukizi mahitaji halisi kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, kwa kuwa jana Mhe. Waziri alitoa ufafanuzi juu ya ujenzi wa sehemu ya kukalia abiria kwenye Bandari yetu ya Malindi pamoja na kwenye makontena kwa hivyo naomba swali hilo kuliondoa.

Mhe. Spika: Swali limeondolewa na Mhe. Mjumbe, tunakushukuru sana kwa kutusaidia muda. Maswali yamemalizika, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe. Tuendelee na shughuli zinazofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Aliyoitoa Katika Uzinduzi wa Baraza la Nane la Wawakilishi Zanzibar Tarehe 11 Novemba, 2010

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shain kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 84 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 alilihutubia Baraza la Wawakilishi mnamo tarehe 11 Novemba, 2010.

Mhe. Spika, hotuba hii ya Mhe. Rais imekusudia iwe ndio dira ya utendaji wa kazi ya Serikali ya awamu saba katika miaka mitano ijayo. Dira hii inaendana na malengo ya Mapinduzi yetu matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964 ya kuleta maisha bora na ustawi kwa wananchi wote.

Mhe. Spika, kwa kuwa hotuba hii ilikuwa ni hotuba nzito, iliyopewa muelekeo wa utekelezaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo ya Umoja wa Kitaifa. Ilijaa maneno ya busara, upenda na matumaini kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla. Muongozo wetu mkubwa utakuwa ni utekelezaji wa ahadi zetu kama zilivyo katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010/2015.

Mhe. Spika, maeneo makubwa ambayo Mhe. Rais aliyagusia katika hotuba yake ni saba.

1) Mhe. Rais alizungumzia vipa umbele katika awamu yetu hii ya saba. Vipaumbele hivyo aligusia suala zima la kazi ya kukuza uchumi, majukumu ya kimsingi yaliyo mbele yetu ambayo aliyaainisha kwamba ni:

    - Mapinduzi ya Kilimo,
    - Mapinduzi ya Ufugaji,
    - Mapinduzi ya Uvuvi,
    - Mazingira, Maliasili,
    - Kukuza ajira nchini na
    - Kupambana na Umasikini.

2) Sehemu ya pili ni suala zima la kuimarisha Miundo Mbinu. Hapo alizungumzia haya ya kuimarisha usafiri wa Anga. Alielezea kwa ufupi hali ilivyo hivi sasa na changamoto ziliopo mbele yetu. Suala zima la Bandari na hali ya umeme.

3) Jengine ni suala la huduma za kijamii, alizungumza zaidi suala la elimu, kumbukumbu za kale, maji, afya, makaazi, michezo na vyombo vya habari.

4) Fungu la hili Mhe. Raisi alilizungumza kwa urefu ni suala la kuyaendeleza makundi mbali mbali yakiwemo makundi ya wanawake, watoto, walemavu, vijana, wazee na wafanyakazi kwa ujumla.

5) Kifungu hiki amezungumzia kuwepo kwa amani na usalama nchini mwetu. Hapa ikizingatiwa suala la maadili kwa viongozi na wananchi kwa ujumla.

6) Suala la demokrasia na utawala bora. Haki mahakamani, umuhimu wa kuwepo Afisi ya BTT na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu katika utendaji Serikalini na kwenye mashirika yetu.

7) Mwisho eneo kubwa ambalo aliliwekea kipa umbele ni suala la uhusiano wa Kikanda na Kimataifa.

Mhe. Spika, kwa kuwa hotuba hii ni miongoni mwa nyenzo muhimu kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza majukumu yao na kwa kuwa kuna haja kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuijadili, kuizingatia na kuitafakari kwa kina hotuba hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inafanyiwa kazi kwa ukamilifu na kwa umakini.

Mhe. Spika, hivyo basi kwa mujibu wa kifungu cha 30 (3) na 22(12) vya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi naomba kutoa hoja kuwa hotuba hiyo ya Mhe. Rais sasa ijadiliwe na Baraza lako tukufu.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja iamuliwe)

Mhe. Spika: kabla ya kujadili hoja niwaombe wale wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala watoke hivi sasa ili waende kuendelea na shughuli yao ya kuchambua Mswada wa Utumishi wa Umma. Wajumbe wote waende kwenye chumba chao kile kile ambacho walichokuwa wanafanyia shughuli hiyo. Naomba sana waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru leo hii kunipa nafasi ya mwanzo katika kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Kwanza nataka nimshukuru Mhe. Rais kwa kutuchaguliwa Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili.

Mhe. Spika, hotuba hii kama alivyoeleza Mhe. Waziri Afisi ya Rais kuwa ni nzito na inataka utulivu mzuri hasa amelenga kutokana na sheria ambazo imempa mamlaka hiyo ya kuweza kuhutubia Baraza kama vilivyoeleza vifungu vya kanuni na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa kuanza kuchangia naazia katika ukurasa wa 25 kuhusu Mapinduzi ya Uvuvi. Mhe. Spika, leo hapa tulimsikia Mhe. Waziri wa Uvuvi alieleza malengo mazuri sana na mahitaji ambayo yaliyokwisha kutekelezewa wananchi. Pia alielezea tahadhari ya kuharibu mazingira ya bahari. Nafikiria kwamba wananchi wameshaelewa kuhusu uharibifu wa bahari. Mimi hilo nakubaliana nalo na wengine sasa hivi tayari wameshaondosha hizi nyavu ambazo zinaharibu matumbawe.

Mhe. Spika, pamoja na hayo ningeomba kwamba kuna mambo mengine ambayo Mhe. Rais huyazungumza lakini mengine inakuwa sisi Waheshimiwa inatupasa tuyachangie ambayo yale Mhe. Rais ameyasahau na sisi tunayaona kuwa yataweza kusaidia kuinua uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nakuja katika suala la uvuvi wa juu, nikimaanisha nini maana ya uvuvi wa juu. Wenzetu sasa hivi katika nchi za Kenya hata Tanzania Bara wameshaanza shughuli hizo za kuwatafutia wananchi wao kwa kuwaondolea umasikini kwa njia ya uvuvi wa juu. Mhe. Spika, wamejengewa mabwawa, wameshajihisha vizuri sana na hivi sasa utakuta asilimia kubwa

tayari wanavyo vianzio hivyo ili uchumi wao uweze kuinuka haraka haraka sana.Mhe. Spika, sisi bado suala hilo hatujalianza hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kama atakubaliana na mimi suala hilo nilijaribu kumdokolea na kumueleza, lakini kwa kuwa Mhe. Waziri ni msikivu basi yuko tayari kama ikiwa ile hali tayari ameshafikia baadaye atakuja kunieleza hali halisi ambayo ameshafikia katika wazo hilo nililompa. Mhe. Spika, kuwakusanya vijana kuwapeleka katika bahari kuu kwa hivi viboti ambavyo ni vya kizamani, hilo ni kuhatarisha maisha kwa sababu leo samaki huwezi kuwapata katika bahari ya karibu lazima uende kwenye bahari ya juu.

Mhe. Spika, kwa hivyo ni kuwatafutia vyombo ambavyo Waziri ameeleza, hilo tunakubaliana nalo lakini na hili namuomba kwa makusudi kabisa aweze kutafuta sehemu ambayo wataalamu wataweza kusema hapa ufugaji wa samaki unawezekana. Kwa hivyo, naomba hili suala lipewe kipaumbele kabisa ili tuweze kuondokana na umasikini sisi na wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa kuendelea katika ukurasa wa 27 kuhusu suala la mazingira. Mhe. Spika, hili suala la mazingira sasa hivi limekuwa ni kubwa sana. Leo hapa nimemsikia Mhe. Waziri amelieleza vizuri sana, lakini kuna mambo lazima tumsaidie Waziri. Mhe. Waziri alizungumza suala la utoaji wa vibali katika masuala ya misitu na hata masuala ya uchimbaji wa mchanga. Hivyo basi namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kwa upeo kwani sasa hivi kuna mbinu zinafanyika.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo kama hawa watu wa misitu na mazingira ndio wenyewe wahusika wanaotoa vibali. Lakini kuna baadhi ya mambo wamefilisiwa na sehemu za halmashauri. Kwa mfano, kuna Halmashauri yetu ya Kaskazini ‘B’ hili niliseme tu wala sitalifumbia macho. Mhe. Spika, leo Halmashauri ya Kaskazini ‘B’ ndio inayopanga, wakati wao si wataalamu. Zamani ilikuwa ukitaka kuchimba mchanga lazima uende Idara ya Misitu na wao wanakaa pamoja na watu wa Mazingira hapo ndipo kibali kinakubalika. Leo utakuta panachimbwa mpaka kunatoka udongo sijui ni wa aina gani inakuwa haupatikani ule udongo wa kuweza kurutubisha ile ardhi ikapata kuja juu.

Mhe. Spika, mimi ningeomba utaratibu ule ule urejeshwe kwa mujibu wa sheria wapewe wenyewe, sio halmashauri ikae kule iseme kwamba tunasema eneo letu hili na watu wa misitu kwa kuwa wanaiogopa halmashauri na wao wakakubali tu na wakajisahau wajibu wao. Mhe. Spika, ni kwamba sheria irudi pale pale mimi naomba hili suala lirekebishwe ili kuleta ufanisi mzuri na kukomesha mazingira mabaya.

Mhe. Spika, pia Mhe. Waziri alikiri hapa kwamba mapungufu ni kuwa sheria hazitekelezwi, hili ni kweli. Mhe. Spika, kwa kumsaidia Mhe. Waziri juzi Makamo wangu wa Pili alikwenda kuna sehemu moja kule Kazole ambayo watu wanachimba mchanga. Mhe. Spika, ni kwamba kuna hawa polisi unapomwambia kwamba gari imeshaingia pahali fulani na tayari inachimba mchanga kinyume na sheria basi polisi anachelewa kwenda kwa wakati ule. Hilo nalo naomba lifanyiwe mkakati mzuri sana, tuwaambie vyombo vyetu hivi vya usalama kuwa vinapopata taarifa waweze kufika kwa wakati unaotakiwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na ukurasa huo huo kuna ukuzaji wa ajira. Mhe. Spika, hili suala la ajira kwa wananchi wetu, kama tunavyosema kuwa vijana ni wengi wenye uwezo wa kufanya kazi. Kwa mfano, suala la kilimo kijana hawezi kuvutiwa, hilo kweli tukubaliane tusifichane, na kwa sababu gani? Mhe. Spika, leo ukitaka kushajihisha vijana walime hiyo ardhi yenyewe iko wapi.

Mhe. Spika, ardhi ya kulima haipo na nyenzo hatuna za kuwapa kwa hiyo kijana huyo atashawishika na nini. Mhe. Spika, tungekuwa na ardhi basi tunawapa wale vijana kwa mujibu wa sheria. Tunawaambia hii ni maalum kwa kilimo sio maalum kwa kujenga na halafu tunawasogezea nyenzo zote ambazo tunahisi anazipata kwa wakati. Kwa hivyo, kama ni hivyo lazima kijana atashawishika ili aweze kulima na kuleta tija katika serikali yake.

Mhe. Spika, jambo hili tulione kwa makusudi kwamba vijana wanashindwa kujiendeleza na elimu pia hawapati kuhusu habari ya kilimo. Jambo hili nalo limekuwa na mapungufu makubwa sana kwa sababu kilimo unapomfahamisha mwananchi au kijana basi ataelewa nini maana ya kilimo, lakini unamwambia kilimo tu hivyo itakuwa hafahamu nini maana ya kilimo, anaona kilimo ni njia moja ya kumua.

Mhe. Spika, kwa sababu kilimo unatumia mabavu kwa kulima kwa jembe, lakini siku hizi kuna zana za kisasa ambazo zinatumia umeme. Hilo ni jambo moja ambalo tukikusudia kutaka kuwasaidia vijana wetu basi lazima nyenzo hizo tunaomba tuwakamilishie hapo ndipo tutapata vijana wa kutulia na kuweza kufanya masuala ambayo yenye maslahi mazuri.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa huo huo wa 28 kuhusu habari ya vijana. Mhe. Spika, ni kwamba tukifikia pahali ambapo Waheshimiwa tukizungumzia suala la utalii ni kwamba serikali imetoa tamko zuri kwani imekaribisha watu wawekezaji kwa lengo la kuleta utalii ili kuweza kuondoa umasikini kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, lakini Wazanzibari hawanufaiki na tamko hili, haya nayo ni mapungufu makubwa sana yanatuletea shida kabisa katika majimbo yetu. Mhe.

Spika, wengi waliotawala kwenye mahoteli ya utalii ni Wakenya hapa tumefungua kile chuo cha kusomesha utalii imekuwa ni sawa na tusiwe nacho, kwani hakiwanufaishi Wazanzibari hata kidogo.

Mhe. Spika, basi hata hizi nafasi za bustani basi hawapewi Wazanzibari watapewa wachache tu hupewa wenzetu wa jirani. Mhe. Spika, hili nalo ni tatizo na pia tuangalie sheria zetu zikoje kwa sababu ukimuendea mtu anakwambia mimi nina mapungufu ya sheria. Mhe. Spika, ndio maana nashindwa kutoa rai nyengine katika hizo hoteli kwa sababu P.O sio Mzanzibari na ukitizama P.O lazima awe Mzanzibari ili aweze kuwasaidia Wazanzibari wenzake, lakini nafasi hiyo inakuwa haipati hata siku moja.

Mhe. Spika, hicho ni kitu ambacho kinatukwaza badala ya kuondoa umasikini mimi nasema kuwa tunaendeleza kuwadidimiza watu wawe masikini wa fukara kutokana na hii hali ambayo inajionesha katika mahoteli.

Mhe. Spika, mimi naona mapungufu hayo tuweze kuyarekebisha ili dhana yetu tuliyoitangaza iende vizuri na wananchi wetu waweze kupata ajira kwa kuondoa umasikini katika maisha yao.

Mhe. Spika, nikija kwenye ukurasa wa 33 kuhusu suala la umeme. Mhe. Spika, suala hili sasa hivi kuna mzigo mzito ambao unatukabili sisi tunaotumia umeme. Kwanza tuangalie bei ikoje, ni kwamba bei ya umeme inatuathiri hili suala tuliangalie vizuri na halafu sasa hivi kuna tabia ya kukatika umeme mara kwa mara. Mhe. Spika, hili sijui ni tatizo gani ni bora tuliangalie kwani tunawapa hasara hawa wanaotumia umeme kwani tunawaunguzia vifaa vyao na hasara nyengine tuangalie na bei imezidi.

Mhe. Spika, mimi nafikiri sasa hivi imefika wakati tusitegemee kibiriti kwa jirani kwani tutachelewa kupika, tutachelewa kuwasha moto kwenye majumba yetu. Mhe. Spika, sasa hivi ipo haja kwani wenzetu wa Bara kila leo wanaleta miundombinu ya kileo kwa kutafuta umeme, sisi hapa sijui tunangojea nini. Mhe. Spika, kutokana na hali halisi ilivyo ni kwamba bado serikali hatujaona hili suala la kulipa kipaumbele suala la kuwaita wawekezaji wa umeme.

Mhe. Spika, kwa kuendelea nakuja katika ukurasa wa 34 suala la elimu. Mhe. Spika, sasa hivi kwa kuwa elimu tunaipa kifua mbele na hususan mashamba nikisema kwa mjini itakuwa najidanganya. Mhe. Spika, tukiangalia sasa hivi sehemu za mashamba kuna waajiri wengi wanatoka mjini hivyo muda wa kusomesha unawapotea kwa sababu yule anatakiwa afike muda ambao wa kuweza kipindi kile cha mwanzo basi kipindi hicho anakikosa. Hili nalo tulizingatie katika hali halisi ya kutoa ajira ni kwamba tuwape kipaumbele wale wazalia wa kule katika maeneo yao.

Mhe. Spika, naamini suala hilo tayari limefanyika lakini lina asilimia ndogo. Kuna wengine bado wanajitolea hawajapata ajira mpaka leo sijui tunangoja nini, na kuna wengine tayari wameshamaliza kusoma mpaka leo wako nje. Mhe. Spika, hili nalo tuone hali halisi ya kwamba tunataka kuikuza elimu, lakini kama hatukufanya utaratibu wa kuwaajiri walimu wakawa wengi, basi hili tuliangalie ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu wapate elimu kwa wakati ambao unakubalika.

Mhe. Spika, sasa naingia katika ukurasa wa 37 kuhusu suala la afya. Mhe. Spika, wewe naamini utakuwa shahidi mara nyingi sana mimi huizungumzia afya na naizungumzia afya kwa upenzi kabisa na kwa upendo wa karibu. Mhe. Spika, tukiangalia takriban wananchi wengi tuna matatizo na matatizo yetu yanatokana kupata tiba kutokana na afya zetu. Kabla sijaendelea kukieleza vizuri kifungu hiki nimshukuru Mhe. Rais kuwateuwa Waziri na Naibu wake kwani Waziri ni mwalimu wa sayansi na Naibu Waziri ni daktari mwenyewe. Mhe. Spika, Mhe. Rais ameona ni vizuri kuwaweka watu wawili hawa kutatokea na mabadiliko fulani katika utekelezaji wao wa kazi.

Mhe. Spika, hii hospitali ya rufaa humu kwenye hotuba ya Mhe. Rais ameeleza mambo mengi sana, lakini kuna tatizo ambalo sasa hivi tusilifumbie macho hili tuliseme na nitalielekeza kwa Waziri wa Fedha kama yupo atanisikiliza. Mhe. Spika, sasa hivi tatizo la fedha kwa madaktari ni kwamba mishahara yao ni midogo, lakini humu kwenye hotuba kuna sehemu ambayo inasema kuwa Rais ataendelea kuwatafuta wataalamu wa kisasa je, hawa tuliokuwa nao tuwapeleke wapi? Mhe. Spika, hiyo fedha ya kumlipa mtaalamu tutaipata wapi wakati huyu wa nyumbani aliyefundishwa na serikali yetu kwa pesa nyingi anapewa mshahara mdogo. Mhe. Spika, hili nalo linasikitisha.

Mhe. Spika, siku moja nilikuwa na mgonjwa ana tatizo la mkojo basi nilipofika kule Dar es Salaam nikaambiwa ngojea tukuletee mtaalamu ambaye ndiye mwenye masuala hayo basi Mheshimiwa ata anakuja kumbe ni Mzanzibari. Mhe. Spika, kwa hiyo hili suala tulione ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ni kuhusu makaazi. Mhe. Rais ana malengo mazuri sana kuhusu masuala ya kifungu hiki lengo la serikali ni kuendeleza upatikanaji wa makaazi bora kwa watu wake. Mhe. Spika, makaazi bora hilo eneo lenyewe liko wapi la kuweza kutenga sehemu hiyo. Mhe. Spika, ni kwamba eneo hilo hatuna na kama lipo eneo hilo tunaomba tuambiwe lipo pahali fulani kuweza kujengewa hizo nyumba za kisasa zenye familia bora.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mji Mkongwe ni kwamba kama tunavyoelewa una historia yake, lakini lakunishangaza mimi juzi nimepita pale Mji Mkongwe

nakuta kumezungushwa mabati. Jambo hili hebu serikali tulione kwani nimeambiwa nyumba ile kuwa imeuzwa. Mhe. Spika, ni kwamba hatuoni kuwa tutawakera hao wafadhili wetu wa *UNESCO*, ile ni historia yetu ya Zanzibar kuwa leo inazibiwa mabati kutaka kutengenezwa nasikia imeuzwa. Mhe. Spika, sijui wanasheria wanalifikiria vipi suala hili la kuuzwa jengo hilo kwa bei nafuu kabisa.

Mhe. Spika, ni kwamba ule ni Mji Mkongwe una hadhi yake na haiba yake, lakini leo tunaiondoa ile haiba yake ya kuonesha historia ya Mji Mkongwe ikoje katika jumba lile.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba tuangalie sheria yetu vizuri ni kwamba mapungufu lazima yatakuwa yamo basi tuweze kulisimamisha lile jengo lisiendelee kujengwa kuweza kufanya utaratibu mwengine. Mhe. Spika, pale pakibadilishwa ni kwamba tumepoteza ramani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kukidhi muda wako nina mengi lakini leo naomba nifikie hapa mimi naiomba serikali wananchi wengi wanalipigia kelele suala hili serikali ikae kwa kina kabisa iweze kulitatua tatizo hili. Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono hoja hii.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wa kutuamsha salama na kufika hapa Barazani leo hii.

Pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwanza kwa kuniteua kuwa Mhe. Waziri na pia ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi katika Serikali hii ya awamu ya saba. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kwa sababu ndio mara yangu ya kwanza kwa Baraza hili tukufu kwa awamu hii niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chumbuni kwa kunichagua tena kuwa Mwakilishi wao.

Mhe. Spika, sasa nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais kwa imani ya wananchi wa Zanzibar ya kumchagua kuwa kiongozi mkuu wa nchi hii. Pia nimpongeze kwa juhudi zake za kuiongoza nchi yetu hii kwa amani, mshikamano na upendo. Huu karibu mwezi wa pili tena unaingia watatu sasa Mhe. Rais amekabidhiwa dhamana ya kuongoza Zanzibar. Mhe. Spika, ni kwamba ameanza vizuri na sisi wasaidizi wake tunamshukuru sana na wananchi pia wana mategemeo makubwa ya kubadilisha hali zao za maisha.

Vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza Makamo wetu wawili Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizi katika Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, matarajio

yetu ni kwamba mambo yatakwenda vizuri, mshikamano miongoni mwetu utaongezeka, upendo utaongezeka na tija itapatikana.

Mhe. Spika, sisi wengine tuliokuwemo katika serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Amani Abeid Karume nampongeza sana kwamba chini ya uongozi wake tumejitahidi sana kufanya kazi za serikali, mafanikio makubwa yamepatikana na ndio njia sahihi ya serikali ya awamu ya saba.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa tarehe 11/11/2010 ni hotuba nzuri ambayo yenye dira ya utekelezaji kazi zetu sisi viongozi wa serikali, Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla. Mhe. Rais alizungumza kwa ufasaha, uwazi na kwa msisitizo zaidi ni kwamba dhamira yake na dhamira ya serikali anayoiongoza katika kuleta maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, katika kuwapunguzia ugumu wa maisha, katika kuleta mshikamano na pia kuyaangalia makundi maalum. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi asubuhi alipokuwa akiwasilisha alizitaja dondoo hizo saba ambazo zinabeba hotuba nzima ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, Baraza letu hili ndilo ambalo linafanya kazi za kisheria na kuisaidia serikali katika mwenendo wa uendeshaji wa serikali kwa kupitisha miswada, kupitisha sheria, kupitisha makisio ya serikali na mambo mengine ambayo yanahusiana na hayo. Ili serikali iende vizuri, serikali iweze kupata mafanikio lazima na Baraza la Wawakilishi lifanye kazi nzuri. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa imani ya Waheshimiwa Wawakilishi ya kukuchagua tena kuliongoza Baraza hili tukufu ni matarajio yangu kwamba Mwenyezi Mungu atakujaalia utuongoze vyema, uwe na afya na mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Spika, katika hili Baraza lenyewe kuna Waheshimiwa wa aina mbili humu ndani, kuna wale wa zamani ambao kutokana na juhudi zao wananchi wao wamewaamini na kuwarejesha tena, naomba niwapongeze sana kwa kuendelea kuaminiwa na wananchi wao, bila ya kuamini wasingeweza kurudi Barazani. Pia kuna Waheshimiwa wapya walioingia Barazani nao ni watu makini wana akili na wanaweza kuisaidia nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo, nao nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote wapya kuja kuungana na sisi kwa dhamira ya kujenga nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mafanikio yote ya Baraza hili yanatokana na utendaji kazi wetu wa mashirikiano chini ya uongozi wako na wasaidizi wako ambao watateuliwa hivi karibuni. Mhe. Spika, tunaelewa kwamba pamoja na kuwa tumeingia humu na serikali imeshaundwa na Mhe. Rais ameshaweka kipaumbele cha serikali yako. Mhe. Spika, jambo kubwa ni kwamba tunakuja kutekeleza ilani ya Chama cha

Mapinduzi ambacho pamoja na kwamba ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa lakini sera zake na ilani yake ndizo ambazo zinatekelezwa.

Mhe. Spika, tulimsikiliza Mhe. Rais kwa umakini sana kuhusu majukumu na malengo ya serikali yake. Jambo kubwa ambalo alisisitiza Mhe. Rais ni kujenga uchumi wa kisasa, uchumi ambao utakuwa na tija kwa wananchi wa Zanzibar na kuleta mafanikio. Mhe. Spika, katika mambo ambayo alisema Mhe. Rais siku ile ni mambo manne makubwa aliyataja katika hotuba yake.

Kwanza, alihakikisha kwamba serikali hii ya awamu ya saba itahakikisha imeimarisha kilimo cha kisasa. Tunazungumza kuwa hadi leo kilimo ndio uhai na asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar matumaini yao na ajira zao zinatokana na kilimo. Mhe. Spika, ingawa siku ile Mhe. Rais alisema bado kilimo chetu hakijawa na tija kubwa lakini akaeleza kwamba katika awamu hii ya saba miaka hii mitano ya uongozi wake, atahakikisha kwamba tunakifanya kilimo chetu kinakuwa na tija, kilimo cha kisasa na chenye faida kwa wananchi wote.

Mhe. Spika, kuna matatizo madogo madogo katika kilimo ikiwemo wizi wa mazao, uharibifu wa mazao kutokana na wadudu, pembejeo na mambo mengine lakini bahati nzuri Mhe. Waziri mwenye dhamana ya kilimo ameanza juhudi tumemuona tunampongeza sana. Kwa hivyo, tunaomba aendelee na juhudi za kuwapa matumaini wananchi wetu wakulima kwa kuwaondoshea kero ya wizi wa mazao na pia pembejeo zipatikane kwa wakati. Mhe. Spika, hili ni jambo moja ambalo Mhe. Rais amelizungumzia kuwa litapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, sekta nyengine ambayo Mhe. Rais alisema kwamba hatuna budi kuitumia kikamilifu ili kuongeza pato ni sekta ya uvuvi na kwa uzito wake ikaundwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo, ni matarajio yetu kwamba watu wote wataweka matumaini makubwa kwenye uvuvi, tutatumia uvuvi mpya chini ya wizara mpya na kiongozi mpya wa wizara ili kuleta tija ya kuona nchi yetu ya Zanzibar ambayo imezungukwa na visiwa inapata tija ya kuleta mapinduzi ya kilimo, mifugo na uvuvi katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika hotuba ile ilielezwa kwamba ni matarajio ya serikali hii ya awamu ya saba kujiimarisha kwa uchumi hadi kufikia asilimia 10 kutoka asilimia 6.7 ya mwaka 2009. Kwa hivyo, sekta ya kilimo na uvuvi pamoja na sekta ya viwanda nayo ina nafasi ya kuimarisha uchumi wa Zanzibar, viwanda vya kati ni muhimu sana kwa uchumi wetu hivyo itaongeza pato na pia vitaongeza ajira kwa wananchi wetu. Vile vile sekta ya utalii hii bado inahitaji kupewa kipaumbele na Mhe. Rais alieleza bayana kwamba sekta hii itaangaliwa kwa jicho la ukaribu ili kusonga mbele katika mambo ya uchumi.

Mhe. Spika, sekta hizi zikitumiwa vizuri zitasaidia kutoa faraja kwa Wazanzibari, kwanza kwa kuwapatia ajira pia na kupunguza umasikini wa wananchi wetu. Vile vile zitaimarika na kuaminika tutakapofikia hatua ya kuamini kilimo kwamba kinaweza kutupatia ajira za kudumu, kilimo kinaweza kuwakomboa wananchi wa Zanzibar, uvuvi utawakomboa wananchi wa Zanzibar, pia uvuvi utasaidia kipato cha wananchi wa Zanzibar na viwanda vitasaidia ajira na kusaidia kipato cha Wazanzibari pamoja na utalii.

Mhe. Spika, nimemsikia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akizungumza na kulalamikia utalii kwamba bado hauwafaidishi Wazanzibari lakini mimi natofautiana naye kidogo kwamba kwa hatua tuliyotokea na tulipofikia basi mafanikio katika sekta ya utalii yapo. Mhe. Spika, ingawa kasoro zipo siwezi kukataa lakini kila tukenda mbele na tukijiandaa vizuri tunaweza baada ya muda tatizo ambalo amesema Mhe. Mshimba ikawa ni historia na likawa sio tatizo tena kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, haya mambo ili yafanikiwe lazima mashirikiano yawepo na katika mfumo mpya wa uendeshaji wa serikali hatuna budi kutilia mkazo mshikamano wa *Public Private Partnership.* Hili jambo katika sekta nyengine lazima serikalini liwemo wananchi wajue wajibu wao, serikali ijue wajibu wao na washirika wa maendeleo nao wajue wajibu wao. Kwa sababu hakuna jambo ambalo litawezekana kufanya kazi kwa upande mmoja, ndio maana mpaka leo Zanzibar shida watu wengi kuiamini sekta binafsi, hata watu ambao wanaajiriwa katika sekta binafsi wanaona kama wanashika shika tu, hawajisikii raha kama bado hawajaingia katika mfumo wa ajira ya serikali.

Hii inatokana na kwamba sekta binafsi bado ni nyepesi lakini sekta binafsi itakua na kwa sababu serikali imeshatoa mlango wa mashirikiano basi tuwaombe na hawa sekta binafsi waukamate mkono wa serikali waupokee ili tufanye kazi kwa pamoja, tushirikiane kwa sababu Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, katika kukuza uchumi wetu wa Zanzibar Mhe. Rais alizungumzia kuliimarisha na kuliendeleza eneo la *EPZ*, alizungumzia eneo la Amani, eneo la Micheweni na eneo la Fumba. Mhe. Spika, ukiangalia kwa ujumla haya malengo ya serikali kuanzia kuimarisha kilimo, uvuvi, viwanda na utalii na kuimarisha eneo la *EPZ* itawezekana kwa sababu serikali iliyopita imeshafanya kazi nzuri katika huduma za miundombinu.

Mhe. Spika, mfano hai ni katika eneo la *EPZ* ya Fumba. Eneo lile ni kubwa na ni zuri kwa uwekezaji lakini eneo lile liko katika eneo la mkakati kabisa. Mhe. Spika, ukiangalia pale kuna Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar.

Uwanja huu tayari umeshafanyiwa matengenezo makubwa na matengenezo mengine yanaendelea ikiwemo jengo jipya la abiria na kujenga upya *task* za uwanja wa ndege. Lakini katika eneo la Fumba lina umeme wa kutosha hatuna tatizo la umeme miundombinu ya umeme ipo na barabara ya kwendea Fumba ni nzuri na serikali ina mpango wa kujenga barabara nyengine ya kuanzia pale *ring road* kuelekea katika maeneo huru ya Fumba.

Mhe. Spika, shughuli hizi zinatoa chachu kwa kuliendeleza eneo la Fumba katika shughuli za kimaendeleo. Mimi nataka niwaombe Mawaziri wahusika kwamba wafanye bidii zaidi kuhakikisha kwamba eneo lile linapimwa vizuri kwani wanatafutwa wawekezaji wa kuekeza ama wawe wa ndani au wa nje bila ya kutia choyo kwamba watu wengine mbona fulani kapata eneo hili atafaidika yeye. Mhe. Spika, tunataka tufanye kazi kwa maslahi ya nchi yetu bila ya kuangalia nani atafaidika mmoja mmoja. Mimi nafikiria tuna timu ya serikali ya kuweza kufanya kazi vizuri na kuleta mafanikio mazuri. Mhe. Spika, fursa hizo zinatoa mwelekeo mzuri kwa uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Rais alizungumzia kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya na makaazi. Mhe. Spika, haya mambo ni muhimu kwa kuwajengea uwezo wananchi wetu ili waweze kutoa huduma nzuri kwa serikali. Kwa hivyo, kwa miaka hii mitano tunatarajia kwamba mambo haya yatakwenda vizuri sana na kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo Mhe. Rais alizungumza ni kutoa huduma maalum kwa makundi maalum. Kwanza alizungumzia wanawake, akazungumzia watoto na wazee. Mimi naunga mkono malengo na dhamira ya Mhe. Rais kwamba ili tuendelee lazima serikali yetu itoe kipaumbele kuwaimarisha wanawake, wenyewe wanasema wakiwezeshwa wanaweza. Mhe. Spika, mimi nahisi serikali iwawezeshe na pia tunajenga matumaini mazuri kwani Mhe. Rais alisema kuwa serikali itaangalia baadae kuanzisha Benki ya Wanawake ili kuimarisha huduma zao.

Mhe. Spika, pia kuna huduma za vijana na watoto hawa ndio taifa la leo na wengine la kesho. Kwa hivyo, kuandaliwa vizuri kwa hawa kutasaidia kujenga Zanzibar njema mpya ambayo itakuwa na nuru ya maendeleo. Mhe. Spika, tumshukuru sana Mhe. Rais kwa kuona mbali na kuona kwamba kuna haja ya kuongeza juhudi za kuimarisha watu hawa. Pia kwa wazee nafikiri ni jambo jema la kutoa huduma nzuri, kwani wazee hao wameitumikia nchi hii vizuri, kwa hiyo na wao hakuna budi kuwahudumia na kuwapa tija na kutoa faida kwa maisha yao.

Mhe. Spika, kwa vile muda umeenda sana naomba uniruhusu nizungumzie maeneo mawili ya mwisho ambayo nilihisi kuwa ni muhimu katika hotuba ya

Mhe. Rais. Kwanza Mhe. Rais alisisitiza umuhimu wa demokrasi katika utendaji wa kazi zetu na kwa bahati nzuri demokrasia katika nchi yetu ipo ya kutosha, tumeitumia demokrasia katika kubadilisha mfumo wa uongozi, tumeitumia demokrasia katika mambo yetu ya kisiasa na ya kiuchumi. Mhe. Spika, ili tufanikiwe lazima demokrasia hii ifuate sheria na sisi ili kuweza kufikia pale ambapo tumelenga chini ya Mhe. Rais wetu hatuna budi tumuunge mkono na kumsaidia kuhakikisha kwamba mambo ambayo yametajwa katika hotuba ile yanafanikiwa na yanaweza kutekelezeka.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, niseme tu kwamba mambo yote haya yatawezekana kutekelezwa na kufikia malengo kama tutakuwa tunafanya mambo yetu kwa kufuata sheria, kwa kulinda amani tuliyonayo na kujenga umoja miongoni mwetu. Tusiruhusu kurudi nyuma, tusonge mbele kwa faida ya Zanzibar na tumuombee dua Mhe. Rais wetu aweze kutekeleza majukumu yake na wasaidizi wake na sisi ambao tuko nyuma yao.

Mhe. Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mmoja wa wachangiaji wa hotuba hii muhimu ambayo ina mwelekeo wa uendeshaji wa serikali na kuimarisha maisha ya Wazanzibari kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa awamu ya saba kipindi cha kwanza. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia hazina ya uzima na uwezo wa kutoka majumbani kwetu hadi hapa katika Baraza. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Spika, vile vile nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuitumia fursa hii kukushukuru wewe na mimi angalau kunipatia nafasi kwa mara ya kwanza kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mhe. Rais wetu Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi hii. Namtakia kila la kheri na ni matarajio yetu kwamba atatuongoza na kutuelekeza vyema na hatimaye kupata maendeleo katika nchi yetu. Sambamba na hilo naomba niwapongeze wasaidizi wake wakuu kwa maana ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais. Niwapongeze kwa kupata nafasi hizo na ni matarajio yangu kwamba watamsaidia vyema Rais na hatimaye kupata uongozi mzuri na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nadhani nitumie fursa hii pia kukupongeza kwa kurudishwa katika cheo chako cha Uspika. Ni matarajio yetu kwamba utatuongoza, utatuelekeza

ili kuweza kufanya kazi vyema katika Baraza hili. Kwa hivyo, tunakupongeza sana Mhe. Spika, na wewe kuchaguliwa tena kuwa Spika wetu, tunaimani kwamba utakuwa makini, mahiri na kwa vile ni mweledi wa mambo haya utumishi wako utatusaidia sana katika Baraza letu.

Mhe. Spika, nimalizie pongezi zangu kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Wawi kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. Kwa kweli hapa hawakupoteza na watarajie kupata kile wanachokihitaji kwa maana ya utumishi ulio makini, mahiri, adilifu na wenye kutukuka mno.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Katika ukurasa wa 22 Mhe. Rais ameeleza kuhusiana na mapinduzi ya kilimo. Naomba kunukuu Mhe. Spika, kwa idhini yako amesema kwamba, "Kilimo ndio chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijijini na huchangia asilimia 27.3 ya pato la taifa katika uchumi wetu na kutoa ajira kwa asilimia 44 ya wananchi vijijini".

Mhe. Spika, ni kweli kwamba hadi sasa hivi kama alivyosema Mhe. Rais kilimo bado kinaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa taifa letu na chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi wetu. Lakini Mhe. Spika, wakulima wetu wanapata tatizo kubwa sana kwa sababu inaonekana kwamba hadi leo wananchi bado wanatumia zana za kilimo zilizopitwa na wakati, utaalamu unakosekana na hata soko la mazao yao ni tatizo.

Kwa mfano, hivi tunavyozungumza katika vijiji vyetu kuna tatizo la mabwana shamba. Mabwana shamba ni tatizo kuwa hawapiti vijijini kutoa ushauri wa kilimo kwa wakulima wetu. Hivyo, wakulima wetu wanafanya kazi ya kilimo katika msingi ya kujaribu na kubahatisha jambo ambalo linapelekea tija kuwa kidogo sana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Waziri wa Kilimo na Maliasili alione hili kwamba tatizo la ushauri kwa wataalamu kwa wakulima wetu vijijini ni tatizo kubwa sana. Kwa hivyo, wakulima wanajaribu kulima katika misingi ya kizamani ya kujaribu na kubahatisha, mtu analima pengine kilimo chetu kinapelekea uharibifu wa ardhi. Sasa ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri hilo ataliona na atajipanga vyema ili kupeleka wataalamu vijijini kutoa hizo *technical advice.*

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba mazao yanayolimwa huko kwetu niseme ni *perishable*, yaani ni mazao ambayo ni *annual cross* na si rahisi kuweza kuyahifadhi. Kwa mfano katika kijiji changu cha Vitongoji katika Jimbo la Wawi wakulima wengi wanalima tungule pamoja na mboga mboga nyengine. Pilipili boga anayajua sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub kule kijijini kwangu. Sasa hii inakuwa tabu kuweza kuyahifadhi mazao haya. Kwa hivyo, sokoni hujaa mazao yale katika kipindi cha mavuno na wakulima wanashindwa

kuyahifadhi wanapeleka sokoni na bei inakuwa ni ndogo sana. Sasa wakulima baada ya kunufaika na kilimo hiki wanauza mazao yao kwa bei ndogo kiasi ambacho hayawasaidii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naishauri Wizara ya Kilimo ikae na wataalamu wake kuona kwamba wanaweza kuwasaidia nini wakulima wa kawaida katika kuweza kuhifadhi mazao yao pamoja na ku-*stabilize agricutural price.* Kwa sababu uzalishaji ukiwa mkubwa bei inakuwa ndogo. Sasa mazao yakipungua ndio wanapata bei lakini uzalishaji ukiwa mkubwa basi wanalazimika mazao yao kuuza kwa bei ndogo sana jambo ambalo linawadhalilisha sana wakulima wetu. Kwa hivyo, ili kutoa ajira itakayowasaidia wananchi wetu vijijini basi Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba wanaandaa utaratibu wa kuweza kuwasaidia wananchi kuweza ku-*stabilize* ile bei kwa kasi uzalishaji ukiwa mkubwa.

Mhe. Spika, halikadhalika tukija katika ukurasa wa 30 Mhe. Rais amezungumzia masuala ya miundombinu ikiwemo barabara. Mhe. Spika, napenda niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika hili kwa kuweza kujenga zaidi ya asilimia 70 ya barabara kuu na kuwa na lengo la kutaka kumaliza hiyo asilimia 30. Kwa hili napenda niipongeze serikali.

Vile vile kuwa na mpango wa kuweza kufanya zile *feeder road* ziweze kupitika angalau kwa mwaka mzima. Sasa Mhe. Spika, katika hili ni kwamba kuna maeneo ambayo yananufaika sana na ujenzi wa barabara hizo. Napenda niipe tanbihi serikali kwamba fedha zinazotumika za kujenga barabara ni fedha za walipa kodi wa nchi hii katika maeneo yote ya nchi, sasa unapochukua huduma ya serikali ukaipeleka katika maeneo machache si vizuriu.

Kwa mfano, jana waziri wakati anajibu swali hapa alisema karibu barabara zote za Ziwani zile *feeder road* zinapitika, lakini sasa Mheshimiwa ukiangalia jimbo jirani tu pale la Wawi jimbo langu kuna *feeder road* muhimu sana kwa Pemba nzima kama vile barabara inayotoka katika machimbo ya tofali ya mawe yaliyoko uwandani inayopita Vikunguni hadi Machomanne. Barabara hii ni muhimu sana kwa Pemba nzima kwa sababu wananchi wa Pemba wote wanategemea matofali ya kuchonga yanayotoka katika kijiji cha uwandani, lakini barabara yake Mhe. Spika, ikiwa itanyesha mvua labda uende kwa helkopta lakini kwa trekta tu haliwezi kupita.

Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Spika, kama Mhe. Waziri kamudu kuzifanyia ukarabati *feeder roads* za Ole kama alivyosema jana, basi na Jimbo la Wawi kuna barabara kutoka Uwandani kupitia Vikunguni mpaka Chake-Chake ambapo yeye Mhe. Waziri anatumia matofali hayo hayo kujengea, kwa nini isijengwe? Kwa hivyo, naomba sana barabara hiyo ijengwe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna barabara ambayo inatoka Kianga kuja Vitongoji, hii ni barabara muhimu sana. Katika hotuba ya Mhe. Rais amesema kwamba kuna mpango wa *Cottage Hospital*s ikiwemo hospitali ya Vitongoji kutaka kuzifanya hospitali za wilaya, lakini Mhe. Spika, kama utaiangalia barabara inayoelekea kwenye hospitali hiyo ni kichekesho, kwa sababu siku za mvua Mhe. Rashid Seif kasema yeye wanatumia vitanda kupeleka wagonjwa, sisi hulazimika kutumia gari za ng'ombe kupeleka wagonjwa kwa sababu watu huwa wanaingia kwenye tope hawawezi kuchukua huyo mgonjwa.

Kwa hivyo, ni matarajio yangu kwamba waziri atakiona kilio hiki ile barabara ya Kianga hadi Vitongoji inahitaji angalau kutengenezwa kwa viwango vya lami, kwa sababu wazazi kutoka Jimbo la Ole analotoka Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wanajifungua katika mazingira magumu, ile barabara haipitiki. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri aione barabara hii kusudi wananchi wa Wilaya ya Chake-Chake waweze kunufaika vizuri na ile Hospitali ya Vitongoji, *Cottage.* Kwa bahati nzuri watu wa jimbo hilo wanajifungulia pale pale kwa Mhe. Waziri, ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri ataliona hilo na atalifanyia kazi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 24 Mhe. Rais amezungumzia suala la ufugaji. Katika jimbo langu eneo la Vitongoji ni wafugaji wazuri katika maeneo ya Makaani kule karibu na bahari. Lakini kama alivyoeleza Mhe. Rais wetu kwamba kuna ongezeko kubwa la harakati za uchumi kiasi ambacho wawekezaji wamekwenda kuvamia katika eneo ambalo wakulima wanafanya shughuli zao za ufugaji. Hivi tunavyozungumza kuna mzozo mkubwa katika eneo la jimbo hilo baina ya wakulima na wafugaji kwa upande mmoja na wawekezaji kwa upande wa pili. Hili ni tatizo kwa sababu mamlaka zinazohusika na suala la ardhi inaonekana kwamba haziko makini katika kupima ardhi, zinakwenda kuondosha wananchi ambao miaka mingi wamejiwekeza katika kilimo kuwapa wawekezaji bila ya kujali maisha yao. Sasa hilo ni tatizo limeshaanza kurindima katika Jimbo la Wawi.

Katika hili Mhe. Spika, naomba nimshukuru kwanza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, mara baada ya kusikia tatizo hili lipo pale Vitongoji akamleta Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais amekuja na tumo mbioni kulitatua. Vile vile napenda niipongeze hii kamati inayoongozwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kweli imefanya kazi ya ziada na kwa kiasi kikubwa imeweza ku-*stabilize* hali pale kwani mambo yanakwenda taratibu katika kutatua suala hili. Vile vile napenda niipongeze Kamati ya Mhe. Makame Mshimba nayo kwa kuweza kutatua kwa kiasi fulani tatizo hili la ardhi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, serikali katika hili lazima iwe makini, katika suala la ufugaji itafika siku wafugaji wawe hawana pakukaa ardhi imeshachukuliwa, kila mmoja anakwenda kuichukua anataka kujenga mahoteli, ukienda na ng'ombe wako unaondoshwa, itafika pahala hapa iwe kama vile Bara kuwe na mzozo mkubwa baina ya wafugaji na wakulima pamoja na wawekezaji. Kwa sababu wakulima wanataka ardhi, ardhi itachukuliwa na mahoteli iwe watu hawana pa kufuga. Hili naomba Mhe. Spika, kuwe na mkakati maalum, ikiwezekana naishauri serikali itoe ardhi kwa *priority*, iweke maeneo ya uwekezaji mbali na maeneo ya kilimo mbali, kinyume na hivyo tutakuwa kama Tanzania Bara, vita havitamalizika vya wakulima na wafugaji hapa.

Sasa moja kwa moja Mhe. Spika, niende katika suala la elimu. Suala hili hivi tunavyozungumza ni kwamba serikali yetu inajitahidi sana kuwasomesha walimu na kuwapa mafunzo katika ngazi za cheti *grade 'A'* pamoja na diploma, wamejitahidi sana. Lakini sasa kuna tatizo Mhe. Spika, kwamba walimu waliokwishafundishwa wanakaa nje kwa kiasi kikubwa hawajapata ajira. Hivi ninavyozungumza kuna watu wana *certificate of education* katika jimbo langu huu karibu mwaka wa sita wako nje, wengine wameshatoka kwenda Bara kutafuta ajira kwenye skuli za watu binafsi.

Mhe. Spika, sasa katika hili inaonekana serikali haiko makini kwa hiyo mimi naishauri kama haina uwezo wa kuwaajiri hawa basi wazuie kutoa mafunzo kwanza mpaka pale watakapopata ajira hawa ndio waendeleze mafunzo, ili hizi fedha za walipa kodi zisitumike zikaa kiholela wakanufaika watu wengine. Hili ni jambo moja.

Mhe. Spika, katika hotuba hii namalizia kwa sababu muda ni mdogo Mhe. Rais ameeleza kwamba kuna mpango wa kuifanya Hospitali ya Wete na Hospitali ya Mkoani kuwa ni Hospitali za Mikoa. Mhe. Spika, ni kwamba tuna safari ndefu katika hilo, kwa sababu tuko katika utandawazi Zanzibar ni kisiwa kimaumbile lakini sasa ni sehemu ya ulimwengu katika *globalization*.

Mhe. Spika, ni kwamba Hospitali ya Wete hivi tunavyozungumza wakati kule Wete wanaishi wenyeji na wageni wa ndani na wa nje ya nchi. Mgeni anaweza akafa ugenini, lakusikitisha sasa kama atakufa mgeni Wete labda tumtie kwenye friza kwani hakuna *mortuary*, leo tunataka kuifanya Hospitali ya Mkoa. Mhe. Spika, hiyo ni aibu na fedheha kama inatokea kesi ya kufa mgeni pale Wete basi hawana sehemu ya kumuweka. Mhe. Spika, naiomba serikali kama inataka kufanya mambo haya ianze sasa Hospitali ya Wete hivi tunavyozungumza kama itanyesha mvua basi wale wazazi mle ndani inabidi tuwahamishe katika nyumba za jirani kwani inavuja vibaya mno.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa sababu Mhe. Rais ameshatoa kauli basi tujitahidi kuisimamia kauli hii kuweza kuitayarisha hiyo Hospitali ya Wete kuwa ya Mkoa kinyume cha hivyo basi tunaweza tukasema maneno bila ya kufanya matendo. Mhe. Spika, siku zote matendo hukidhi haja maridhiwa kuliko neno.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba suala zima la utumishi hasa hawa walimu pamoja na madaktari wanafanya kazi ngumu, lakini lakusikitisha mimi juzi napita pale hospitali naona kuna wazee wa miaka mingi wanashindwa kwa mafao na watoto wadogo tu waliokuja juzi, jambo hilo wananung'unika sana kwani hakuna ile *scheme of service* pale. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa katika hili serikali ilione ili na wale wazee wa zamani waweze kunufaika vizuri katika maslahi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia. Mhe. Spika, baada ya kukushukuru na mimi ningeomba nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani kwa fursa walionipa kuweza kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, vile vile nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake nzuri yenye matumaini makubwa kwa Wazanzibari. Mhe. Spika, mimi nilikuwa na michango kama minne tu.

Mhe. Spika, mchango wangu wa kwanza uko katika ukurasa wa 22 katika suala zima la kutilia mkazo kuhusu kilimo. Ni kweli usiopinga Mhe. Spika, kwamba suala la kilimo limekuwa ni suala la uti wa mgongo katika nchi yetu, na kweli tumeona baada ya mabadiliko ya kiuchumi ya nchi yetu kuweza kuweka mahoteli katika maeneo mbali mbali, ni kwamba nchi yetu imekuwa ikitegemea mazao mengi kutoka Tanzania Bara hususan mboga mboga. Mhe. Spika, katika hili ni kweli suala la kilimo kwa nchi yetu linaweza likatusaidia na linaweza likawasaidia wananchi kuinua kipato chao cha kila siku.

Mhe. Spika, pamoja na dhana nzito na dhamira nzuri ya Mhe. Rais katika suala la kilimo na mimi ningependa kusema kwamba kwa hivi sasa kuna mambo ambayo yameanza kujitokeza yanaweza yakarejesha nyuma dhana hii nzuri na bora ambayo Mhe. Rais ameelezea kwa ufasaha kabisa katika ukurasa wake wa 22. Mhe. Spika, maeneo mengi ambayo tulikuwa tunategemea kwa kilimo siku hadi siku yamekuwa yakivamiwa na wananchi kwa kujenga ujenzi holela. Hata jana Mhe. Spika, kama tumeangalia vyombo vya habari tuliwaona wananchi wakilalamika maeneo yao ya kilimo baada ya kuvamiwa na watu kwa kujenga ujenzi ambao hautambulikani.

Mhe. Spika, jambo hili limeanza zamani na niwashukuru baadhi ya mawaziri waliopita walianza kuonesha jitihada ya kutokomeza hili suala la kuvamia mabonde. Mimi nataka nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma alipokuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi alipokuwa akipiga maburdoza majengo yaliyokuwa hayastahiki ndani ya mabonde. Mhe. Spika, jitihada zile na kwa sababu tumepata mawaziri mahiri kabisa, basi ningemuomba Waziri anayehusika akayaangalia kwa kina maeneo ya mabonde ambayo ni maeneo maalum kwa kilimo cha mboga mboga kwa wale waliovamia basi ni kwamba maeneo yale bado yaendelee kuwa wazi na ile dhana ya kilimo ikaweza kupata nguvu zaidi.

Mhe. Spika, mchango wangu wa pili katika hotuba ya Mhe. Rais ni kwamba Mhe. Rais katika ukurasa huu ameelezea vizuri dhana na dhamira yakuboresha maji safi na salama. Mhe. Spika, ni kweli tukiri kwamba suala la maji safi na salama katika Mji wetu wa Zanzibar limekuwa ni tatizo, jitihada serikali imefanya kubwa na hivi karibuni tulikuwa tuna mradi wa Japani na katika hotuba hii Mhe. Rais amesema kwamba tumefikia asilimia 75.

Mhe. Spika, mimi nazungumza kwamba pamoja na dhamira nzuri ya Mhe. Rais na jitihada kubwa ya serikali yetu basi ningeiomba wizara husika ikafuatilia kwa kina hii Taasisi ya Mamlaka ya Maji kwa sababu tunapata matatizo kwamba serikali inajitahidi sana, inatoa fedha nyingi, miradi mikubwa mikubwa lakini bado kuna matatizo ya kiutalaamu na ya kiutendaji katika taasisi zinazohusika. Mhe. Spika, ni kwamba hatuelewi kama uwezo ni duni au ni matatizo ya kibinafsi. Kwa hivyo, katika dhana hii na kwamba tunataka kuboresha suala hili ili kuondosha kadhia ya matatizo ya maji katika Mji wetu huu wa Zanzibar ningemuomba Mheshimiwa husika akalifuatilia kwa kina suala hili ili wananchi wetu ile dhamira ya Mhe. Rais ikapata ufanisi kwa haraka kama vile wananchi wanavyotarajia na alivyojenga imani na serikali yao hii ya awamu ya saba.

Mhe. Spika, mchango wangu wa tatu na wa mwisho ulikuwa katika ukurasa wa 41 katika kuonesha jitihada za kukuza michezo katika nchi yetu. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Rais kwa dhamira nzuri ya kuboresha suala la michezo katika nchi yetu. Ni ukweli usiopingika dhamira hii imeanza kuonekana tangu katika awamu ya sita ya serikali yetu iliyopita, jitihada zimeonekana hususan katika masuala ya mchezo wa miguu. Pia nimpongeze aliyekuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo (Mhe. Ali Juma Shamuhuna) kwa jitihada zake alizoonesha katika awamu iliyopita kuweza kufika Geneva kututafutia wanachama wa *FIFA*.

Mhe. Spika, hiyo ni jitihada nzuri yenye kuonesha mwelekeo kwani sura imeanza kuonekana. Mhe. Spika, katika kulizungumzia suala hili la michezo naiomba taasisi husika kwamba ili michezo ikuwe basi kuna mambo lazima yanahitajika yaimarishwe zaidi. Mhe. Spika, kuna haja yakuutengeneza uwanja mpya uwe mbadala badala ya Uwanja wa Amani kwani maeneo tunayo nina imani viongozi walioko ni mahiri basi watakuwa na upeo wakuona jinsi gani ya kuweza kulitatua tatizo hili. Mhe. Spika, ni kwamba kiwanja tulichokuwa nacho bado hakitoshelezi hususan kule ambako tunataka kuelekea.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niziombe taasisi zinazohusika kutusaidia kuondosha migogoro inayoanza kujitokeza katika zile dhana na dhamira ya kutaka kuelekea katika ulimwengu wa *FIFA*. Hivi karibuni tulikuwa tuna chaguzi, lakini chaguzi hizi zimeonekana zimekubwa na misuko suko ya hapa na pale. Mhe. Spika, misuko suko hii haitotupeleka pale ambapo tunataka kwenda wala haioneshi zile dhamira za viongozi wetu juu ya jitihada zao za kutaka kuboresha masuala haya. Kwa hivyo, nimuombe waziri anayehusika kufuatilia kwa kina ili kutatua migogoro hii na kumaliza katika njia ya haraka ili vyama vyetu vya soka viweze kupata viongozi bora na dhamira ya kule tunakotaka kuelekea tuweze kufika kwa haraka.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi yakuweza kuunga mkono hotuba ya Mhe. Rais. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya uzima na salama, Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize Baraza letu kwa usalama.

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwa ushindi mkubwa, pia nawapongeza wenzangu tuliochaguliwa na tukaweza kurudi tena katika Baraza hili. Vile vile nikupongeze na wewe Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa ukarudi tena kutoongoza katika Baraza lako tukufu. Pia nataka niwapongeze wanawake wenzangu wote wa Mikoa waliotuchagua kwa mara ya pili wakaturejesha tena katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kitabu hiki cha hotuba cha Mhe. Rais mimi nasema kimelenga mambo mengi na hotuba yake ni nzuri na hata kama hatukuichangia basi hotuba hii imepita. Mhe. Spika, hotuba hii imetulenga katika elimu na kutugusa kwenye makundi mbali mbali. Kwanza mimi nataka nimpongeze Mhe. Rais kwa kuwagusa wanawake, watoto na walemavu kwa jumla sote tukawa tumo katika kitabu hiki na kuweza kujua haki zetu za msingi.

Mhe. Spika, Mhe. Rais ameweka mkakati wa kuweza kujuulikana makundi haya ili yatokana na udhaifu na wao walionao, kuanzia masomo, vituo vya afya na kushughulikiwa mambo mbali mbali. Pia kuweza kuondokana na ule ubia wa kutungiwa majina yaliyokuwa hayana maana. Mimi kwa hilo namshukuru sana Mhe. Rais kwa kutuona wananchi wake. Mhe. Spika, pia katika elimu nashukuru sana kwani walemavu tulikuwa nyuma sana, pia tumeshajihishika na serikali imetuona hivyo tunasonga mbele kielimu tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutugusa katika sehemu za uchumi sisi wanawake. Kwa mfano, kama kwenye vikundi vya ujasiri amali na mambo mengine. Mhe. Spika, ni kwamba wanawake tunakaa katika vikundi na tunaona jitihada ya serikali wanavyotupatia mikopo na mambo mengine ni kwamba wanawake tunajishughulisha sana kwa mambo mbali mbali.

Mhe. Spika, sasa nije katika afya ni kwamba watu wenye ulemavu tuna matatizo sana naiomba serikali itusikie pale tutakapofika hospitali hakuna huduma yakuweza kupata mbio mbio wale watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, ukenda hospitali ukiwakuta watu wenye ulemavu mara nyengine utawakuta wamekaa hawana mtu wa kuwahudumikia. Hivyo, tunaomba wakati serikali imetoa mwanya kwa walemavu hivyo wale wahusika wanaohusika tunaomba waweze kutusaidia tukifika sehemu kama hizo tuweze kuonekana.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu akitujaalia tunamuomba Mhe. Rais wetu ampe hekima na busara aweze kutuendesha zaidi na tunamtakia kheri na salama katika uongozi wake. Mhe. Spika, mimi naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais mia kwa mia.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, salama na afya na kuweza kukutana hapa kuendelea na mambo yetu na taratibu zetu ambazo tumejipangia. Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kuchukua fursa hii vile vile kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kunichagua mimi kuwa Mwakilishi wa kuwawakilisha ndani ya Baraza la Wawakilishi katika kipindi hiki cha miaka mitano inayokuja mbele.

Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kusema kwamba hotuba hii imetengenezwa kitaalamu na ni nzuri sana na imetembea katika maeneo yote, hakuna dosari kubwa sana yakuweza kusema kwamba labda mimi nitatia dowa katika jambo fulani. Isipokuwa mimi nitatilia msisitizo zaidi katika maeneo mawili, eneo la kwanza ni eneo la uchumi ambapo uchumi wetu kwa maelekezo ambayo yamepatikana ndani ya kitabu hiki ni uchumi ambao

unaonekana umetawanyika katika maeneo tofauti. Kwa hivyo, ni wajibu wetu kama wasimamizi wakuu wa serikali kusaidiana na viongozi ambao wamewekwa ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inaimarika kiuchumi zaidi.

Mhe. Spika, eneo la pili ambalo nimeliona ni kwamba suala zima la mazingira. Mhe. Spika, sisi tukiwa kama ni viongozi na ni walimu kwa maeneo yetu, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sisi tuwe mbele na tuwe mabalozi wazuri kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanakuwa mazuri, yanakuwa safi na salama. Mhe. Spika, sio siri kwamba Mji wetu hususan wa Zanzibar kwa sasa ni mchafu mno, wageni wanaotembelea tunaokaa nao wanatwambia kwamba Mji wenu ni mchafu. Kwa hivyo, tujitahidini na sisi tuwe walimu tuhakikishe kwamba tunasafisha Mji ili wageni wanaokuja waweze kuneemeka zaidi na wafurahike zaidi na waipende Zanzibar na watusaidie katika suala zima la utalii.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii. Kwanza nikushukuru wewe kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, pia niwapongeze Waheshimiwa wenzangu waliopitia kwa nafasi mbali mbali, nawapongeza kwa kuchaguliwa na wananchi wetu. Mhe. Spika, kwa kweli nikianza kuchangia hotuba hii kipengele baada ya kipengele itakuwa ni vigumu, lakini nitakwenda *in general*. Mhe. Spika, ni kwamba hotuba hii kila sekta ambayo imo humu itatuhusu sisi viongozi na hasa wale viongozi waliofanikiwa kupata uwaziri, hivyo ni majukumu yao kwamba haya yote ambayo ameyatoa Mhe. Rais katika hotuba hii iwe ni dira kwetu ili kuyatekeleza yale yote ambayo ameyaeleza.

Mhe. Spika, vile vile niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani walionichagua naunga mkono hotuba hii lakini kidogo nikenda kwenye suala la maji itabidi niseme kuwa eneo langu la Amani na maeneo mengine jirani basi itakuwa asilimia ndogo sana ambayo mimi naipata kupitia sekta hii ya maji. Kwa kuwa unajua tumeomba ridhaa za wananchi hivyo tusaidiane pamoja na serikali na waziri husika hili suala alifuatilie kwa umakini sana kwa sababu mimi na Waheshimiwa wenzangu kwenye eneo letu lenye majimbo matatu ikiwemo Jimbo la Magomeni, Jimbo la Kwahani na Jimbo la Amani tuna mradi wetu wa SEMUSO lakini kusema kweli tumefuatilia kwa makini sana lakini mpaka sasa hivi hatujapata ufafanuzi.

Kwa hivyo, ninaomba tushirikiane sisi kama viongozi tuliomba ridhaa za wananchi nimuhakikishie Mhe. Waziri kuwa tumejikubalisha kuwa hili tatizo tushirikiane na wao, ingawaje tunajua kuna mapungufu ya uvunaji wa maji,

lakini tumesema kama sisi ni viongozi basi turuhusiwe maeneo ambayo sisi tumeyaona ili tuchimbe visima ili tuondoshe hili tatizo la maji katika majimbo yetu haya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi kutokana na haya yote kwa niaba ya Jimbo langu la Amani niseme naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais na hasa nikitizama kwamba mengi yameshazungumzwa humu na wanawake ndio sisi, na mwanamke ukimuweka anakuwa pamoja na mtoto wake haya mengine yote maendeleo ya mtoto ukimuwezesha mama nahisi yatakwenda vizuri. Mhe. Spika, mimi naunga mkono hotuba ya Mhe. Rais asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, ahsante sana baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais ya tarehe 11/11/2010. Mhe. Spika, kwanza nianze kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, baada ya hayo namshukuru sana Mhe. Rais kwa hotuba yake hii iliyojaa hekima, busara na miongozo mbali mbali.

Mhe. Spika, sasa nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Utaani kwa kunichagua kwa mara ya pili kuwa mwakilishi wao, naishukuru imani yao kwangu na kama walivyonipa imani na mimi natoa imani kwao kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, nikushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili inathibitisha wazi kuwa Waheshimiwa Wajumbe wanaridhika na uongozi wake. Baada ya kusema hayo sasa naomba uniruhusu rasmi kuichangia hotuba ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, hotuba hii kama alivyosema mjumbe aliyetangulia kila unapoiona chakusema tayari kimeshasemwa ndani ya hotuba yenyewe, lakini kwa sababu tunatakiwa tuichangie basi tutaboresha au tutaongeza kwani ishakuwa bora. Mhe. Rais katika hotuba hii alitoa vipao mbele kwa sekta mbali mbali kwa mustakbal wa uchumi wa Zanzibar katika hayo alitaja ustawi wa huduma za kijamii kwamba itakuwa ni *priority* ya kwanza katika kazi ya Serikali ya Awamu ya Saba itayoongozwa na yeye Mhe. Rais.

Mhe. Spika, katika hilo huduma za kijamii nimechukua jambo moja la elimu. Mhe. Spika, katika dunia yoyote ile utaikomboa jamii hii kwa kuipa elimu bora, sasa hivi nchi yetu ya Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la elimu. Lakini elimu hii si kwamba hatuna walimu au majengo ya kufundishia, lakini elimu imekuwa ghali kuwafikia walengwa tukitilia manani watoto wengi wanaopaswa kuanza darasa la kwanza ni watoto wa jamii ya kimasikini. Mhe. Spika, watoto hawa wazazi wao wanashindwa kulipa ile ada ya kuandikishwa

mtoto yule, mzee anadaiwa shilingi elfu saba, mwengine kuna shilingi elfu tano, mwengine shilingi elfu tatu kwanza huwa hakuna kima maalum ni vurugu katika hilo.

Mhe. Spika, uwezo wa mzazi kumudu shilingi elfu saba hawana. Mhe. Spika, ni kwamba watoto wetu unawaona wanahangaika na wazazi wao nenda huku rudi kule Waheshimiwa hawa waliomo ndani. Lakini uwezo wetu wa kutoa huduma hii nao ni mdogo ndio pale tuliposema tunaisaidia serikali kwa kiasi kikubwa. Waheshimiwa waliomba kwamba serikali ituone tena katika mambo fulani.

Mhe. Spika, elimu naomba sana serikali suala la mchango litizamwe upya wazazi hawana uwezo wa kuwalipia watoto wao.

Mhe. Spika, suala la nishati ya umeme wala sio hanasa kwa maendeleo ya binadamu ni suala la lazima umeme ni ghali, kuunga umeme ndani ya nyumba ni ghali lakini hata kuulipia ni ghali na kununua. Uchumi wa jamii ya Zanzibar ni mdogo mno mwananchi huyu tunamwambia ajiwezeshe yaani. nakusudia *private sector* wanajiunga vijana wanaleta kiwanda chao kupasua mbao ama chenginecho, Lakini ile bili ya umeme wanashindwa kama nyumba ya kuishi leo ni zaidi ya laki tano kiwanda je hicho kidogo. Mhe. Spika, maaneo haya yanakwaza mno maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine nashukuru Mhe. Rais katika kukuza uchumi wa Zanzibar pia aliona tuondokane na kule tunakotoka sasa tuende na uchumi wa kisasa kwa kutumia sayansi na teknolojia. Mhe. Spika, nataka niguse maeneo mawili haraka haraka upande wa kilimo wenzangu waliotangulia wameutaja lakini bado nitaendelea kusema kwamba kilimo chetu kwa maeneo yetu mengi ambayo yameshavurugwa kwa upande wa kilimo, yanavurugwa na wenyewe tupo tunashuhudiwa yanaporwa yale muhimu na mazuri kwa ajili ya kilimo tupo tunaona baadae tunakuja kusikitika ama kwa kusema sasa hali ya mazingira ni mbaya, maeneo ya kilimo yamechafuliwa na ndio sisi tunaotoa vibali vya kujenga majumba, ndio tunaoruhusu watu kukata miti ovyo ovyo. Mhe. Spika, sasa nataka kujua mshauri nani katika hili.

Mhe. Spika, kilimo chetu Zanzibar tutalima kupata chakula angalau cha kujikimu lakini kilimo kitakachoweza kumkomboa Mzanzibari hasa wa kijijini ni kilimo kile kitakachokwenda sambamba na utalii wetu, hivi ni mboga mboga badala ya kuagizia Afrika ya Kusini na bara matunda, uvuvi na mifugo yetu. Nadhani tukijikita hapa tutaweza kuwakomboa wananchi wetu kuweza kufaidi kilimo hiki lakini pia waweze kufaidi na mkono huu wa pili ambao ni tegemeo nyeti sasa hivi la uchumi kwa Zanzibar yetu, mboga mboga tutaweza kuzilima mwaka mzima pamoja na matunda yake, hapa serikali ni lazima iamue

kujipanga kwa udhati kabisa kuwawezesha wananchi lakini tu si suala la kwamba dhana hizi ziwepo na pembejeo ziwepo lakini na upatikanaji wa zana zenyewe zote pamoja na pembejeo, ili wamudu kuzinunua hapa ni lazima kuwe na mtazamo maalum kwa mabenki yetu kuweza kutoa mikopo kuwawezesha wananchi kumudu gharama za kilimo hiki.

Mhe. Spika, katika kilimo hicho cha mboga mboga na matunda lakini na mifugo ndipo hapo tutaweza kutizama viwanda Zanzibar tunahitaji viwanda Mhe.Rais kavitaja lakini nadhani viwanda hivi vitakuwa ni vile vya kati na viwanda vidogo vidogo vitakavyowawezesha hasa kina mama kusarifu mazao yao ya kilimo na wale wawekezaji watakapokuwa wamefika nchini hapa kwa mgodi wetu wa bahari tuliyonayo, matumizi ya bahari kuu ametwambia mufti Mhe. Waziri Said Ali Mbarouk kwamba yuko mbioni Mwenyezi Mungu akimjaalia atakaposimama akawa sasa anafanya hasa lile lililokusudiwa nadhani tutaweza kuleta mapinduzi ya uchumi kupitia sekta hizi kwa udhati na kuwezesha watu wetu kufaidika na bahari yao, kufaidika na ardhi yao.

Mhe. Spika, lakini naomba kutumia fursa hii adhimu kuwatanabahisha waheshimiwa wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kwamba tumepata tatizo kubwa sana sasa hivi, tatizo ambalo linahitaji hatua za haraka sana kwa vyombo vinavyohusika na hili. Tuna adui mkubwa anaitwa Chensoo huu ni msumeno unaotumia umeme misitu inaangamia, miti ya uchumi mikarafuu na minazi lakini msheli sheli na wengine wanaofanana na hayo ni tatizo tena tatizo na tusiposimama kujipinda na kupambana nalo miaka mitano ijayo tukimaliza baraza hili tutazungumza vibaya zaidi kuhusu chensoo hii na ukame ndani ya visiwa vya Zanzibar.

Mhe. Spika, watu wanaotumia wamebuni teknolojia sasasa hivi ule mngurumo huusikii kunaunganishwa bomba kama mpira halafu unawekwa kwenye chombo cha maji kama ni ndoo cha chenginecho, husikii kelele hata kidogo. Lakini asubuhi ukiamka eka moja ya mkarafuu haipo, minazi haipo, mishelisheli hakuna, mfenesi haupo hali hii naomba sana serikali isimame kidete na waheshimiwa wajumbe wa baraza lako tusimame kidete kuisaidia serikali kwa kuiokoa Zanzibar yetu, hii krini ambayo inatajwa mpaka ulaya tutakuwa sisi ndio mahasidi wakubwa kutokuilinda lakini tutabeba dhima kama ninavyoendelea kuzungumza siku nyingi kwa jamii yetu kwa kizazi kinachofuata, wazee wetu wamefanya kazi kubwa kuipanda miti, kutupandia mimea mikubwa ya vyakula miti ya misiti tukapata mbao na kujenga leo tunaihasidi, inavurugwa na tunashuhudia na tunanyamaza kimpya na sio ajabu baadhi ya waheshimiwa wako wakamiliki misumeno hii.

Mhe. Spika, nakuomba sana hili ni tatizo uchumi wa nchi hii pamoja na vyenginevyo lakini mkarafuu bado unategemewa, nalisema hili ka kusikitika

sana mama mmoja amenipeleka shambani kwake kwenye shamba la eka tatu mikarafuu nimehisabu kumi na moja imekatwa nilisikitika mpaka nikawa na hali ngumu sana, msumeno kijijini nimekwenda kwa sheha nikamuuliza unawafahamu wenye kumiliki misumeno hii ananambia mimi siwajui, lakini naamini anawajua na sisi wengine Waheshimiwa humu tunawajua. Hili naiomba serikali ichukua hatua muafaka kuihami hali ya nchi hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa mara nyengine unipe fursa hii angalau na mimi kusema lolote juu ya hotuba ya Rais. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na mimi naomba nitume fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache yanayohusiana na hotuba ya Mhe. Rais.

Kwanza nianze na pongezi kwa sababu hii ni hotuba yetu ya kwanza ya ufunguo wetu wa baraza hili la saba ni vyema basi kwanza nitume fursa hii kwa kukupongeza Mhe. Spika, kwa kuchaguliwa kwako naamini kwamba tulikuchagua kwa sababu ya uwezo wako, huruma zako na busara zako katika kukiongoza chambo hiki, umekuwa ni mhimili mkubwa katika chombo hichi muhimu cha serikali. Pili naomba niwashukuru sana wananchi wa jimbo la Chake Chake kwa kunirejesha tena katika chombo hiki katika kuwatumia, naomba niwaahidi kwamba nitaendelea kuwapa utumishi mzuri na siku zote nitaendelea kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika jimbo letu.

Mhe. Spika, katika kuchangia hotuba ya Mhe. Rais naomba nianza kwa kumpongeza Mhe. Rais kutokana na kuchaguliwa kweke kuiongoza nchi yetu kadhalika niwashukuru wasaidizie wake wawili kwanza Maalim Seif Sharif Hamad kama Makamo wa Kwanza na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kama Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika: Waheshimiwa hivi punde tu nimekumbushwa na Katibu wangu mezani hapa kwamba mawasiliano humu ndani mbali ya tatizo la *echo* lakini simu zinatutabisha vibaya mno, sasa tujitahidi turudi kwenye kanuni yetu namba 61(1) ya kanuni ambayo tumeipitisha jana tu kwamba hiyo ni marufuku kuachia simu kuweko wazi, kupunguza isilie sana bado haitoshi kwa sababu ukiweka *vibration* mawasiliano yatakuwa yanaleta matatizo, tunaomba sana waheshimiwa wajumbe tufuate taratibu za kanuni hiyo ili simu zetu tuzifunge na tusizitumie tukiwa ndani ya ukumbi huu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, naamini kwa uwezo waliokuwa nao wasaidizi hawa wa Rais wataendelea kumsaidia Rais katika kulivusha jahazi letu katika kipindi hiki muhimu, kwa kuwa rais ana wasaidizi wengine ambao

ni mawaziri naomba pia niitume fursa hii kwa kuwapongeza sana mawaziri na manaibu waziri kwa kuwa wao ndio watakaokuwa na kazi ya yale yote aliyoyazungumza Mhe. Rais, yale yote aliyoyapanga Rais watekelezaji ni Mawaziri.

Kwa hivyo wao itakuwa ni sehemu kubwa ya kuteleza ahadi zilizotolewa na Mhe. Rais naomba niwapongeze wao mawaziri pamoja na manaibu kwa kuamini kwamba rais hakukosea kuwachagua, sidhani kwamba niongoni mwao kuna mmoja kama ni mjomba wa Rais hapana. Mhe. Rais kawachagua kutokana na kwamba anawaamini kwamba wana uwezo na wanaweza kumsaidia nawapongeza sana na niwaombe wasimuangushe Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu ya wananchi taifa letu linawategemea sana watu hawa.

Mhe. Spika, serikali hii ya awamu yasaba kwa kweli imekuja katika mazingira mazuri ya maridhiano ya kisiasa na tumeunda serikali hii ya umoja wa kitaifa, kwa hivyo kama ilikuwa zamani tunatafuta sababu kwa nini hatuendelei hatuendelei kwa sababu tuna migogoro ya kisiasa, sasa kipengele kile au sababu ile haipo tena sasa tuna mazingira mazuri ya umoja katika nchi yetu, tuna amani nzuri na utulivu wa kutosha wa kisiasa. Kwa hivyo kama ilikuwa sababu hatujaendelea kwa kipindi kirefu kwa sababu hizo nadhani sasa sababu hizo hazipo tena hatuwezi kuzungumzia tena sanabu hizo, nadhani tuyatumie vizuri mazingira hayo mazuri tuliyokuwa nayo ya kisiasa na sasa kuijenga Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi nakiri kwamba hotuba ya Rais inakidhi mwelekeo mzima wa mwelekeo wetu, imejitosheleza kwa kila upande na kwa kila sekta imegusa katika kila eneo, kwa kuwa na sisi ni wawakilishi wananchi tunatakiwa tutie neno basi angalau tuweze kueleza mawili matatu ili kuipa baraka zetu. Mimi binafsi nimeigawa katika sehemu nne kubwa.

1) Hotuba ya rais imegusia namna tutakavyojenga uchumi wetu.
2) Lakini pili ni namna ambayo serikali hii itaweza kuimarisha huduma za kijamii,.
3) Suala zima la kukuza demokrasia na utawala bora na
4) Suala zima la Muungano.

Mhe. Spika, tukichukulia maeneo yote manne yanatoa tafsiri ya utekelezaji wa dira ya maendeleo ya 2020 na maeneo yote yanatoa tafsiri ya utekelezaji katika mpango wa kupunguza umasikini kwa wananchi, vile vile sula zima la *millennium development gold.* Sasa eneo la kwanza la kukuza uchumi Mhe. Spika, tatizo kubwa linalotukabili katika nchi yetu ni suala zima la uchumi na ingelipendeza zaidi wakati tunajadili hotuba hii ya Rais Mawaziri

wangelikuwepo, haya ni mapungufu kama tunajadili hotuba ya Rais na Mawasiri hawapo ni tatizo.

Mhe. Spika, kwa kuwa naamini haya tunayoyazungumza hotuba ya Rais ni mtambuka inagusa kila wizara kwa hivyo ilikuwa inapendeza zaidi Mawaziri wakawepo kama Waziri wa fedha na wengine ili kila mmoja akachukua lile linalomhusu, sasa tunawaomba wenzetu katika serikali katika mambo muhimu kama haya kama hakuna sababu ya msingi basi wasiondoke ondoke, kwasababu sisi itakuwa tunazungumza na nani *(Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo kubwa tulilokuwa nalo ni suala zima la uchumi tunapaswa kama alivyoeleza Mhe. Rais tujenge uchumi kazi yetu ya miaka mitano hii ni kujenga uchumi imara, tutakapojenga uchumi Mhe. Spika, tutaondokana na utegemezi kwa sababu hadi sasa mipango yetu mingi ya kimaendeleo inategemea wafadhili, mwalimu alisema ikiwa tutaendelea kutegemea wafadhili itakuwa uhuru wetu hauna maana yoyote. Mhe. Spika, hilo ni lazima tufanye mapinduzi ya kweli katika sekta zote za uzalishaji, tuwe na mapinduzi ya kweli katika sekta za uzalishaji tutakapokuwa na mapinduzi ya kweli katika sekta zote za kilimo, uvuvi, sekta za viwanda na sekta nyengine nina hakika kwamba uchumi wetu utaongezeka.

Mhe. Spika, zamani tulikuwa tunazungumzia suala zima la kujenga uchumi katika dhana hii ya serikali peke yake, lazima sasa hivi tufike pahala tubadilike ile dhana iliyowafanya wenzetu waendelee kwa kuihusisha Serikali na sekta binafsi sasa ni wakati muafaka wa kuitekeleza kwa vitendo, suala lile lisibakie tu kwamba ni hadithi zinazoendelea. Ili tukuze uchumi wetu ni lazima tuone kwamba na sekta binafsi tunaipa umuhimu wake katika kushirikiana na serikali ili kuimarisha uchumi wetu.

Kwa hivyo mipango mingi itakayokuja sasa hivi ya serikali na baadae ni matumaini yetu kwamba itahusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa mipango hii ya serikali ili tuone kwamba uchumi wetu unakua katika namna ya ukweli. Hoja yangu ni kwamba tunachokitaka matumaini yetu na matumaini ya wananchi tunaomba kwamba uongezeko la uchumi basi uendane na mabadiliko ya hali ya maisha ya wananchi, hii ndio hoja ya msingi kabisa sio tu kuja hapa kila siku na kuambiwa uchumi unakua, lakini tukienda katika maisha halisi ya wananchi hatuoni mabadiliko ya maisha yao. Tutakuwa tuna haki ya kuiuliza serikali uchumi huu unakua wapi haja yetu hatutaki uchumi ukue katika takwimu, nataka tuone uchumi ukikua na uhalisia katika maisha ya wananchi.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba tunataka kukuza uchumi wetu na tunahitaji tuone maendeleo ya kukua kwa uchumi uendane na mabadiliko ya hali halisi ya maisha ya wananchi.

Mhe. Spika, suala jengine alilozungumzia Mhe. Rais ni suala la huduma za kijamii mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964 wazee wetu walipindua kwa sababu hiyo, kipindi kile lengo kubwa lilikuwa ni hilo, hali ya maisha ya wananchi za kijamii zibadilike na ndio maana basi muasisi alitangaza suala la elimu bure, alitangaza maji bure, huduma za afya bure pamoja na masuala mazima ya ardhi hayo ndio yalikuwa maeneo muhimu yaliyogusa mapinduzi ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, hali ilivyo sasa katika sekta hizo hairidhishi na huduma za kijamii ukienda kwenye afya sasa hivi kama walivyozungumza wenzangu tatizo kunakuwa matatizo makubwa, huduma hazirishi. Katika sekta ya elimu nayo kama ilivyozungumzwa hapa kuna matatizo makubwa sasa hivi tunakwenda katika elimu kweli tunakubaliana watu wachachi lakini mchango inakuwa ni kupindukia kwa wanachi wetu. Kila sekta mtoto anapoingia michango kila kitu kinachogusa elimu sasa hivi ni michango ni tatizo kubwa maji safi na salama ni tatizo kubwa, lakini vile vile suala la ardhi kama ilivyozungumziwa asubuhi nalo ni tatizo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, katika serikali ya awamu ya saba tunapaswa kufanya kazi kubwa sana ya kuboresha huduma za kijamii, tuboreshe hutuma za kijamii ili ile dhana na azma ya mapinduzi yetu iandane na uhalisi wa mambo ulivyo.

Mhe. Spika, eneo la tatu ni suala la demokrasia na utawala bora Mhe. Rais kagusia hilo na mimi nampongeza sana, kwa sababu ukuaji wa uchumi una mahusiano makubwa sana na suala zima la demokrasia na utawala bora, kama ikiwa hakuna demokrasia na utawala bora uchumi hauwezi kukua na uchumi unaweza kukua kwa watu wachache. Juzi tulisikia yaliyotokea Tunisia Rais yule aliyeondoka alimuoa mwanamke mmoja katika saluni baada ya miaka miwili mwanamke yule akawa ni bilionea, sasa ujumi unakua lakini unakuwa kwa mtu fulani na ndio maana watu wa Tunisia wakachukua maamuzi.

Kwa hivyo haja yetu tunataka uchumi ukuwe na uenee kwa watu wote waliomo mijini na vijijini, mimi napongeza sana hatua iliyochukuliwa na serikali hii ya kulipa uwezo kwa sababu moja katika taasisi muhimu ya kukuza demokrasia pamoja na utawala bora ni Baraza la Wawakilishi, lazima tuwe na Baraza la Wawakilishi lenye uwezo. Kwa sababu hili ndio linalosimamia serikali sasa Baraza hili likiwa goi goi na serikali yayo itakuwa goi goi, lakini baraza hili likiwa makini nina hakika kabisa na Mawaziri watakuwa makini.

Kwa hivyo napongeza sana uamuzi wa serikali na juhudi za serikali wa kulipa fungu maalum baraza hili ili liweze kutekeleza majukumu yake na likose visingizio, wananchi sasa hivi wanasema Baraza la Wawakilishi ndio

limekwisha serikali ya umoja wa kitaifa haina kitu kwa hivyo hamna upinzani wala hamna chochote. Nataka niwahakikishie wananchi kwamba serikali ya awamu ya saba ni makini na wawakilishi ni makini zaidi. Na tutahakikisha serikali yetu inatekeleza kama ambavyo inaahidi mbele ya baraza. *(Makofi)*

Lakini jengine ni suala la kuipa uhuru zaidi Mahkama, Mahakama zetu ndio vyombo vya haki nayo vile vile serikali ina wajibu mkubwa kupitia wizara inayohusika kuhakikisha kwamba Mahakama nazo zinakuwa msitari wa mbele katika kutoa haki katika nchi yetu.

Lakini jambo jengine ni kuimarisha Afisi za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni jambo la msingi sana, kwa sababu yote yanayofanywa serikali huja mbele yetu na ikataka kuidhinishia fedha kila mwaka, lakini hili kama ikiwa hatukulisimamia vizuri mapato ya serikali juhudi zote zinazochukuliwa na serikali katika kuimarisha uchumi zinaweza kuangukia patupu, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaimarisha Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili nae awe na uwezo wa kuisimamia serikali katika suala zima la matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Spika, karibuni nimesikia kuna utafiti mmoja uliofanywa kule kwa weznetu wa Jamhuri ya Muungano asilimia 33% ya matumizi ya serikali yanaingia katika mifuko ya watu, sasa hii ni hatari na kama hili tutaliruhusu basi juhudi zote zinazochukuliwa na serikali zinaweza zisifike pahala na matokeo yake tukajikuta kwamba wananchi wanaendelea kuteseka na kupata tabu. Naiomba serikali izidi kuipa nguvu Afisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ili mapato ya wananchi fedha za umma ziendelee kutumika kama zinavyoidhinishwa na Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, lakini jengine ni suala zima la kumairisha demokrasia na utawala bora naomba sasa serikali ijenge utamaduni mpya wa kuwajibika, naomba mawaziri wawe makini sana . Kenya kule leo waziri yoyote anayepatwa na shutma bila ya kujibu kwanza inabidi akae pembeni ule ndio utamaduni mpya na ndio utamaduni ambao sasa hivi tunaelekea nao, serikali ijenge utamaduni naanza kufurahi jinsi mawaziri wanavyokuja na kujipanga katika kujibu masuala. Hii serikali tuliyokuwa nayo inatupa matumaini kwamba mawaziri watakwenda katika mwenendo mzuri na hivi ndivyo tunavyotaka.

Mwisho ambalo Mhe. Rais kalizungumzia kwa upande wangu ambalo nahisi ni muhimu ni suala zima la muungano, pamoja na juhudi zote zinazochukuliwa na serikali lakini muungano watu kwa sehemu moja unakuwa ni tatizo katika kuimarisha uchumi wetu. Naomba wazee wetu walipounganisha nchi hii waliunganisha kisiasa, sasa naomba muungano wetu huu tuutumie kiuchumi uwe ni muungano wa uchumi sasa pamoja na siasa yaani pande mbili za

muungano zisaidiane katika suala zima la uchumi mnasaba wa suala hili, tunaomba serikali hii ya awamu ya saba ishughulikie kero zilizomo kwenye muungano.

Kero zilizokuwa za muda mrefu hatuna haja ya kuendelea na kero siku zote huwa nazungumza suala hili serikali, chama ni hicho hicho watu tunatumia lugha moja tunafahamiana, nchi yetu ina amani hakuna sababu ya kuendelea na kero za muungano kwa muda mrefu kila ambacho kinawezekana tukitatue ili tusonge mbele katika nchi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba niseme kwamba ikiwa Zanzibar yenye amani na utulivu imewezekana pia Zanzibar yenye maendeleo makubwa inawezekana. Mwenyezi Mungu naomba aibariki serikali yetu ya awamu ya saba, alibariki baraza hili. Mwenyezi Mungu aibariki Zanzibar na Tanzania kwa jumla Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni mdogo isingependeza kumuita Mhe. Mjumbe kwa kuendelea na mjadala huu na kwa maana hiyo tusitishe shughuli yetu hadi juoni. Lakini tukumbuke tu kwamba watakaotangulia kwanza kujadili hotuba hii jioni Mungu akipenda ni pamoja na Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ismail Mussa Ladhu, Mhe. Moh'd Haji Khalid na wengineo wengi lakini hawa ndio watakuwa wanatangulia mwanzo. Kwa hivyo tujitahidi pamoja na waheshimiwa wengine kufika mapema kama taratibu zilivyo.

Nataka niongeze jambo moja ambalo Mhe. Omar Ali Shehe na mimi nilikuwa na nia ya kulisema kwamba hotuba hii ya Mhe. Rais imegusa mambo mengi ni serikali nzima, ndio ilikuwa inalenga mambo ambayo yanategemea serikali yetu hii ya awamu ya saba itekeleze, kwa hivyo sehemu kubwa ya mambo ambayo yanataka kutekelezwa yamo ndani ya hotuba hii. Bila ya shaka Mhe. Rais kagusa sekta mbali mbali zinazohusiana na wizara mbali mbali kwa sababu hiyo Mhe. Waziri mtoa hoja pengine hatokuwa na wasaa mpana wa kuweza kufafanua baadhi ya hoja ambazo waheshimiwa wajumbe mmezisema na bila ya shaka atahitaji msaada mkubwa sana kwa mawaziri wengine ambao tupo.

Kama mawaziri itakuwa hawapo basi maana yake yale ambayo waheshimiwa wajumbe wanaelekeza kwa serikali baadhi ya mawaziri watakuwa hawakupata taarifa hizo, si vibaya basi kwa wale ambao hawakuwepo kurudi kwenye Hansard kujua nini kimezungumzwa ili hatimae waone maoeneo gani muhimu ambayo yatasaidia kuchangia na kumsaidia Mhe. Waziri mtoa hoja katika hotuba hii.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi Saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa wazima katika jioni hii ya leo na tukaweza kufika hapa katika ukumbi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii ya kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Mhe Rais. Mhe. Spika, labda kwa sababu ni mara ya kwanza kwa awamu hii, labda na mimi nitumie fursa hii kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chonga kwa kuendelea kunichagua kwa mara ya tatu mfululizo. Nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuhakikisha kuwa nawatumikia ipasavyo.

Mhe. Spika, hotuba hii ya Mhe. Rais tukiisoma basi huoni kama kuna sababu ya kutia neno lako jengine. Ni hotuba iliyoandikwa kwa umakini mkubwa na kwa utaalamu wa hali ya juu. Kila unaposoma basi unaona yale mawazo ambayo ungeyachangia, basi yeye kaenda mbele zaidi kuliko yale yako wewe kwa sababu majukumu yetu ni kuwatumikia wananchi, kwa hivyo hatuna budi kutia baraka japo kidogo.

Mhe. Spika, mimi nafikiri lengo letu kuu sote kwa jumla ni kuhakikisha kwamba tunaboresha maisha ya wananchi wetu, tunawaondolea umaskini wa kipato, tunawapatia ajira, ilimradi na wao waweze kuishi maisha mazuri. Hayo ndio malengo yetu sote kwa jumla.

Mhe. Spika, nianze kwenye ukurasa wa 22 ambapo hotuba hii imezungumzia sana mapinduzi ya kilimo. Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mambo yote mazuri yanayohusu kilimo basi Mhe. Rais katika hotuba yake hii ameyazungumza. Kwa mfano amezungumzia namna kilimo kinavyoweza kutoa ajira kwa wananchi, amezungumza namna kilimo kinavyochangia uchumi wa nchi yetu na amezungumza namna kilimo kinavyoweza kuwapunguzia umaskini wananchi, kwa hivyo ni mambo mazuri sana.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi huwa najiuliza sisi Wazanzibari tunakosea wapi kwa sababu mikakati yetu, mipango yetu, sera zetu na kila kitu ni mambo mazuri sana na kila mtu akiyasoma basi anaridhika kwamba haya yataweza kuwafikisha Wazanzibari pahali pazuri. Sasa sijui tunafeli kwenye *practice* au tunafeli wapi. Maana yake nasema tumeganda, mimi nahisi tumeganda kwa

sababu mimi sio mchumi lakini viashiria visivyokuwa vya kitaalamu vinaonyesha bado wananchi wa Zanzibar ni maskini sana. Sina hakika sikufanya vigezo na wenzetu wa nchi nyingine, lakini kwa hapa tulipo ukiangalia mahitaji ya mtu binafsi yanayotakiwa ayapate na hali halisi ya watu ilivyo, tunaweza kusema kama wananchi wa Zanzibar ni maskini.

Mhe. Spika, mimi hujiuliza huwa tunafeli pahali gani kwa kweli. Nadhani labda nitoe nasaha tu kwamba kilimo kweli kinaweza kutufikisha pahala pazuri, ni sekta moja muhimu sana lakini tunahitaji kujipanga na kuyafanyia kazi haya ambayo tunayaazimia kila mwaka.

Kwa mfano tunahitaji kupiga hatua katika kilimo lakini bado tuna ukosefu wa matrekta. Mimi ninavyoamini hatuwezi hata siku moja kufanya mapinduzi ya kilimo kama hatujakuwa na zana za kutosha za kulimia. Kijembe Mhe. Spika, cha kutumia kifua kitatumaliza wala hakitupeleki pahala. Kwa hivyo, mimi nadhani suala la kwanza serikali ihakikisha kwamba kuna matrekta ya kutosha ya kulimia.

Mhe. Spika, hivi karibuni baada ya wananchi wa Jimbo la Chonga kunichagua, nilijitahidi kupita kila eneo na kila tawi langu, mote nilimopita nikawauliza watu kero zao, basi kero ya kwanza waliyokuwa wakinitajia waliniambia bwana tunahitaji kulima lakini hatuna matrekta, hata ukilipata hilo trekta muda ule wa kilimo hasa umepita, kwa hivyo wanakwama hapo.

Mhe. Spika, sasa nahisi matrekta serikali itoe umuhimu wa peke yake lakini sio matrekta tu, tunahitaji pia miundombinu ya umwagiliaji. Maeneo mengi ya Zanzibar sasa hivi zile mvua za kawaida basi zimeanza kupungua na hii labda ni ile aliyoisema Mhe. Assaa asubuhi hapa kuwa inatokana na uchafuzi wa mazingira, miti inakatwa ovyo sana na mvua zimeanza kukimbia sana. Kwa hivyo, tunahitaji serikali ijitahidi katika kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Pia wananchi wanahitaji pembejeo, ardhi unayoilima kila siku hiyo hiyo haiwezi kuwa na tija tena kama hujaitia mbolea.

Mhe. Spika, vile vile wananchi wanahitaji kuwezeshwa, huwezi ku-*invest* katika kilimo sasa hivi kama huna pesa. Sasa nafikiri kuna haja ya kujipanga vizuri zaidi ili wananchi wakapatiwa mikopo hii ya kibenki ambayo inaweza kuwasaidia katika kuekeza kwenye kilimo.

Mhe. Spika, jambo jengine ni taaluma. Mimi hata leo nikiamua kulima siwezi kulima kwa sababu sina taaluma ya kilimo. Kwa hivyo, ni vizuri tukawa na taasisi ambazo zinaweza kutoa taaluma za kilimo. Mhe. Spika, ukiwa mtaalamu wa kilimo unaweza kutumia ekari moja basi ukazalisha mazao ambayo mtu asiyekuwa mtaalamu hata akilima ekari 10 hawezi kuzalisha. Kwa hivyo,

taaluma ni kitu muhimu sana. Ninafikiri tukifanya hivyo basi kilimo katika nchi yetu kinaweza kikatufikisha kwenye hatua kubwa sana.

Mhe. Spika, kilimo ni sekta moja ambayo inaweza kutoa ajira nyingi. Jana Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa anatoa takwimu hapa kwamba watu wengi Wazanzibari wanategemea ajira kutoka serikalini, jambo ambalo uwezekano ni mdogo sana. Lakini sekta kama hizi ikiwa zitafanyiwa mipango mizuri basi watu wanaweza kujiajiri huko, maana bila ajira mtu hawezi kwenda.

Vile vile sekta nyengine ambayo inaweza kutoa ajira kubwa sana ni uvuvi. Mhe. Rais ameeleza kwa urefu namna sekta hii inavyoweza kuwabeba watu wengi. Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar wamezungukwa na maji ya bahari, na kwa sababu ndio mazingira yao wengi sana huwa wanajiajiri kwenye mambo ya uvuvi. Lakini uvuvi wanaofanya wao sio uvuvi endelevu. Wanatumia ile mitego ambayo sasa imepigwa marufuku, hawana vyombo vya kuwafikisha kwenye uvuvi wa kisasa zaidi, uwezo hawana. Sasa mimi nafikiri tunaweza kuekeza hapa katika uvuvi, lakini tunarudi pale pale kwamba ni lazima wananchi wetu wawezeshwe.

Mhe. Spika, tuliona juhudi ya serikali hii iliyopita ya kujaribu kuwakusanya watu katika vikundi na kuwasaidia vifaa vya kuvua kama mashua, mitego na vyengine wanajiendeleza, lakini bado vifaa vile Mhe. Spika, havijaweza kuwafikisha pahali pazuri, maana hawajaweza kuvua katika bahari kuu, wanatembea hapa hapa karibu tu ambapo kwa kweli mavuno yake sasa yamekuwa madogo.

Mavuno ya samaki wengi yako bahari kuu. Mimi nafikiri serikali ingefanya juhudi ya makusudi. Ama kama ni kuwashajihisha *investors* wanunue meli za kisasa ambazo zitaweza kuwafikisha wananchi wetu katika maeneo ya bahari kuu kwenda kuvua au serikali yenyewe inunue hivyo vifaa. Maana inaonekana *investors* wamekuwa wazito sana wa kuekeza katika masuala ya uvuvi. Serikali inaweza kujitahidi kupata angalau kwa awamu, lakini kupata meli zile za uvuvi, tusiiachie bahari yetu, je wakija maharamia wakavua samaki halafu wakiondoka nao.

Mhe. Spika, mimi naamini kwamba kama tutapata vyombo vya kisasa vya kuvulia basi wananchi wetu wanaweza wakapata ajira kubwa sana na nchi yetu ikakuza uchumi kwa kupitia sekta ya bahari. Tunahitaji pia tuwe na viwanda vya kusindika samaki na hili nashukuru Mhe. Rais pia kalieleza katika hotuba yake.

Mhe. Spika, zamani nakumbuka tulikuwa na chuo nafikiri Fidel Castro, kilikuwa kikiwafundisha vijana mambo ya kuvua na ubaharia kwa jumla.

Nafikiri kuna haja pia tukarudia ule utaratibu, kwa sababu Mhe. Spika, jambo la kwanza ni taaluma kabla ya jengine lolote. Ukishampa mtu taaluma, ukishamsaidia ajira sio lazima umuajiri wewe tena. Kwa hivyo, serikali ilitilie umuhimu sana na ilione hasa hili kwamba kuna haja ya kuwa na Chuo cha Uvuvi tena cha kisasa chenye wataalamu na vifaa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye miundombinu na huduma za jamii. Mhe.Spika, katika ukurasa wa 13 wa kitabu hiki cha hotuba hii ya Mhe. Rais ameeleza sana namna nchi yetu ilivyopiga hatua katika miundombinu hasa ya barabara na maji. Lakini Mhe. Spika, mimi nimeona changamoto ndogo tu hapa, kwa kweli sijui kama tunazingatia mambo ya usawa kwa sababu wananchi wa Zanzibar wote wana haki sawa. Sasa unapofikisha huduma ni lazima uangalie wapi tumefikisha kwa asilimia ngapi na wapi wako nyuma kwa asilimia ngapi.

Bahati mbaya sana Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Chonga, nafikiri kama kuna asilimia 75 basi ile 25 iliyobakia haijatekelezeka katika Jimbo la Chonga. Yaani kama wangefanya kule kwenye Jimbo la Chonga basi wangeweza kusema kuwa tumefikia asilimia 100, lakini hii kasoro iko Jimbo la Chonga Mhe. Spika, nasikitika sana tena sana. Nimetumia miaka 10 kuinasihi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwajengee wananchi wa Jimbo la Chonga barabara. Mhe. Spika, toka mapinduzi mpaka leo ni mwaka wa 47 Jimbo la Chonga halina barabara hata moja iliyotiwa lami. Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe waliowahi kutembelea jimbo langu wataniunga mkono.

Mhe. Spika, nije kwa haraka haraka kwenye barabara ya Tundauwa Chanjamjawiri haijajengwa mwaka wa 47 huu, kuna barabara ya Chake-Chake Pujini haijajengwa, gari zote Mhe. Spika, zinavunjika. Mimi katika kipindi cha miaka mitano nimenunua gari mbili na zote hazifai tena, barabara ya Mpitiwa Pujini haipitiki, barabara ya Mgelema Kipapo ni tatizo kubwa, barabara ya Chanjamjawiri Pujini haipitiki, barabara ya Kuyuni Ngomeni hata serikali hawaitambui. Ningefurahi sana kama nikisema maneno haya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano akawa yuko hapa, maana yake mwaka huu nitamfanyia bughudha kubwa.

Mhe. Spika, sambamba na barabara ni mwaka wa 47 kuna maeneo hasa ya magharibi ya Jimbo la Chonga hawajaonjapo maji hata siku moja. Maji wanayotumia Mhe. Spika, huwezi hata kunawiya mikono inasikitisha sana na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na yeye ajitayarishe nitamfanyia bughudha kubwa kweli kweli mwaka huu.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nilitaka nalo niliguse kidogo na hili linaweza likaleta jawabu ile niliyokuwa najiuliza kwa nini Wazanzibari

hatuendelei. Mhe. Spika, Zanzibar sasa kuna mmong'onyoko wa maadili kwa asilimia chini ya 80. Tulikuwa na mila zetu nzuri sana tulizorithi kwa wazee wetu sasa zinapotea Mhe. Spika, sijui kwa sababu gani? ni hatari kubwa.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu anasema, Masheikh wamo nikikosea watanirekebisha hapa.

"Innallaha Layu ghairu Mabikaumin Hata Yughairu Mabianfuisin"

'Yaani Mwenyezi Mungu hazibadilishi neema alizowapa waja wake mpaka yabadilike yale yaliyo ndani ya vifua vyao'.

Mhe. Spika, ndani ya vifua ni muchafu hatupendani, hatumuamini Mwenyezi Mungu hatumuogopi. Sasa tusishangae tena tusishangae kabisa. Kuna hadithi nyengine nataka nimalizie nayo nimeiokota humo humo kwenye Kuran.

Kulikuwa na kikundi cha watu wamefanya ushirika wao wa kilimo, wakalima vizuri na Mwenyezi Mungu akawatilia baraka kweli kweli, wakapata mazao ya kutosha, maskini za Mungu wakawa wanakwenda kuomba na wakigaiwa. Mara nafsi za wale wanaushirika zikabadilika, wakaazimia siku moja wakasema leo bwana maskini yeyote asionje kitu, wakajitahidi kutoka mapema sana na kwa njia za uchochoroni ili wasije wakaonekana wanakwenda kondeni kwao ili wakavune mazao yote na maskini siku ile asipate kitu. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu alishusha tauni yake pale, walipokwenda shamba lao hawakulijua wakajiuliza ilikuaje, halina chochote. Kwa hivyo ni nafsi zilibadilika.

Mhe. Spika, kama hadithi ambayo mara nyingi Mhe. Abubakar Khamis Bakary huwa anaitoa hapa. Mfalme mmoja aliyepita na ujumbe wake katika safari huko akakuta msamaria mmoja ana shamba lake zuri, lina mazao mazuri matamu, kisha wakajipumzisha jua na yule msamaria mwema (mkulima yule) akawapa takrima pale, akawatafutia matunda akawapa wakala na wakafurahi sana. Mfalme akasema hili shamba linafaa kuwa shamba la serikali na akaweka azma ya kulitaifisha.

Basi wakakaa hata siku nyengine wakapita tena pale, kabla ile azma yake hajaitekeleza lakini imo ndani ya nafsi, wakapita kwa yule mzee, walipopita wakakuta shamba limebadilika sana mazao yake yamekuwa mabaya machungu wala hayana ladha. Yule mfalme akamuuliza mbona mzee mambo yamekuwa hivi, tulipopita mara ile yalikuwa matunda matamu, sasa mbona yako hivi kwa sababu gani. Yule mzee maskini hajui kama yule anayemuuliza vile ni mfalme. Yeye akamjibu tu, inawezekana ikawa mfalme wa nchi hii roho yake imebadilika. Sasa mfalme akajiuliza alaa! kumbe ile azma yangu ya kutaka kulitaifisha hili shamba ndio iliyofanya hivi.

Sasa Mhe. Spika, yote haya nakusudia kusema kuwa tunapaswa sisi kama viongozi wa watu, kujitahidi kurudisha mila na silka za Wazanzibari, watu waendelee kupendana, tusifanyiane chuki na tujitahidi kuwaelekeza watu katika kumuogopa Mwenyezi Mungu, yale mambo ambayo yanakwenda kinyume na taratibu za Mwenyezi Mungu tujitahidi kuyazuia, hivyo hivyo japo serikali haina dini lakini tunaweza kufanya baadhi ya mambo. Nafikiri Mhe. Spika, nyoyo za watu zikitengenea basi Mwenyezi Mungu atatunyooshea yote hayo, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Nafikiri Waheshimiwa Wajumbe hivi sasa mnaiona ile sababu ya kupewa cheo cha Maulana Mhe. Mjumbe huyu. Ahsante sana *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kukutana hapa katika mkutano wetu huu. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa machache juu ya hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, nianze kwa kuwashukuru wale walioanzisha maridhiano ya kisiasa. Kwa hivyo, nianze kwa kumshukuru Dk. Aman Abeid Karume kwa ujasiri wake na kuweza kuandaa mazingira mema ya kisiasa, hadi leo ikawa tuko hapa kama ndugu wa baba mmoja na mama mmoja. Mhe. Spika, pongezi au shukrani kama hizo zimfikie mwenzake waliokaa pamoja Maalim Seif Sharif Hamad. *(Makofi).*

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika. Mimi ninavyokuona ni mtu wa hekma, busara, maarifa na uadilifu. Kama maneno yangu ni sahihi basi Mwenyezi Mungu akuongezee busara zako na hekma zako ili uweze kutuongoza vyema *(Makofi).*

Mhe. Spika, sasa nimshukuru Mhe. Rais Dk. Ali Moh'd Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na hatimaye kuja hapa na kuweza kutoa hutuba yake hii ambayo ni kama dira katika Baraza letu hili. Hatimaye nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile kwa kunichagua mimi kuwa Mwakilishi wao kwa kipindi hiki.

Baada ya shukurani hizo nianze kwa upande wa elimu. Elimu tunafundisha watoto wengi lakini sio wote wanaofikia kiwango cha ile elimu ambayo tunawafundisha, kwa sababu gani. Kwenye madarasa ya msingi, darasa la kwanza linachukua zaidi ya wanafunzi 80. Mwalimu anayewahudumia watoto hawa ni mmoja. Hapa mwanafunzi anataka kupikwa na kufundishwa. Ni imani

yangu kuwa mwalimu huyo hana uwezo wa kuweza kuwahudumia wanafunzi 80 wote wakaenda vilivyo.

Mhe. Spika, nilikisoma kitabu kimoja cha ualimu kinachoitwa '*teacher in the making'* lakini cha ukoloni hicho kitabu, kitabu hiki kinaonesha kuwa darasa la kwanza wanafunzi kwa wingi wawe 20 na mwalimu darasani wakati wa kuwafundisha asizidi dakika 15 kwa mfululizo. Sisi tuna wanafunzi zaidi ya 80 wanafundishwa, sijui siku hizi ni dakika ngapi, lakini huko siku za nyuma ilikuwa wanafundishwa kwa dakika 45 tu kwa mfululizo. Sasa wanafunzo wadogo wa aina hiyo na kwa muda wa aina hiyo basi wanamaliza darasa la kwanza wengine wanakuwa hata kalamu au penseli kukamata hawawezi. Sio kwa sababu walimu hawana uwezo, lakini kundi analofundisha ni kubwa, hawawezi kupata taaluma inayotakiwa.

Mhe. Spika, wito wangu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ijaribu kufanya marekebisho juu ya suala hili. Vyenginevyo tutafundisha wengi na hatimaye wanaopata elimu inayostahili ni wachache.

Mhe. Spika, kabla ya kuja hapa nilitembelea katika skuli ziliomo katika jimbo langu, zikiwemo Kengeja, Mtambile na Kangani nikaelezwa tatizo hili. Licha ya hivyo, kwa sababu kuna skuli nyengine elimu ya maandalizi haipo. Kwa hivyo, mtoto wa miaka 6 au 7 basi moja kwa moja anaingia darasa la kwanza, ni tofauti na hapa mjini. Sasa akifika skuli kule anafundishwa masomo 8, anafundishwa somo la Kiswahili, Kingereza, Hesabati, Elimu ya Jamii, Sayansi, Dini, Kiarabu na Michezo. Kwa mwanafunzi anayeanza basi masomo haya ni mengi mno, hasa kwa kuwa huko nyuma hajapata taaluma nyengine yoyote ukilinganisha na wanafunzi wanaotoka maeneo ya mjini. Kwa hivyo, walimu wanashindwa kuwahudumia vyema. *Syllabus* ni mpya na hawana vitabu vya kuwafundishia. Kwa hivyo, tutawafundisha wengi lakini sio wote watakaopata elimu inayokubalika.

Mhe. Spika, kuhusu walimu wenyewe maslahi yao sio mazuri sana. Ningeitaka serikali iwafanyie wafanyakazi *scheme of service*. Nilikwenda baadhi ya sehemu, mwalimu aliyefanya kazi miaka 20, tuseme ni mwalimu wa *form IV* na mwalimu wa *form IV* mwengine aliyeajiriwa miaka 2 au 3, ama huyo wa miaka 20 atakuwa anapitwa au kama anampita basi itakuwa ni kwa *increment* 1 au 2. Pengine ni mjukuu wake kielimu, lakini mapato yao hayapitani sana. Hii wale wakongwe inawatia wivu.

Ualimu Mkuu ni *post*, lakini posho lao ni Shs. 12,000 na wasaidizi wao ni shilingi 6,000/-kwa kule Pemba watakapokwenda mkutano mmoja tu kule Chakechake na kurudi posho hili limemalizika, posho ambalo amepewa atumie

kwa mwezi mzima. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Spika iwaongezee posho Walimu Wakuu.

Vile vile nilipotembelea Skuli ya Kengeja niligundua kwamba haina mwalimu wa *Science*, isipokuwa yupo mwalimu mmoja tu ambaye anakwenda kwa *parttime*. Kutokana na hali hiyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ijitahidi kufundisha walimu wa *science*, kwa sababu hivi sasa walimu wetu wengi ni wa masomo ya *arts*.

Kwa kweli hali hii inaweza kutufikisha pahala tukakosa hata madaktari, kwa sababu wanafunzi wengi wanasoma masomo ya *arts*, kama vile Kiswahili, English, Dini na Kiarabu na wengi wanayakimbia masomo ya *science* na wala sijui kwa nini.

Mhe. Spika, katika hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar alielezea kwamba kipato cha wastani cha Mzanzibari ni shilingi 726,000/-. Hali hii ni sawa na shilingi 6,500/- kwa mwezi na shilingi 2016 na centi 66 kwa siku. Kwa maana hiyo, Mzanzibari pato lake la wastani ni dogo mno, ni wachache wanaoweza kuishi kama wapo kwa shilingi 2016 kwa siku. Kwa hivyo, hali ya wananchi wetu iko hivyo, yaani kipato chake kwa wastani ni shilingi 2016 kwa siku.

Hivyo, ili kuongeza kipato hiki basi ni lazima serikali ichukue juhudi za makusudi za kuwaelimisha wananchi waweze kujiajiri katika sekta binafsi kwa lengo la kuongeza kipato chao. Nadhani jambo hili ndilo linalosababisha vijana wetu waache maadili yetu na wajiingize katika wimbi la wizi na maovu mengine.

Vile vile katika kufanya ziara kwenye jimbo langu nimefika mpaka kijini kimoja kinachoitwa Chole. Kwa kweli hiki ni kijini ambacho kiko baharini na wananchi wake ni wavuvi, wanasema samaki katika bahari ndogo ya kawaida hawapo tena na hivi sasa samaki wengi wamekimbilia bahari kuu ambayo imevamiwa na meli za kigeni.

Mhe. Spika, wanasema wao wanapoingia meli hizi zinatembea bila ya sawi wasi na wakati mwengine ngarawa zao hupigwa vikumbo huko baharini. Kwa hivyo, ninaiomba serikali pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ichukue juhudi za makusudi kwa ajili ya kukabiliana na wimbi hili la meli za kigeni katika bahari yetu kwa lengo la kuwanusuru wavuvi wetu na matokeo haya mabaya.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la umeme. Hivi sasa sehemu nyingi duniani hata jirani zetu Tanzania Bara, watu

wanapoanza kujenga sehemu fulani, basi Shirika la Umeme nao hufika kwa ajili ya kutanguliza huduma zao.

Kwa hivyo, sisi tunaomba na ufuatiliaji wake unakuwa na matatizo. Kwa kuwa tunaomba, basi huduma hii huchukua muda mrefu kutufikia pale tunapoihitaji. Kwa mfano, hata nguzo iwe hapo nje ya uwanja basi umeme kuutia ndani fedha nyingi sana. Kwa maana hiyo, ninaiomba wizara inayohusika kupitia kwako Mhe. Spika, ilitupie macho suala hili kwani watu wanahitaji huduma hii, lakini upatikanaji wake ni mgumu mno.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea kuna Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari wanaombwa mara baada ya kuahirisha kikao hiki cha jioni wakutane na makatibu wao kuna masuala muhimu ambayo yanahitaji kuwekwa sawa.

Waheshimiwa wenyewe ni Mhe. Salim Abdallah Hamad, Moh'd Said Moh'd, Mhe. Assaa Othman Hamad, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Abdi Mosi Kombo watakutana kwenye vyumba vya kamati namba 2. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

Tuendelee kwa kumsikiliza Mhe. Hija Hassan Hija na baadaye Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii kwa lengo la kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar, ambayo ameitoa mwanzoni katika ufunguzi wa Baraza hili.

Kabla sijaanza kutoa mchango wangu, kwanza nianze na kumpongeza Mhe. Rais kwa uamuzi wake wa kuwateua wazee wenye busara Mhe. Seif Sharif Hamad na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi wakiwa ni wasaidizi wake. *(Makofi)*

Vile vile niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuamua tena kukurejesha wewe kuwa Spika, wetu pamoja na kuungana na wazee wenye busara kwa ajili ya kuongoza taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa tathmini ya haraka haraka tukiangalia muhimili wa utendaji kwa maana ya Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na wasaidizi wake, tukiangalia muhimili wa Sheria, yaani Mahakama na Baraza la Wawakilishi kwamba wazee ndio wameshikilia nafasi hizi za uongozi. Kwa hivyo, ni dhahiri

kwamba busara itapatikana na Zanzibar itaendelea mbele katika maendeleo yake. *(Makofi)*

Sasa katika kujua umuhimu wa wazee, Mhe. Rais katika hotuba hii amezungumzia malengo makubwa ya serikali hii ni kuwaenzi wazee wa Unguja na Pemba. Kwa kweli katika hotuba hii Mhe. Rais amesema wazi wazi kwamba serikali itaendelea kuwaenzi wazee kwa kuwapatia huduma muhimu hasa matibabu pamoja na makaazi.

Nadhani uamuzi huu wa serikali ni wa busara sana na unapaswa uendelezwe, kwani kwa sasa wazee wetu wa Zanzibar, yaani Unguja na Pemba wako katika hali mbaya sana na hasa wale ambao wamewekwa katika Nyumba za Wazee za Unguja na Pemba.

Tumekuwa na utaratibu wa kuwahifadhi wazee kwenye makaazi ya serikali, lakini huduma za wazee wale zinakuwa ngumu na mbaya sana. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, katika mambo ya kufanya nafikiri ni vyema kuwahifadhi wazee hawa vizuri na sio kwa jina tu. Kwa mfano, baadhi ya vituo ambavyo tumetembelea kama ni wawakilishi wako basi wazee hao hawapati huduma nzuri hasa za matibabu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wazee hawa nafikiri wanaweza kufariki wengi kutokana na magonjwa mbali mbali yanayowasumbua, kwa sababu madaktari wa nchi hii hawapangiwi utaratibu mzuri kwa ajili ya kuwaangalia wazee wale wanaoishi kwenye nyumba za serikali.

Kutokana na hali hiyo, nitoe nasaha zangu kwa serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wafanye wanavyoweza pamoja na kuwa uwezo wa serikali ni mdogo, lakini kuhusiana na hili la huduma za matibabu na maposho ya wazee mambo haya yapatikane kwa wakati na yawe bora zaidi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo alilizungumza kwenye hotuba yake Mhe. Rais ni kuhusu uwezeshaji wa wananchi, kwamba serikali itafanya kila bidii kwa ajili ya kutafuta mifumo ya fedha kwa lengo la kuwawezesha Wazanzibari kama vile ambavyo tumeanza kwenye Mfuko wa AK na JK.

Kwa kweli Wazanzibari wengi ni wanyonge na wanao mpango wa kujiimarisha kwenye biashara ndogo ndogo. Kwa hivyo, tusingetarajia wakati huu tulionao sasa tukaona wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanapata usumbufu kama vile jana walivyopata matatizo pale Darajani.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo jana hawakufanyiwa jambo zuri. Katika hali ile ambayo wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wanakopa benki

kwa lengo la kujiendeleza kidogo kidogo, matokeo yake askari wanawavamia na kuwatoa kwa nguvu na wala hali hii haipendezi.

Nadhani ni vyema kwa serikali kujipanga na kuwatengea maeneo maalum wafanyabiashara wetu wadogo wadogo ambayo hayatokuwa na matatizo wala kuwaadhibu. Kwa kweli katika hali hii ya unyonge wafanyabiashara wadogo wadogo kusumbuliwa, kupigwa na kunyang'anywa mali zao. Nafiriki hivi sasa si wakati tena wakufanyiwa masuala kama hayo.

Mhe. Spika, nasaha zangu wizara zinazohusika ziwaandalie maeneo maalum ambayo ni mazuri na hayatokuwa na matatizo wala bughudha kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wafanyabiashara wadogo wadogo.

Nadhani eneo waliloandaliwa la Saateni, limevamiwa na watu wenye fedha, sasa mtu mwenye shilingi 500 za biashara hatoweza kukaa kule. Kutokana na hali hii mtu mwenye mtaji wa shilingi 20,000/- hatoweza kupambana na mtu mwenye mtaji wa shilingi milioni 40/-.
Kwa hivyo, ni vyema kuwekwa utaratibu mzuri wa serikali, ili wafanyabiashara wadogo wadogo waweza kufanya biashara zao bila ya matatizo na kujipatia kipato pamoja na kuondosha maovu ambayo serikali kila siku inayapigia kelele.

Vile vile suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu makaazi. Mhe. Rais wa Zanzibar amezungumza wazi kabisa mji wa Zanzibar umekuwa na kiza kikubwa na azma ya serikali hii ni kuweka mataa katika mji huu. Mhe. Spika, katika hili naomba nimpongeze sana Mhe. Rais, kwamba tangu alipokamata madaraka haya hivi sasa Zanzibar Mji wetu unang'ara usiku mzima, hii ni hatua nzuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninaomba kwa sababu limezungumzwa na kuonekana linawezekana na yale mengine ambayo yamezungumzwa nadhani bila ya shaka yanawezekana, basi ni vyema yafanyiwe kazi kama lilivyofanyiwa kazi hili la mataa ya mji wa Zanzibar.

Nikiendelea na mchango wangu napenda nilizungumzie suala la sekta ya afya. Zanzibar tumefikia malengo ya *millenium* kwa majengo pamoja na vituo vya afya, lakini tuko nyuma sana katika maslahi ya madaktari.

Mhe. Spika, katika zama hizi tulizonazo ambapo Pemba kunakusudia kupandisha dajara hospitali mbili Mkoani na Wete. Sasa Pemba nzima haina madaktari wa kutosha wa meno, yaani wapo madaktari watatu na hivi sasa mmoja tayari ameshastaafu na mwengine ndipo anaendelea na kazi.

Kwa hivyo, huku tukiendelea kujenga majengo mazuri kupitia misaada ya wafadhili wa nje, basi ni vyema sasa *to focus* katika kuwatafuta wataalamu wa afya Unguja na Pemba. Kwa kweli sio kama wataalamu hawasomeshwi, lakini wanaondoka kwa sababu ya maslahi.

Mhe. Spika, tumefanya utafiti kwamba wafanaykazi wenye *level* moja ya elimu. Kwa mfano, wataalamu wa Ukunga mwenye elimu ya diploma Zanzibar wanalipwa shilingi 240,000/- na Tanzania Bara wanalipwa shilingi 600,000/- na ushei. Sasa katika hali hii nani mwenye uzalendo wa kuweza kubakia hapa Zanzibar na kufanyakazi, kwa kweli uzalendo unazidiwa na shida.

Kwa hivyo, lazima maslahi ya wafanyakazi yapandishwe, ili wataalamu wetu hapa wasikimbie, vyenginevyo wote watakimbia kwa sababu hakuna mzalendo atakayeishi hapa na njaa, uzalendo lazima uzingatiwe na maslahi.

Kwa maana hiyo, tusiwasomeshe watu kwa fedha za umma na baadaye tukawachezea, yaani tukawaondosha, kweli wataalamu wanakimbia kwa sababu ya maslahi yetu madogo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie kidogo ni kuhusu suala la maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Tumeambia kwamba mradi wa maji hivi sasa umefikia asilimia 75, lakini kwa mwananchi wa kawaida na hata mimi sioni kama kuna asilimia 75 ambayo imefikiwa.

Kwa hiyo, matarajio ya Wazanzibari ni kuyaona yale maji au tuambiwe kwamba ule mradi bado haujafunguliwa. Kwa mfano, leo ukipita mitaani kama vile Jang'ombe, Kwahani, Magomeni wananchi wanatembea na madumu hadi saa 7 za usiku kama vile wanatafuta asali au maziwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani ni vyema Mamlaka ya Maji itueleze mradi tayari umeshafunguliwa au tatizo nini, kwa kweli hatuwezi kupewa takwimu tu ya asilimia 75 na kusema ni kubwa kwa kipimo cha kitaalamu.

Kwa maana hiyo, vizuri tukaambiwa kwamba mradi bado haujafunguliwa au tunasubiri idhini ya Japan ndio tufunguliwe au tatizo nini. Lakini kama mradi umefanikiwa basi tungeona matunda ya maji yanapatikana na kuondosha usumbufu wa watu majumbani ya usiku na mchana.

Kwa kweli leo ni hatari kubwa na Mwenyezi Mungu atunusu kwa sababu ikinyesha mvua basi upo uwezekano wa kuibuka maradhi ya kuharisha, wananchi wanatumia maji ya kuokota kutokana na ukosefu wa maji safi na salama.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu mazingira. Kutokana na hali hiyo, naipongeza sana serikali kwa uamuzi wake wa kusimamia mazingira na hasa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa mfano, hivi juzi nimesikia imepiga marufuku uharibifu wa mazingira hasa maeneo ya Kisiwa Panza, Mwambe pamoja na sehemu nyengine.

Kwa kweli katika sehemu moja ambayo mazingira yameathirika ni eneo la Mwambe. Nadhani asilimia 40 ni wananchi wenyewe na 60 ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio imechangia katika uchimbaji wa kifusi bila ya kuzingatia athari za kimazingira.

Mhe. Spika, juzi nilimchukua Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na kumpeleka Mwambe na kumuonesha, baada ya kumuonesha nilimuomba kwamba mnapomaliza kuchimba basi fukieni. Sasa tunapowaacha hawa wakandasi wanapomaliza na kuondoka, maana yake mashimo yanaendelea kuongezeka Unguja na Pemba.

Sasa ikiwa idara hii inakusudia kusimamia mazingira, basi lazima miradi ya maendeleo inayokuja Zanzibar ni vyema kuzingatia uharibifu wa mazingira, yaani wafukie baada ya kumaliza kuchimba, kwa sababu wananchi hawana uwezo wa kuyafukia mashimo yale. Vyenginevyo suala hili litakuwa ni ndoto na wala halitowezekana kudhibitiwa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nichangie kwa haraka haraka. Takwimu zinaonesha kwamba uchumi wa Zanzibar unapanda na matarajio ya serikali hii waweze kupandisha kutoka asilimia 6.7 hadi 9. Lakini mimi nimekuwa nikijiuliza na bila ya shaka wananchi wa kawaida kama mimi hawaoni ile dhana ya uchumi kupanda.

Kwa mfano, Mhe. Omar Ali Shehe kwamba kuna wasi wasi wataalamu wanachukua vigezo vya wachache kwa takwimu ya Zanzibar ilivyo, watu milioni moja na laki mbili. Sasa ukiwachukua matajiri wa Zanzibar, basi inawezekana kweli ikaonekana uchumi ni mkubwa.

Mhe. Spika, nina wasi wasi kwamba matajiri wa Zanzibar ndio kigezo cha kuona uchumi umekua, lakini hali halisi ya uchumi wa Zanzibar ni mdogo pamoja na umasikini ni mkubwa zaidi.
Kwa hivyo, leo kuna Mhe. Mjumbe mmoja alisema kwamba mtu mmoja wastani wa kipato cha siku ni shilingi 2016/-. Kwa kiwango hiki nadhani tusibweteke na kusema pato la Mzanzibari limepanda, kwa sababu hii ni hatari kubwa sana.

Nadhani ni vyema hivi sasa tuache ule utaratibu wa kuja hapa na bajeti ya serikali na kutajiwa msaada wa Denmark, China na Canada tukawa tunapiga makofi. Kwa hiyo, tunachokihitaji ni kuona kwamba vipi tumepunguza utegemezi kwa bajeti ya serikali, kwa sababu mtindo wa kusubiri wafadhili na baadaye kupiga makofi ni tatizo na tukiendelea na mtindo huu basi maisha hatukwamuki.

Kutokana na hali hiyo, naiomba Wizara ya Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Spika, sasa ituambie tunakusudia kujikwamua kinamna gani katika uzalishaji na sio *income* ya serikali.

Kwa kweli *income* ya serikali kuna njia nyingi kama vile mikopo pamoja na misaada, lakini uzalishaji uko vipi hapa Zanzibar. Nadhani hicho ndicho kipimo cha uchumi na sio *income* ya serikali, kwa sababu serikali inapata mapato kwa njia nyingi na uzalishaji hapa ni mdogo sana.

Kwa mfano, leo mpaka tungule tunaagizia kutoka Bara, sasa mwananchi wa kawaida unapomwambia uchumi umepanda na hatuna hata tungule, mayai na hili ni tatizo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niipongeze serikali kupitia kwako, kwamba hivi sasa imeamua kutumia tafiti za Vyuo Vikuu kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar. Tumekuwa na kilio kikubwa kwamba Zanzibar mipango inapangwa, lakini bila ya kutumia tafiti za wataalamu.

Sasa kama serikali hii imeamua kutumia tafiti za wataalamu, kwa kweli ni jambo la kupongezwa na wala tusiwe na mipango ya kubahatisha. Kwa hivyo, lazima tafiti za wataalamu ndani ya vyuo vyetu zitumike kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliyoitoa hapa 11/11/2010.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu (SW) aliyetujaalia jioni hii kuwa katika hali ya uzima na afya njema ya kuweza kuzungumza mambo ya nchi yetu.

Pili nikupongeze wewe Mhe. Spika kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, ambaye unaliongoza Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Vile vile niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kojani walionichagua kwa mara ya kwanza kuwa Mwakilishi wao. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hotuba nzuri aliyoitoa katika ukumbi huu, iliyojaa hekima na busara na imemaliza mambo yote na kilichobakia ni utekelezaji tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu hotuba ilikuwa nzuri sana, lakini sisi tutasema tuko kazini ni vyema kuchangia mawili matatu, kwa ajili ya kuboresha hotuba ya Mhe. Rais.

Nianze mchango wangu na suala la nishati. Kwa kweli suala hili la nishati ya umeme Mhe. Rais amelizungumza sana kama hivi sasa upo katika kiwango kizuri na kweli ni jambo ambalo halifichiki kwamba umeme upo katika hali nzuri. Maana yake mpaka kisiwa cha Kojani umeme unawaka, tunashukuru sana kwa hili. *(Makofi)*

Kwa kweli serikali imekusudia kuwapatia umeme wananchi wa katika visiwa vyetu vya Makoongwe, kisiwa Panza na Shamiana. Vile vile kwa kuwa Mhe. Rais amezungumza kama ataendeleza mambo yaliyofanyika katika awamu ya sita na miongoni mwao ni suala la umeme.

Sasa tukiangalia umeme umefika mjini mpaka vijijini, lakini katika vijiji sehemu nyingi umepita barabarani tu na wala haujasambaa ndani ya vijiji vyenyewe. Kwa mfano, kijiji cha Mchanga mdogo umeme upo barabarani tu na watumiaji wake ni kidogo sana kiasi watu watatu tu, kwa hiyo suala hili linahitaji kuendelezwa kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Vile vile wananchi wa Kinikanigasi wamejitahidi na nguzo zao tayari zimeshasimamishwa pamoja na malipo, lakini mpaka leo bado hawajapata umeme, ambapo wametumia nguvu zao za michango na wala hawajapatiwa huduma hiyo.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wizara husika ifanye jitihada za kutosha, ili wananchi hao wafaidike na huduma ya nishati ya umeme.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la elimu. Serikali imekusudia kukuza elimu kuanzia Maandalizi mpaka Elimu Mbadala. Kwa mfano, tukiangalia kutoka mwaka 2007/2008 wapo wanafunzi ambao wamehitimu mafunzo ya uwalimu ngazi ya cheti, lakini mpaka leo bado hawajapata ajira na hususan katika Jimbo langu la Kojani.

Mhe. Spika, katika kusoma, kupata elimu pamoja na mafunzo kama hayo, basi mategemeo ni kupata ajira kwa ajili ya kuondoa ile dhana potovu inayosemwa katika vijiji japo ukisoma hupati kazi.

Kwa hivyo, tunaiomba Serikali yetu ya Awamu ya Saba ya Umoja wa Kitafia ilifanyiekazi suala hili la vijana wetu wanaosoma, basi wanapomaliza wapate ajira na hiyo itakuwa ni changamoto kubwa.

Mhe. Spika, katika Wilaya ya Chakechake na Wete bado watu hawa hawajapatiwa ajira, afadhali kidogo watu wa Wilaya ya Mkoani na Micheweni tayari wameshaajiriwa hivi sasa karibu mwaka mmoja, ambao walisoma pamoja na hawa vijana. *(Makofi)*

Sasa nizungumzie suala la maji. Tukiliangalia jambo hili dhana yake ni maji safi na salama. Vile vile huduma hii kama walivyozungumza wenzangu waliotangulia kwamba bado ni duni sana, kwa sababu tunapozungumza imefikia asilimia 75, lakini unapotembea kama alivyozungumza Mhe. Hija Hassan Hija ni tatizo kubwa na watu wanapata usufumbu saa nane za usiku watu wanahangaika na madumu hasa sehemu za Kikwajuni Unguja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika huduma hii ya maji imekusudiwa kuelekezwa mijini na vijijini, lakini hivi tunavyozungumza kuna *Operation* ya Kata Maji ndani ya Jimbo langu la Kojani. Hali hii inatokana na wananchi hawana uwezo wa kulipia maji. Kwa hivyo, tunaiomba serikali ifuate matunda matukufu yaliyopatikana mwaka 1964 ya Mapinduzi ya Zanzibar, yaendelee kuwa bure ili wananchi waweze kukidhi haja zao. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la uvuvi. Wavuvi kama Mhe. Mjumbe mwenzangu alivyozungumza pale kwamba ni ajira binafsi, ambayo inaajiri watu wengi na inaisaidia serikali sana katika mambo ya kujipatia riziki halali, ambapo wananchi wetu wanafanyakazi hii.

Kwa kweli uvuvi ni jambo zito ambalo ni gumu. Kwa mfano, hivi karibuni serikali ilikuwa inagima marufuku uvuvi haramu. Mhe. Spika, kweli katika jimbo langu wavuvi ni wengi sana na mimi nakubali kwamba walikuwa na uvuvi haramu.

Pamoja na hayo, uvuvi haramu ule waliuacha na kufuata njia mbadala ya kutafuta uvuvi wa *ring net* ambao wanao wanauita kwa jina la mtando. Sasa aina hii ya *ring net* pia inasemekana ni uvuvi haramu, Mkurugenzi wa Uvuvi Nyararu alipiga marufuku uvuvi wa mtando. Kwa kweli tulikuwa makini na

kukata rufaa na kwenda mpaka Bungeni kwamba huu si uvuvi haramu, kwa sababu ulipitishwa hapa Bungeni na ipo sheria inayohusiana na uvuvi huu.

Mhe. Spika, wavuvi hawa wa Kojani wanahitaji kuwezeshwa na tunaweza kupata mafanikio mazuri baada ya kuwaelimisha na wala hawana matatizo. Tunaposema Kojani kama ni jina maarufu, lakini linashirikisha wavuvi wengi waliomo ndani ya visiwa vya Zanzibar na Tanzania Bara, ni kwamba watafutiwe vitendea kazi ikiwemo champion ya kuzamia, viatu vya kuogelea na zana nyengine hii unakusudia kumuangamiza, wavuvi wanaotumia zana hizo wanapokuwa baharini kwa kutumia zana ile ili kuona kile wanachokifanya sasa wanaambiwa ni uvuvi haramu, tunaomba utubainishie uvuvi haramu ni upi na uvuvi wa halali ni upi, halafu watu hawa huchomewa nyavu zao ovyo ovyo bila ya kuwapa nyavu mbadala. Jambo ambalo ni kero kubwa sana huwezi kumvunjia mtu sehemu yake wakati anaotaka kujenga na kama hujampa sehemu nyengine.

Lazima ukitaka kumuondoa mtu katika sehemu hii umpe sehemu nyengine ili apate kukidhi haja zake za kupata rizki, kwani hii ndio sehemu ambayo anapata rizki ya kula na watoto wake pamoja na kuwasomesha.

Mhe. Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii kwa mara ya mwanzo kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika serikali hii ya umoja wa kitaifa.

Kwanza kabla ya kuchangia chochote natanguliza shukurani zangu za dhati kabisa kwa wananchi walioko katika jimbo la Mtambwe kwa kunichagua kwa kura nyingi kuliko aliyekuwa mgombea wa jimbo lolote katika baraza hili tukufu, kwa sababu si mara ya mwanzo naamini wananchi hawa wamenichagua wakiwa na imani kuwa nitawatumikia ipasavyo, namuomba Mwenyezi Mungu anisaidie niifanye hiyo kazi.

Pili Mhe. Spika, nimefarijika vya kutosha leo kusimama hapa katika hali tuliyo na serikali tuliyokuwa nayo ya umoja wa kitaifa nikiwa bado ni muwakilishi jambo ambalo nilikuwa nikiliota kwa muda mrefu sana, imani yangu ni kuwa tutashirikiana kuona kuwa yale malengo ya kuchaguliwa tutaisaidia serikali kuipeleka kule wananchi wanakoihitajia.

Mhe. Spika, mwisho natoa shukurani kutokana na uzoefu wako kuona umerudi tena katika baraza hili kama ni spika wetu, mimi nakwita spika kiongozi.

Mhe. Spika, katika kuchangia kitabu hiki cha Mhe. Rais alichokitoa katika ufunguzi wa Baraza hili la nane la wawakilishi, kwanza nashukuru kitabu kimeandikika kiutaalam na kina malengo ya kuipeleka serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ya umoja wa kitaifa pamoja na watu wake kule ambako wananchi wanatarajia. Lakini kuweka melengo ni jambo moja kuyatekeleza ndio kitu muhimu sana kwa sababu hiyo nawaomba waheshimiwa wawakilishi wale ambao wamebahatika kuchaguliwa kuwa Mawaziri kutoka CUF na CCM waiunge mkono hotuba hii, kwa kutafuta kila inavyowezekan rasilimali ya nchi na kutafuta misaada kuona kuwa lengo lililokusudiwa limefikiwa.

Mhe. Spika, katika hotuba hii kumezungumzwa mambo mengi lakini mimi nitazungumza machache tu, kwanza naomba nizungumze huduma ya jamii na hii ni elimu. Mhe. Spika, elimu ni jambo la lazima na kulifanywa mapinduzi mwaka 1964 ili mnyonge nae aweze kusoma na taifa ambalo lina wasomi wengi huwa ni taifa endelevu, ili wananchi waweze kusoma na kuikomboa nchi hii kwa makusudi kabisa elimu iliwekwa bila ya malipo na inaendelea hivyo na mpaka leo bado hakujatokea mabadiliko yoyote ya adhima hiyo, lakini kilichojitokeza na naamini Waziri aliyekuwepo na waliotangulia nyuma yake kwa nia safi kabisa ni suala la kuchangia elimu ili skuli zetu ziweze kujikizi katika mambo madogo madogo.

Sasa kwa bahati mbaya nilipotembelea katika jimbo langu la Mtambwe kutoa shukurani kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi nilikuta matatizo mazito yanayohusiana na elimu, kuna wanafunzi au watoto ambao tayari wameshafika umri wa kwenda skuli, lakini hawakuandikishwa kwa sababu tu wazazi wao hawakuwa na pesa za kutoa ili waweze kuandikishwa baadhi ya skuli ilikuwa ni elfu nne, skuli nyengine elfu sita na kama tunavyoona wazee wetu. Mheshimiwa kazungumza sasa hivi kuwa kipato cha Mzanzibari cha wastani ni shilingi 2016/= kwa siku, hili mimi limeniumiza kwa sababu mwanafunzi hana kosa na mzee huwa hana cha kuchangia sio kosa lake ndio hali ya nchi ilivyo hivi sasa na sote tunakubali kuwa taifa letu ni masikini sana.

Kwa hivyo ninaloomba mimi hii kuchangia mimi sisemi iondoke lakini isiwekwe sheria ifanyiwe kila mbinu lakini watoto wetu wapate kusoma, kukosa kwa wazee cha kulipia isiwe ni sababu ya kukatishwa masomo, wengine kuna wale waliosoma na wazee wamekuwa wakichangia lakini mzee huyo huyo ana watoto zaidi ya watatu mpaka wanne, analipia huku na kule na hali yetu tunaijua. Kwa bahati mbaya wengine wameshindwa na fedha ya kutoa na kulipia kwa sababu ya kuingia darasa jengine pia na hawa wamezuiliwa kusoma, hili mimi limenisikitisha sana.

Sasa katika jimbo langu ambalo lina skuli saba kuna wanafunzi wengi wako nje kwa sababu tu wazazi wao wameshindwa kuwalipia kwa sababu hii au ile,

Mhe. Spika, ninaloomba naiomba serikali sisemi kwamba iondoe kuchangia elimu lakini labda ingelitoa maelekezo kuona kuwa lile lengo la serikali na hasa la elimu na ile hotuba ya Mhe. Rais kuwa watoto katika awamu hii ya saba watapatiwa elimu bora na kila mtoto aliyefika umri wa miaka sita hadi kumi na moja anastahiki kwenda skuli atapelekwa skuli. Kwa hivyo haya mambo ambayo yanakwenda kinyume na hotuba ya Mhe. Rais, yatafutiwe mbinu za kitaalam ili tuone kwa watoto hawa hawakoseshwi haki hii muhimu na ya lazima.

Mhe. Spika, jengine tunaelewa mazingira tuliyokuwa nayo hivi sasa watoto wetu wengi kabisa baada ya kumaliza masomo mpaka wakachukua *degree* ni masomo ya art kama ilivyoelezwa, hii inatokana na ukosefu wa usomeshwaji wa uhakika kwa masomo ya sayansi tokea huko chini wanakotoka, sioni sababu kwa nini huko nyuma tulisoma na tukapasi vizuri tu kwenye sayansi leo isiwezekane. Lakini ninavyohisi ni kwa sababu ya kukosekana vifaa hivi vya kufundishia sayansi, tunajua tuna maskuli mengi katika majimbo yetu yanayofikia madarasa ya kumi na mbili lakini ni machache mno ambayo yana maabara, kwa maana hyo watoto wetu hawapati kusoma masomo ya sayansi.

Mhe. Rais katika kutoa hotuba yake ya ufunguzi wa baraza la nane alisema kapata habari mwenyewe akaita *breaking new*s kuwa viko vifaa vya sayansi vimeshafika katika makontena ambavyo vitaweza kutumika kwa madaraka thalathini na saba, muda umeshapita kidogo tokea kupata taarifa ile ningeliomba kujua kwamba vile vifaa vimeshagaiwa na vimegaiwa vipi na ikiwa bado na sisi tunaomba vigaiwe katika namna ambayo wawakilishi tupo tupeleke vilio vyetu angalau tupate japo kwa skuli zote, kwa skuli nyengine itakuwa ni rahisi kwenda kuchukua mafunzo japokuwa kwa kipindi watakachotaka wenyewe kuliko kubakia hivi hivi ikawa tunakwenda tu.

Mhe. Spika, sasa naomba niingie katika miundo mbinu zimezungumzwa barabara zilivyo na zilizobakia na kwa awamu ya saba wameahidi kutengeneza barabara zote za mashamba na mijini kwa kuweza kupitika kwa kipindi cha mwaka mzima, katika barabara hizi nafikiri nafikiri unakumbuka kuwa siku zote nilikuwa napiga kelele kuhusu barabara ya Mtambwe, kila mtu anasema barabara ilivyokuwa mbaya lakini mimi nataka kwa ushindani hakuna barabara mbovu, mbaya ambayo hata binaadamu hawezi kupita kama barabara ya Mtambwe, nilipiga kelele hizi na siku moja Mhe. Mwakanjuki alipokuwa akipitisha vifungu nilipiga buti na mwisho akaahidi kwamba nikiondoka nitakwenda Mtambwe na nitalala huko huko lazima nileta mabadiliko, lakini Mwenyezi Mungu hakumjaalia kutokana na yaliyomfika Mwenyezi Mungu amsaidie mpaka leo hali ndio ile ile.

Kwa bahati mbaya basi Mawaziri na na Manaibu wao nimewahi kwenda nao na kuwaonyesha ile barabara ilivyo, miaka miwili iliyopita nilifarijika kusikia kuwa tumepata msaada na kuwa barabara ile itajengwa upya na mimi nitafutahi, nashukuru majumba yameshatiwa X lakini ni mwaka mzima hivi sasa hakuna chochote kinachoendelea na sisi tunazidi kuteseka. Ninaloomba Mhe. Spika, kwa sababu tunaoishi katika jimbo la Mtambwe ni binaadam kama binaadamu wengine isipokuwa majimbo mengine tunashinda tu kwa uchumi sisi tuna mazao mengi, sisi tumezungurukwa na bahari alhamdullillah kama huu msaada tulioupata haujawa tayari kuanza basi kwa vyovyote vile kufanywe hali ya dharura nikasaidiwe angalau ile njia itiwe tiwe vifusi badala ya kutengenezwaa ili tuweze kupita hivyo hivyo kwa tabu, lakini ninavyofanyiwa siridhiki na sivyo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa bado dakika tano.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, ikiwa ni dakika tano nazungumzia kwa ufupi kiwanja cha ndege kilichoko Pemba, katika taarifa ya Mhe. Rais amesema kuwa kiwanja kile kitatengenezwa na ndege zitaweza kutua usiku na mchana, mimi kwa ufupi naomba kueleza kuwa kile kiwanja kwa hali ilivyo sasa hivi na tokea kilivyojengwa ni kidogo kwa kutoa huduma, kwa hivyo zaidi ya kutia taa tu na kuziwezesha ndege kutua usiku na mchana mimi ningeliomba utaratibu maalum uwepo kile kiwanja kikuzwe barabara yake ya kurukia na kutulia ndege, lile jengo ambalo tunapumzika ni dogo sana nalo lijengwe na sisi Pemba tuwe na usafiri wa uhakika wa kutumia hizi ndege.

Mhe. Spika, kwa sababu ya dakika tano naomba niende katika usafiri wa meli, tulizungumza asubuhi hapa kwamba wananchi wanaokaa Wete wanapata tabu sana ya usafiri kwa kutumia meli lakini Mheshimiwa Waziri hakunifahamu, kule kila wiki meli inakuja siku moja meli yenyewe inaitwa buraq, utaratibu uliokuweko na ushahidi ninao ni kuwa siku mbili kabla ya meli kuondoka unaambiwa tiketi hakuna na ni kweli huwa zimeshauzwa, lakini siku ya kuondoka hakuna raia mwenye kubakia mwenye tiketi na aliyekuwa hakukata tiketi mbali ya mizigo waliyokuwa nayo. Kwa maana hiyo, nasema watu wanaosafiri kutoka Wete kuja Unguja wanakuja katika hali mbaya wanajazana vibaya kiasi cha uwezo wa meli inayoweza kuchukua na Mwenyezi Mungu atunusuru lakini wakati wowote linaweza kutokea tokeo ambalo sio la kufurahisha.

Mhe. Spika, ushauri wangu na ombi langu kwa Mhe. Waziri ni kufanya utaratibu hizi safari za meli kuja Wete ziongezeke na halafu waangaliwe katika upakizi, kwa sababu ni jukumu lake kuona kwamba meli inachukua ule uwezo wake.

Mwisho Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati naomba kuzungumza hizi na na nakuomba sio vibaya mzee wako ukaniongeza angalau dakika mbili, kitabu cha Mhe. Rais kilieleza maelezo mazuri kuhusu utawala bora na ishaalla na mimi namuomba Mwenyezi Mungu tuingie katika utawala bora kweli, mimi silaumu lakini kumsaidia Mhe. Waziri kufikia huko utawala bora pia ni wajibu wangu. Mheshimiwa utawala bora unaonekana katika mambo kadhaa mimi hapa nazungumzia daftari la kudumu la kupiga kura ni kitu tunachokijua kuwa katika kipindi kilichopita Mhe. Spika, kuna watu Wazanzibari waliotimiza masharti yote na ambao wameshapiga kura miaka chungu nzima huko nyuma safari hii walikosezwa kwa sababu tu hawana kadi ya Uzanzibari ukaazi.

Kuna vijana kuanzia miaka kumi na nane na kuendelea kwa miaka mitano iliyopita walikosezwa kwa sababu hawana vyeti vya Uzanzibari ukaazi, lakini basi kitu kilchokuwepo ni kuwa huwezi kupata cheti kile mpaka utimize umri na wao waliokuwa wakiwainisha kwamba huyu anafaa na huyu hafai kigezo chao cha umri ni kupata cheti cha kuzaliwa cha *register* ambalo hilo ni gumu kwa sababu kuna wazee wengine wamezaliwa wala mambo ya vyeti hawayajui na wameshapiga kura sio mara moja, sio mara mbili wala sio mara tatu.

Kuna wengine wanapeleka vyeti vya kuzaliwa vile vidogo ambavyo unapata *register* pia wamekataliwa hawa ni Wazanzibari wetu, halafu la kusikitisha kabisa daftari la Muungano watu walipoandikishwa wote wale waliingia katika daftari la muungano wazanzibari wakaona *NEC* wametuhurumia kuliko hii tume yetu ya *ZEC*, wakati katiba inazungumza Mzanzibari yoyote akishafika umri wa miaka kumi na nane anayo haki ya kupiga kura na atakosa haki hiyo akikosa kupeleka vielelezo vinavyoonyesha umri wake hasa na mtu akishakuwa na cheti cha kuzaliwa kiwe ni *register* au sio *register* au ukimtizama kwa sura mtu wa miaka 40 au 30 tunawajua.

Kwa hivyo ninaloomba kwa kudumisha demokrasia hebu tuanze hapa kwa yale ambayo tulipitikiwa kwa bahati mbaya au kwa mazingira yoyote tuseme yaliyopita si ndwele tugange yajayo tuanze upya sote tuwe pamoja, hawa wenzetu wote waliokosa haki zao warejeshewe mara moja.
Mhe. Spika, nina mengi lakini naheshimu wakati wako. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nami niunge mkono wenzangu waliotangulia kwa kumuunga mkono Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuchaguliwa kuiongoza serikali hii ya awamu ya saba ya serikali ya kitaifa.
Pili Mhe. Spika, naomba nikupongeze wawe kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Baraza letu hili tukufu, pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitowashukufu

wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunichakua kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuwawakilisha katika Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kuanza mchango wangu katika ukurasa wa 27 kwenye kipengele cha kupambana na umasikini, kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuanzisha Wizara ya Kazi Uwezeshaji wananchi na Ushirika kwa kuona umuhimu wa Idara ya Ushirika katika jamii inayotuzunguruka.

Mhe. Spika, Mhe. Rais katika hotuba yake alieleza kwamba ataendeleza mafunzo na elimu kwa wajasiriamali ili kuhamasisha wananchi katika maisha yao, lakini mimi nilikuwa naomba kabla Mhe. Rais kuwaendeleza hawa wajasiria mali naomba kwanza Mhe. Waziri awaendeleze wafanyakazi au maafisa ushirika wa Wilaya na Mikoa katika sehemu zao.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu kwanza awaendeleze wale kwa sababu Idara ya Ushirika hapo nyuma kabla haijaingizwa katika Wizara hii maalum ilikuwa kama mtoto yatima, ilikuwa haipo katika sehemu maalum ilikuwa ipo ipo tu kwenye Wizara ya kilimo lakini hata kwenye chati haimo kama Wizara ya Kilimo Vyama vya ushirika. Lakini Mhe. Rais aliliona hilo akaona umuhimu wake na kuwaingiza katika Idara ya Kazi na Uwezeshaji.

Mhe. Spika, nimesema wapatiwe mafunzo kwanza maafsa na wawezeshwe kwa kupatiwa vitendea kazi kwanza vyama vya ushirika, kwa sababu bila ya wao hata hao wajasiria mali wakipatiwa elimu itakuwa haina mfuatiliaji wala mwendelezaji wa elimu hiyo. Hasa ukizingatia kwa mfano Wilaya ya kati kuna vyama vya ushirika vinafika mia nne au mia tano lakini afisa ushirika katika wilaya ile ni mmoja tu na hana hata baskeli ya kufuatilia kikundi cha ushirika kilicho Ukongoroni, Michanvi, Charawe, Pongwe au sehemu nyengine. Kwa hivyo hata kama utampatia mafunzo lakini mafunzo yale kama hayakupata ufuatiliaji Mhe. Spika, itakuwa ni bure.

Kwa hivyo Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi awapatie mafunzo kwanza maafisa wa ushirika ili wafanye shughuli zao kiutaalam sio kiuzoefu, pia wapatiwe vitendea kazi ili waweze kufuatila vikundi na wajasiria mali ili waweze kuendeleza yale mafunzo ambayo watapatiwa na Wizara.

Mhe. Spika, pia naomba kuchangia hotuba ya Mhe. Rais katika kipengele cha afya hapa alisema kwamba atawapa madaktari wetu mafunzo ya kuwa mabingwa kwenye fani mbali mbali, wapo madaktari au wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanapatiwa mafunzo wanakwenda kusomeshwa kwa ajili ya kuwahudumia Wazanzibari lakini madaktari hao wanapokwenda kusoma nchi mbali mbali kwa pesa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanashindwa kuwa waadilifu au kuwa wazalendo hubakia huko na kusema hapa hakuna

mshahara wa kulipwa wao. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri apange mpango wa makusudi wa kuwadhibiti wale wafanyakazi ambao wanapelekwa kule waondoke kwa mkataba maalum na warejee hapa waje wafanye kazi wahudumie wananchi wenzao wazalendo, na waweze kujali ile nguvu ya serikali ambayo imewapeleka kule.

Mhe. Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja ya Mhe. Rais na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni hii ya leo kuchangia kwa kifupi kuhusiana na hotuba muhimu ya Mhe. Rais, kama walivyotangulia wenzangu napenda kutoa pongezi kwa viongozi wote kuanzia Mhe. Rais mpaka wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa na kuendelea kufanya kazi katika awamu hii ya saba. Pia napenda niwashukuru sana na niungane nao mkono katika jitihada za kujenga nchi hii wananchi wote wa jimbo la Ziwani ambao walinichagua kwa mara ya pili kungoza katika jimbo hilo kama ni muwakilishi wao.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu moja kwa moja kwenye ukurasa wa ishirini na tatu ya hotuba ya Mhe. Rais katika ukurasa wa 23 na 24 kulielezwa kuhusu mambo ya uimarishaji wa kilimo, kama ambavyo inafahamika kwamba visiwa vyetu tokea tulikotokea kilimo kilikuwa ni uti wa mgongo na Mhe. Rais anataka mapinduzi ya kilimo, mimi naomba nipendekeze mambo matatu muhimu katika suala la kilimo ili tuweze kuleta mapinduzi halisi.

Kwanza suala zima la kuimarisha kitengo cha matrekta, takwimu tulizokuwa nazo zinaonyesha kwamba ardhi inayolimwa kwa mkono ni kubwa zaidi kuliko ardhi inayolimwa kwa trekta kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo ili tulete madabiliko lazima sasa ardhi inayolimwa kwa trekta ianze kuwa kubwa zaidi kuliko ile inayolimwa kwa mkono. Namuomba sana Mhe. Waziri mpya wa Kilimo ambaye kama tunavyomjua kwa ujasiri wake aweze kuleta haya mabadiliko katika kilimo hicho.

Katika kubadilisha zana nzima ya matrekta ni suala la karakana za matrekta zilizokuwepo Mbweni na pale Machomanne. Karakana hizi zipo katika hali mbaya na ndio tegemezi kubwa la utengenezaji na *service* ya hayo matrekta.

Baada ya hilo kuna suala la maradhi ya wadudu wa matunda. Suala hili kutokana na Sera ya Kilimo ya Kuimarisha Usafirishaji wa Mazao ya Matunda ni suala linahitaji kupewa uzito mkubwa ili kuweza kuingia katika uso wa dunia ili na sisi kuweza kusafirisha matunda yetu nje ya Tanzania.

Mhe. Spika, suala la Sera ya Ardhi. Hivi sasa tuna tatizo kubwa la mipaka baina ya ardhi ya kilimo na ardhi ya maendeleo ya ujenzi wa majengo mbali mbali. Tunaomba sana wizara mbili hizi zikae kitako na kufikiria upya sera ya matumizi ya ardhi kwa sababu ardhi yetu ni ndogo. Ikiwa itavamiwa namna hii wale wakulima au wafugaji ambao wanategemea sana ardhi hii watashindwa kutekeleza hayo.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 27 kuna suala la kuondoa umasikini. Mhe. Rais alilitaja hili na pengine ndio chanzo cha kuunda Wizara ya Kuwezesha. Masuala haya ni lazima yaende na utafiti. Nadhani wanaohusika wote kuanzia Wizara ya Fedha na Wizara hii husika wangepata msukumo zaidi ikiwa watakwenda katika haya na kufanya utafiti ni nani hasa ambao wangestahili kupatiwa msukumo katika kuondoa umasikini. Inawezekana juhudi kubwa zinafanywa lakini wale wale ambao mifuko yao ishatuna bado wanaendelea kutunishwa na masikini wanaendelea kuwa masikini zaidi. Kwa hivyo huo utafiti unapaswa kufanyika ili suala hili liweze kupatiwa utatuzi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 29 Mhe. Rais alizungumzia kuhusu suala la ajira. Kwa kweli suala la ajira linategemeana na mambo mengi. Moja wapo ikiwa ni hali ya kiuchumi wa nchi lakini pia ni elimu gani tunayotoa katika nchi. Je elimu hii ni muwafaka na nchi yetu na wakati tulio nao sasa hivi au ni elimu ya nadharia ambayo inawafanya vijana wetu wengi wabaki kungojea ajira zilizokuwa za kuajiriwa serikalini au mwahali mwengine, lakini hawawezi kujisukuma wenyewe au kujiajiri wenyewe.

Katika kushughulikia suala la ajira kwanza kuwe na takwimu. Mara nyingi unanisikia katika Baraza lako tukufu nikihoji kwamba wakati tunapoletewa takwimu hakuna maelezo kikamilifu kuhusu vijana wangapi wamemaliza vyuoni na wangapi wameajiriwa na wangapi bado wanabaki hawajaajiriwa. Suala la kutokuwa na takwimu sahihi kuhusu hali ya ajira pia linapelekea kwamba tatizo hili linakosa kushughulikiwa.

Tungeliomba Wizara husika na karibu kila wizara ingelikuwa na utaratibu wa kuona kwamba wao hasa mahitaji yao ni nini na wakatoa mapendekezo ama kwa Wizara ya Elimu au wizara nyengine husika kwamba vijana wanaowataka ni wa aina hii.

Mhe. Spika, kwa mfano katika moja ya mchango wangu wa nyuma nilisema kwamba suala la elimu ya ufundi limepewa uzito mdogo kwa hapa Zanzibar kuliko elimu nyengine. Hata vyuo vyetu vikuu vingi vinatoa elimu nadharia. Pamoja na kwamba tumefungua Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbweni lakini hakijafanyika chochote kuonesha kwamba kweli tulifungua chuo kikuu cha elimu ya teknolojia Mbweni.

Mhe. Spika, ikiwa tutaendelea hivi hivi kutegemea elimu za nadharia na elimu ya ufundi ikapewa uzito mdogo, nadhani kwa suala la Visiwa bado tutaendelea kutegemea ajira na itakuwa ni suala gumu sana kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, nataka niende katika suala la Miundo mbinu ambalo limezungumzwa na Mhe. Rais katika ukurasa wa 30. Naomba nimnukuu kwa maslahi na manufaa ya Mhe. Waziri wa Miundombinu. Katika ukurasa wa 30 Mhe. Rais anasema hivi:-

> "Kuhusiana na barabara, Serikali yangu itakuwa na majukumu matatu makuu. Jukumu la kwanza ni kuhakikisha kwamba barabara zote kuu zilizobakia yaani asilimia 30 zinakamilishwa katika kipindi kifupi kijacho.
>
> Jukumu la pili ni kuhakikisha kwamba tunazijenga kwa kiwango cha kupitika mwaka mzima"

Mhe. Spika, Mhe. Rais kasema mwaka mzima hakutoa mwezi wa Machi mpaka Juni, barabara zote ndogo ndogo za mijini na vijijini ikiwa na ile yangu ya pembeni kule. Kwa hivyo naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba maneno haya ni ya Mhe. Rais aliyemuajiri sio mimi. Kwamba na barabara yangu ya pembeni imetajwa kwamba barabara zote za mijini na vijiji zipitike kwa mwaka mzima.

Kwa hivyo naomba ninukuu maneno kidogo ya mwisho katika Miundo Mbinu hapa.

> " Kazi hii itafanyika kwa wakati mmoja kwa Unguja na Pemba, sasa sioni sababu ya Mhe. Waziri kusema kwanza tutafanya kubwa halafu tuje tufanye ndogo. Wakati Mhe. Rais kasema zitafanyika kwa wakati mmoja"

Kwa hivyo naomba sana tumuheshimu Mhe. Rais ili barabara hizi zijengwe kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 34 Mhe. Rais alizungumza kuhusu suala la elimu mimi naomba ninukuu maneno yake kidogo hapa katika ukurasa wa 34.

> "Ni nia ya serikali yangu kuongeza ubora wa elimu ya Skuli za Sekondari na kuhakikisha watoto wote waliofikia umri unaostahiki wanapatiwa elimu hiyo."

Mhe. Spika, hapa nataka niseme kidogo, Mhe. Rais hakusema wanafunzi wamalize kidatu cha nne au elimu ya Sekondari, alisema wapatiwe elimu bora. Tunawaomba sana waheshimiwa mawaziri, Waziri wa Elimu akija atueleze viwango vya wanafunzi walivyopasi na sio wangapi wamemaliza.

Mhe. Rais kaagiza kwamba wanafunzi wapatiwe elimu bora. Elimu bora kwa maana ya mwanzo ni matokeo mazuri ya mitihani. Lakini elimu bora vile vile kama alivyosema ni kubadilisha mitaala kiasi tukawafanya wanafunzi wetu wakaweza kujitegemea, hiyo ni moja katika suala la elimu bora. Ikiwa mitaala yetu haitabadilika itakuwa ni mitaala tegemezi yaani mwanafunzi anavyomaliza skuli anabaki bado kungoja ajira, basi bado elimu yetu haitakuwa bora.

Napenda nikumbushe mfano ambao niliutoa sijui mwaka gani katika Baraza lako tukufu. Wakati mmoja Mhe. Spika, tulipata mgeni wakati mimi bado nipo Wizara ya Elimu. Tulikuwa na *workshop* akaja mgeni mmoja kutoka Marekani New York anaitwa Dokta Harbat, yeye alituambia katika mafunzo yake tuchukue kipande cha sponji akasema kitieni ndani ya maji akisha akasema kinyanyue, kinakuwa ni kizito sana kipande kile cha sponji baada ya kutia ndani ya maji. Akasema sasa kikamue, ukikikamua mara moja maji yote yanatoka na kubaki kitupu. Akasema hivi ndiyo mnavyosomesha vijana wenu. Mnamtwika mambo mpaka akimaliza skuli utamuona kachukua mambo mengi halafu akimaliza tu hana cha kufanya anakaa katulia kule.

Wanasema wao walipoona kwamba Japan ni nchi ndogo inawapita wamarekani, walikusanya wataalamu wao wote wa waelimu wakasema achaneni na vitabu vyetu kwanza tutizame sisi tumekosea wapi. Wakafanya *educational review* kwa ajili ya kuitizama Japani kwa nini Wamarekani na nchi yao kubwa ile wapitwe na Wajapani. Sisi tumeshapata mambo matatu makubwa sasa hivi.

1) Tumeshapata utulivu na amani.
2) Tumeshapata Serikali ya Umaja wa Kitaifa.
3) Tumeshapata Muelekeo wa Kubadilishwa Katiba, ambayo sehemu moja ni kikwazo cha maendeleo yetu.

Tubadilikeni kwenye elimu ili tuone kwamba tunamchukua Mzanzibari aweze kuishi katika ulimwengu wa sasa wa sayansi na teknolojia. Na sisemi hivyo kwa maana ya kuwa ni neno maarufu linavyotumika mimi nasema kwa maana halisi hasa ilivyo. Kwa sababu ni elimu bora.

Mwisho napenda nizungumzie kwamba kila mwanadamu moja katika jambo kubwa analotaka ni usalama wa maisha yake. Usalama upo wa aina nyingi.

Usalama mmoja ni mkubwa sana ambao kila mmoja anautarajia, wengine wanakula chipsi, wengine wanakula wali, wangine wanakula muhogo, yaani chakula. Kunapotokea usumbufu wowote katika chakula hali inakuwa sio tulivu. Tunaiyomba sana serikali kumfanya kila mwananchi akawa na utulivu wa amisha yake. Hali ya chakula iwe tulivu katika nchi.

Tuliomba Baraza la Mawaziri kwa kupitia hotuba hii ya Mhe. Rais waweze kukaa kitako na kuona ni njia gani wata *stabilize* hali ya chakula katika nchi. Hizi *fluctuation* zinazotokea mara kwa mara zinapunguzwa kwa kiwango kikubwa ili wananchi waweze kutulia. Kwa sababu tumeshawaelekeza wananchi kwenda katika maendeleo ghafla anaambiwa bei ya mchele imeongezeka mara mbili. Sasa tunampunguzia utulivu wake.

Mwisho kabisa ni suala la utawala bora. Mimi nadhania kwamba bado tunahitaji kufanya tathmini ya muda mfupi wa namna gani tunavyokwenda katika utawala bora. Tumeona kwamba hali hii ya utulivu imewafanya wananchi wetu waweze kujieleza uzuri zaidi katika kutatua matatizo yao. Hii ni sehemu muhimu ya serikali kuitumia sasa hivi, kwa saabu wananchi hata katika redio, katika magazeti, vyombo vya habari, wananchi wanajieleza wazi wazi kwa njia wanazopenda wenyewe.

Huu ni wakati muhimu sana wa kuutumia serikali kuona mambo yale yaliyokuwa yanawakwaza wananchi yanaondolea. Mimi sina haja ya kueleza nini utawala bora lakini mambo mengi yanajulikana. Moja kati ya linalosumbua kwa kiwango kikubwa huko chini ni suala la kupatikana vyeti vya kuzaliwa. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aturekebishie suala hili ili wananchi wetu waanze kupata vyeti vya kuzaliwa kwa wakati. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuweka katika hali hii ya furaha na afya njema kuweza kufika hapa katika Baraza letu hili tukufu. Pili nakupongeza Mhe. Spika, kupata kurudi tena katika Baraza hili kuliongoza, Mwenyezi Mungu akupe uwezo zaidi uweze kuliongoza vizuri.

Kabla ya kuanza kuchangia nilichoamua kukichangia, kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwake na pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa kwao. Imani yangu ni kwamba viongozi hawa watatu mahiri watashirikiana na kushauriana vizuri kuliongoza Baraza hili la Mapinduzi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Rais katika hotuba yake hii kaegemea katika nyanja tofauti hana alichokibakisha, kwa sasa naomba nichangie sehemu ya wanawake.

Mhe. Rais aliangalia sana suala la wanawake, yamenifurahisha sana masuala aliyoyaongelea Mhe. Rais kuhusu wanawake. Kwa niaba ya wanawake wenzangu naipongeza hotuba ya Mhe. Rais kwa kutuingiza wanawake katika hatua hii.

Mhe. Spika, wanawake ni watu wenye matatizo mengi katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Ninachokiomba kwa serikali wanawake ni watu wenye uwezo wa kuwezeshwa. Wanawake ni wajasiri amali wakubwa katika nchi yetu ya Zanzibar. Vikundi vingi vya ushirika vya mboga, mboga vya kujiajiri wenyewe wanawake hawa.

Naiyomba serikali kupitia wizara husika inayoshughulikia mambo ya wanawake, iwaone sana wanawake hao na kulitilia maanani suala la wanawake kuwatafutia soko la kuuza biashara zao baada ya kujiajiri wenyewe kwa vilimo vidogo vidogo vya mboga mboga.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alizungumzia sana suala la afya. Afya ni muhimu kwa mwanadamu. Naiyomba serikali kupitia wizara husika alitilie maanani sana suala la wodi za wazazi na watoto na clinic za wajawazito, ikiwezekana waondoe michango yote ya mama wajawazito wanapokwenda kujifungua pamoja na watoto.

Mhe. Spika, Mhe. Rais pia alipitia katika nyanja ya walemavu. Kuna walemavu katika nchi yetu hii Tanzania kwa jumla na Zanzibar yenyewe. Nashukuru Mhe. Rais alisema kwamba anawajua walemavu na anawathamini na anawajali. Ninachokiomba kwa serikali kupitia Wizara husika inayoshughulikia walemavu, wawaangalie sana dada zetu na mama zetu waliokuwemo ndani ya jamii. Wawape msaada kwa nguvu zote wa hali na mali kwa kuwasaidia kwani mlemavu ni sehemu ya binadamu na ni binaadamu kamili na lililompata yeye ni mwenyezi Mwenyewe kamuandikia na sisi pia Mwenyezi Mungu anaweza akatuweka katika hatua hiyo.

Mhe. Spika, nitagusia kidogo katika suala alililoligusia mwenyewe Mhe. Rais katika hotuba yake nalo ni suala la utawala bora. Suala la utawala bora ni haki ya msingi ya kila raia. Naiomba Wizara husika kupitia Waziri wa Katiba na Sheria atoe mafunzo maalum ya kumfanya kila mmoja ajue haki ya kimsingi kwani wengi wetu hatujui haki zetu za kimsingi ni zipi.

Baada ya hapo kuna mambo ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni tatizo kubwa sana katika Visiwa vyetu hivi viwili vya Unguja na Pemba. Naiomba sana wizara husika ifuatilie kwa makini sana na kwa ukaribu kwa sababu kuna asilimia kubwa ya Wazanzibari wanaoishi mbali na Zanzibar hii hawana vitambulisho vya Uzanzibar ati kwa sababu ya kukosa vyeti vya kuzaliwa.

Mhe. Spika, kuna mtu anamiaka zaidi ya 80 na ukimuona unamjua kwa sura kwa vile hana cheti cha kuzaliwa keshapiga kura na keshajiandikisha zaidi ya mara nne na tano, ananyimwa haki hii kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa. Naomba sana wizara inayohusika na suala hili likae kwa makini na ifatilie, yaliyopita yawe yamepita kwa bahati mbaya au kwa suala lolote lile, lakini sasa tufungue ukurasa mpya wa maisha ili kila mmoja apate haki yake ya msingi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka niseme naiunga mkono hotuba hii Mhe. Rais aliyoitoa tarehe 11, November 2010. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nami nikapata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa tarehe 11, November 2010.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote kuwemo humu tukiwa wazima na afya njema na tukaweza kushiriki katika vikao vyetu hivi kwa niaba ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Pili nitumie nafasi hii au fursa hii kukishukuru chama changu cha Mapinduzi kwa kuniteuwa kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni lakini hatimaye nikapata ushindi wa kishindo katika jimbo hilo. Pia niwashukuru wananchi wote wa jimbo la Magomeni kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. Nawaahidi kwamba sitawaangusha, nitaitumia nafasi hii waliyonipa kwa kuwawakilisha, kuwatetea bila ya woga na bila ya jambo lolote lile ambalo litanipa hofu. Nitajitahidi kuyaeleza matatizo yao na kuiambia serikali nini wananchi wa Jimbo la Magomeni wanahitaji kutoka serikalini.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini pia na kwa hotuba yake hii nzuri ambayo imeeleza mambo mengi. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Makamo wote wawili Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili kwa kuteuliwa katika nafasi zao hizo. Imani yetu kwamba watafanya kazi vizuri kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wale wote walioteuliwa kuwa mawaziri kwa kuweza kumsaidia Mhe. Rais. Imani yetu kwamba watafanya kazi nzuri na hatimaye nchi yetu itapata maendeleo. Pia nisiwasahau wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wote waliochaguliwa kutoka majimboni na pia kwa nafasi za akina mama na zile nafasi za Rais. Nawapongeza kwa kuteuliwa kwao kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo na pongezi sasa nije kwenye hotuba ya Mhe. Rais. Mhe. Spika, nchi yetu hii imeingia katika mabadiliko makubwa. Imeingia katika mabadiliko ya mfumo wa muundo wa serikali. Matarajio ya wananchi kwamba muundo huu utaleta mabadiliko makubwa yakiwemo mabadiliko ya siasa, uchumi lakini pia na katika huduma za jamii.

Mhe. Spika, wananchi wetu wanaangalia ni jinsi gani serikali hii itakavyoweza kuwasaidia katika kutatua matatizo yao mbali mbali. Wananchi wetu bado vipato vyao havilingani na matumizi yao. Vipato vimekuwa vidogo na matumizi yamekuwa ni makubwa mnao. Hili linawaletea matatizo katika hali yao ya maisha. Ni matumaini yao kwamba serikali hii mpya italeta mbadiliko na itaondosha matatizo ya maisha miongoni mwao.

Mhe. Spika, utakubaliana nami kwamba kuna baadhi ya wananchi katika maeneo wanakula mlo mmoja kwa siku. Kwa hivyo mabadiliko haya ya Katiba na mabadiliko haya ambayo yapo sasa hivi tunaamini kwamba yatawawezesha wananchi wale kuishi vizuri, kupata chakula kizuri, kupata chakula cha uhakika na waishi maisha mazuri kwa raha mustarehe.

Mhe. Rais katika hotuba yake alizungumzia mambo mengi, alizungumzia nyanja nyingi. Alizungumzia vipa umbele ambavyo amevitoa au atakavyovitoa katika uongozi wake wa miaka mitano hii ambayo tunaendelea nayo. Maeneo ambayo Mhe. Rais ameyagusia ni katika maeneo ya ustawi wa huduma za jamii kama vile maji, afya, elimu, umeme na mambo mengine. Lakini pia Mhe. Rais amezungumzia suala zima la uimarishaji wa miundombinu kama vile barabara, viwanja vya ndege na bandari. Lakini pia aligusia zaidi namna ya sekta za uzalishaji wa mali atakavyoziimarisha, lakini pia amezungumzia juu ya suala la maadili ya viongozi na pia juu ya utumishi wa wafanyakazi wa umma na amezungumzia zaidi suala la kudumisha masuala ya Muungano.

Mhe. Spika, mimi nitagusia baadhi ya maeneo ambayo yamenigusa. Mhe. Spika, yote ambayo Mhe. Rais ameyazungumza ni mambo mazuri na ni makini, laiti kama serikali itaweza kuyatekeleza haya hata kwa asilimia 50 basi nchi yetu itapiga hatua kubwa. Lakini naamini kwa ujasiri uliokuwepo na sura

ninazoziona kwa viongozi wetu basi yote yale ambayo Mhe. Rais ameyaahidi tutaweza kuyatekeleza kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mambo haya yanahitaji uchumi imara, lakini pia na kuimarisha masuala ya mapato. Kwa sababu huwezi kuyatekeleza haya bila ya kuwa na uchumi lakini pia huwezi kuyatekeleza bila ya kuwa na mapato ya kuridhisha.

Mhe. Spika, katika masuala mazima ya kuimarisha uchumi sekta ya viwanda ni muhimu, nchi yetu ina uhaba wa viwanda, ni lazima serikali itilie mkazo juu ya suala la kuimarisha viwanda vidogo vidogo na vile viwanda vya kati. Na kwa sababu sekta hii ya viwanda ina changamoto nyingi ikiwemo maeneo yale ambayo yanaweza kuanzishwa viwanda vyenyewe.

Kwa mfano, maeneo ya uwekezaji, maeneo ya maeneo huru kama vile Micheweni pamoja na Fumba ni lazima maeneo haya yaimarishwe ili tutoe nafasi kwa wawekezaji kuweza kuweka viwanda na maeneo haya ni lazima yafanyiwe miundombinu kama vile maji, barabara na umeme ili tuwawezeshe wawekezaji waweze kuwekeza katika masuala ya viwanda. Lakini pia suala la huduma ya umeme katika sekta ya viwanja maeneo haya yamekuwa mazito mno. Kwa hivyo, serikali lazima iangalie eneo hili la viwanda katika kuimarisha uchumi wake.

Katika kuendeleza uchumi wetu Mhe. Spika, ni lazima tutumie rasilimali tulizokuwanazo, rasilimali ya bahari. Mhe. Spika, rasilimali ya bahari ni lazima tuitumie ipasavyo. Kwa sababu visiwa vyetu hivi vimezungukwa na bahari, lakini hadi leo hatujaweza kuitumia rasilimali ya bahari ipasavyo. Kwenye bahari zetu kuna samaki wengi lakini hatujaweza kuwavua na kuwatumia kwa ajili ya kukuza uchumi. Lakini katika bahari zetu pia kuna rasilimali ya mafuta hatujaweza kuisimamia vizuri, tumekuwa tukizungumzia sana suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta, lakini inaonekana sasa hivi suala hilo tumeliacha kabisa sijui kwa sababu gani.

Suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta Mhe. Spika, linaweza kuwa mkombozi wa visiwa hivi. Niwaombe Waheshimiwa Mawaziri, nimuombe Mhe. Waziri anayehusika na Wizara ya Maji na Nishati aliendeleze suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Na kwa sababu upatikanaji wa mafuta katika visiwa hivi utaweza kutusaidia kuongeza uchumi na kuondosha matatizo ya wananchi wetu, rasilimali hizi Mwenyezi Mungu ametujaalia tunazo.

Lakini katika suala la kuimarisha mapato bado sekta ya utalii haijaweza kushughulikiwa ipasavyo. Sekta ya utalii ni sekta kiongozi ambayo inaweza ikaimarisha sana uchumi wetu, lakini mapato pia yanayotokana na utalii bado

hayajakusanywa ipasavyo. Sasa hivi kuna utalii wa watalii wa *packages*, inaonekana watalii wale wanaikosesha serikali mapato makubwa na kwa sababu kuna mbinu nyingi za ujanja ujanja.

Lakini eneo jengine Mhe. Spika, ni eneo la misamaha ya kodi. Eneo hili linaikosesha sana serikali mapato. Mhe. Spika, juzi tulipokuwa kwenye kamati ya Fedha na Uchumi tulipokwenda *TRA* kule taarifa tulizokuwanazo kwamba katika miezi mitano hii iliyopita serikali tayari imetoa misamaha ya kodi zaidi ya shilingi bilioni tisa. Mhe. Spika, kisiwa kama chetu, nchi kama yetu yenye mapato kidogo kusamehe fedha zaidi ya shilingi bilioni tisa kwa miezi mitano ni kiwango kikubwa mno. Kwa hivyo, tumuombe sana Mhe. Rais aangalie sana sera au zipitiwe sana, Mhe. Waziri anayehusika na misamaha ya kodi aangalie upya sera za misamaha ya kodi. Kwa sababu eneo hili linaiumiza sana serikali, inapunguza mapato makubwa sana ya nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, eneo hili linaweza likatusaidia ili kuona kwamba tunaongeza mapato ya nchi. Lakini eneo jengine ambalo tunahitaji kuliangalia sana katika kipindi chetu cha miaka mitano, ni kufuatilia kwa karibu ripoti ya *joint financial commission*. Mhe. Spika, eneo lile ni muhimu sana na kwa sababu tutakapolifuatilia eneo lile litatuongezea sana mapato yetu katika nchi yetu na tunaweza kuzitumia fedha zile kwa ajili ya kufanya mambo yetu. Mhe. Spika, eneo lile linahitaji kuangaliwa kwa makini, miaka mitano iliyopita tumekuwa tukilizungumza sana. Lakini wenzetu wa Tanzania Bara bado hawataki kulisimamia jambo hili ili likakamilika.

Mhe. Spika, kiwango cha asilimia 4.5 katika fedha za misaada ya kibajeti ni kiwango kidogo mno wakati mwengine tunapata nafasi ya kujiuliza kwa nini wenzetu Tanzania Bara wanapiga hatua. Mhe. Spika, mimi naamini katika eneo hili la fedha za misaada ya kibajeti zinazotolewa na wahisani linaweza likatusukuma sana. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Rais na mawaziri wanaohusika walisimamie sana jambo hili ili kuona ripoti hizi za *joint financial commission* zinafikia mwisho ili tuone tunapta mapato ya kutosha kwa ajili ya kufanya haya mambo ambayo tumeweza kuyakusudia.

Mhe. Spika, Mhe. Rais pia amezungumzia suala la maji, suala hili la maji lina changamoto nyingi sana pamoja na kwamba watu wa takwimu wanaeleza kuwa katika masuala ya maji kwa mjini tayari wananchi asilimia 75 wanapata maji safi na salama, na wale wa vijijini asilimia 60 ndio wanaopata maji safi na salama. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi sikubaliani na takwimu hizi, takwimu hizi ambazo zinatolewa na wataalamu wetu wa Idara ya Maji kwa kweli haziridhishi. Mhe. Spika, kwa sababu katika Jimbo langu la Magomeni mimi nathubutu kusema ni asilimia 20 tu labda ndio inayopata maji safi na salama na sio kwa kawaida maji haya yanapatikana kwa siku pengine wiki mara moja.

Mhe. Spika, Jimbo langu la Magomeni lina matatizo makubwa ya maji na kwa kweli jambo hili linanisononesha sana na linanisikitisha. Mhe. Spika, sioni sababu kwamba wananchi wale hawapati huduma ya maji kama walivyo wengine, na kwa kweli Mhe. Rais afanye utafiti wa kutosha juu ya masuala ya maji hasa katika maeneo ya Mijini, kwani takwimu hizi sio sahihi zinapotosha na zinadanganya umma, Mhe. Spika, maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi hayapatikani. Mhe. Spika, leo inasikitisha kwamba Serikali ya Japani imetoa fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuondosha matatizo ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Fedha hizo zimetumika na makampuni ya kitaalamu yamekuja yakafanya utafiti na ripoti ikatolewa.

Mhe. Spika, isitoshe Serikali ya Japani imetoa zaidi ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuondosha matatizo ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi. Lakini inasikitisha kiwango kikubwa cha fedha kimetumika, lakini bado matatizo ya maji yanaonekana yapo kwani wananchi bado wanalalamika juu ya upatikanaji wa huduma ya maji. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mwenzangu Mhe. Abdalla alizungumza sana juu ya suala la kuwa karibu na mawaziri wanaohusika na masuala haya. Mhe. Spika, na mimi nitakuwa karibu sana na Mhe. Waziri wa Maji rafiki yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa sababu sisi tuko hapa kwa ajili ya wananchi, tupo hapa kwa ajili ya kuwatumikia watu leo inasikitisha kuona bado miaka 47 baada ya mapinduzi wananchi wetu wanalalamika na maji. Mhe. Spika, ni lazima ufumbuzi wa jambo hili uweze kupatikana kwa kina.

Mhe. Spika, Sekta ya Elimu nayo inachangamoto nyingi, kuna ukosefu wa walimu wa sayansi. Mhe. Spika, dunia ya leo tunapozungumzia suala la sayansi na teknolojia lakini skuli nyingi hasa za sekondari zina matatizo ya walimu wa sayansi, hii ni changamoto kubwa ambayo Wizara yetu ya Elimu inataka ikabiliane nayo kuona kwamba tunapata walimu wa sayansi wa kutosha. Pia kuna ukosefu wa maabara kuna skuli za sekondari hazina maabara.

Mhe. Spika, kama skuli yangu ya Nyerere hakuna maabara leo tumtegemee mwanafunzi wa sayansi katika skuli kama hiyo ambaye hajafanya mazoezi kwa vitendo hata mara moja. Kwa hivyo, hii ni changamoto kubwa sana kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mazima ya elimu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ukosefu wa madawati inasikitisha kumuona mtoto wa skuli ya sekondari anakaa chini, hali hii bado ipo na hii ni changamoto kubwa kwa serikali juu ya masuala ya vikalio.

Mhe. Spika, suala la mikopo kwa wanafunzi wetu wanaotaka kwenda katika elimu ya juu hili ni tatizo. Mhe. Spika, ni kwamba bado kuna wanafunzi wengi wanakosa fedha kwa ajili ya kupata elimu ya juu.

Mhe. Spika, mwisho nataka nizungumzie sekta ya kilimo. Mhe. Spika, sekta ya kilimo sasa hivi nayo ina changamoto hususan katika maeneo ya kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Rais ametuahidi kwamba katika kipindi hiki ataweza kutekeleza masuala ya kilimo cha kisasa. Kwa hivyo, suala la kilimo cha umwagiliaji maji ni muhimu ambacho kinahitjai kuendelezwa na kitakuwa ndio mkombozi wa matatizo yetu katika maeneo ya kilimo.

Mhe. Spika, mwisho suala la sekta ya afya, sekta hii Mhe. Rais ameahidi kutoa huduma bora za afya na wenzetu wa afya wakubali hilo na walifanye hilo. Pia kuwe na uwezo wa kutoa fedha kwa ajili ya wagonjwa ambao wanataka kusafirishwa kwenda nchi za nje. Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo la upatikanaji wa fedha hasa kwa wale wagonjwa wetu ambao wameshindikana kutibiwa hapa ambao wanahitaji kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Kwa hivyo, serikali itoe kipao mbele itenge fedha zaidi kwa ajili ya wananchi wetu wale wanaohitaji kupata matatibabu zaidi kwenda nchi za nje.

Mhe. Spika, mwisho kwa kuwa muda wako umekwisha kwa hiyo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja na serikali hii naitakia kila la heri iweze kutekeleza mambo vizuri na ni matumaini ya wananchi itafanya vizuri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kabla ya yote sina budi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na vile vile kuweza kujadili mambo yetu makubwa ambayo yanalihusu taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Spika, pia nawashukuru wananchi wa Zanzibar kwa kuendesha uchaguzi kwa amani na utulivu, jambo ambalo leo hii limetufikisha hapa katika sura mpya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya umoja wa kitaifa. Vile vile napenda kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa kunichagua mimi kwa kura nyingi sana, kura ambazo zimenifanya leo hii nisimame hapa katika Baraza la Wawakilishi na kuzungumza mambo ambayo yanalihusu taifa lao.

Mhe. Spika, pia nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hotuba yake hii nzuri ambayo ameitoa siku ya tarehe 10/11/2010. Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba nichangie mambo matatu makubwa katika hotuba hii ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, suala la kwanza nitazungumzia suala la elimu la elimu ambalo wenzangu wengi wamelichangia hili. Mhe. Spika, katika hili ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata kuingia katika shule za msingi. Kwa hivyo, naiomba serikali yetu iondoshe yale malipo madogo ambayo kwa sasa hivi yapo kutokana na hali za wananchi wetu hasa kule vijijini ili wanafunzi wetu waweze kupata haki hii ya msingi.

Mhe. Spika, vile vile katika hili ili tuweze kuwainua wanafunzi wetu kielimu ni kwamba tunahitaji walimu wetu wawe na maslahi ambayo ni mazuri sana kwani bila ya walimu hawa kuwa na kitu ambacho wao kitawafanya wafanye kazi ya ziada nadhani hii hali ya kuwa elimu iko chini itaendelea hivi hivi. Kwa hivyo, naiomba Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba yenye sura mpya iangalie mishahara ya walimu katika jicho la huruma zaidi kuliko wizara nyengine zozote zile.

Mhe. Spika, hata hivyo naomba nizungumzie suala la wanafunzi wetu wa elimu ya juu hasa wale ambao wanasoma katika vyuo vya Zanzibar na hasa katika Chuo Kikuu cha Zanzibar cha Tunguu. Katika hili Mhe. Spika, kwanza naishukuru serikali angalau kwa kuwapatia baadhi ya wanafunzi mikopo na kuweza kusoma katika chuo kile cha Tunguu. Lakini katika hilo, mikopo ambayo inatolewa kwa hapa ni mikopo mitupu ambayo inahusiana na masuala ya ada ya kusomea tu. Mhe. Spika, jambo hili linawafanya wanafunzi wetu kupata shida kubwa sana hata ile ya usafiri kutoka maeneo ya mjini na kufika pale chuoni.

Mhe. Spika, vile vile masuala ya *stationary* na haja nyengine ambazo mwanafunzi anatakiwa azipate kwa ajili ya kujikimu zinakosekana. Kwa hivyo, kwa hili naiomba serikali yetu hii iwatizame kwa jicho la huruma wanafunzi wetu ambao wanasoma katika Vyuo Vikuu vya Zanzibar iweze kuwapatika mikopo.

Mhe. Spika, jambo jengine ni suala la vijana, katika hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar amezungumza sana suala la vijana. Kwanza napenda kumpongeza tena Mhe. Rais kwa kutujali sisi vijana na kujua kwamba kuna baadhi ya matatizo mengi ambayo yanatukabili sisi, na sisi kwa kutambua kwake kwamba ni sehemu moja muhimu katika taifa letu hili la Zanziba.

Mhe. Spika, katika hotuba hii Mhe. Rais wa Zanzibar amezungumzia kuhusu Baraza la Vijana la kitaifa. Hili ni jambo zuri la kupongezwa lakini katika hili naiomba serikali kupitia wizara inayohusika kuharakisha uanzishwaji wa Baraza hili la Vijana kwani kwa kuliona kwake ni kuwa limetupa matumaini

makubwa sisi vijana kuweza kutushirikisha katika shughuli zetu mbali mbali ambazo zinatuhusu sisi.

Mhe. Spika, jengine kuhusu vijana ni kwamba madawa ya kulevya ni tatizo kubwa ambalo linatuathiri sana sisi vijana hasa sasa hivi vijana wa Kizanzibari kila pembe unayokwenda unawakuta watu wanasinzia tayari wameshakula madawa ya kulevya. Mhe. Spika, mambo haya kwa kiasi kikubwa yanapunguza nguvu kazi ya vijana na ndio nguvu ambazo tunazitegemea sisi kama serikali ili vijana hao waweze kufanya kazi kwa ajili ya kutupatia kipato katika taifa hili. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hili naiomba sana wizara ambayo inahusika na masuala haya kufanya juhudi za dharura ili kulipunguza tatizo hili kwa manufaa ya vijana wetu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la ajira ni tatizo kubwa sana kwa vijana kwani vijana wengi hujiingiza katika mambo ambayo hayastahili yale ya uvunjaji wa sheria za nchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako hili tukufu namuomba Mhe. Waziri anayehusika kwamba katika hotuba ya Mhe. Rais amesema kutakuwepo mfuko maalum ambao utawashughulikia kuwakopesha vijana ili waweze kujiajiri wenyewe. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana mfuko huu uharakishwe haraka ili kuwanusuru vijana wetu waepukane na tatizo hili la ajira.

Mhe. Spika, mwisho nasema na mimi naungana na wenzangu kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia nyingi ambazo kuhesabika kwake naona hakuna. Kwa hivyo, kwa maneno mafupi mimi naiunga mkono hotuba hii, ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha hapa leo tukiwa na siku ya pili ya mkutano wetu wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwanza nawapongeza viongozi wetu kwanza Mhe. Rais Mstaafu Dk. Amani Abeid Karume na Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuleta maafikiano mpaka leo tuko hapa kwa imani moja na msimamo mmoja. Mhe. Spika, hata mgeni akija hapa basi hawezi akamchagua nani CUF na nani CCM.

Mhe. Spika, vile vile namshukuru Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, pia nalipongeza Baraza hili tukufu kwa kukuchagua wewe kuwa Spika wa Baraza hili, kwa hiyo natoa shukurani zangu za dhati kwako. Vile vile natoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe kwa imani yao kunichagua ili leo niko hapa nina ngara pamoja na wenzangu. Kwa hivyo, nawaahidi wananchi wa Jimbo la Matemwe

nitawatumikia kama walivyonichagua na sitokuwa na hofu wala sitoogopa ili kuwatumikia na kuleta maendeleo yao pamoja na Tanzania nzima.

Mhe. Spika, nimekisoma kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Rais mimi nakiita jina la kamusi la watu wa Zanzibar kwa sababu kitabu hiki kimeeleza yote ya maendeleo yetu. Mhe. Spika, kama utakifuata kitabu hiki ninahakikisha kwamba hatutoyumba na wala hatutorudi nyuma, isipokuwa tutazidi kuleta maendeleo.

Mhe. Spika, mimi nitachukua neno moja ambalo neno hili litakuwa limechanganya mambo yote yaliyokuwemo hili, neno hili linaloitwa miundombinu. Mhe. Spika, miundombinu imeanzia kwa watu wawili baina ya Mhe. Seif Sharif Hamad na Mhe. Amani Abeid Karume walipokubaliana kuileta miundombinu ili sisi Wazanzibari tukaafikiana na tukaleta moyo mmoja na hivi sasa leo tumekuwa kitu kimoja na hakuna malumbano yoyote katika nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa hilo.

Mhe. Spika, miundombinu ni kitu ambacho kikubwa sana tukikifuata sisi watu wa Zanzibari tutakuwa na maendeleo mazuri sana. Kwanza nitalizungumza Jimbo langu la Matemwe ni kwamba sasa hivi linakosa miundombinu kwa mambo mawili muhimu ambayo yanakosekana. Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar yeye mwenyewe aliwahi kuja katika jimbo letu akaliona hilo ni ukosefu wa barabara na maji safi na salama.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hapa jana aliitaja sana Pemba lakini nafikiri aliisahau Matemwe kwa hiyo namkumbusha kwamba Matemwe kuna uzito mkubwa wa ukosefu wa barabara hasa katika sehemu ya Kijini na Kigomani. Mhe. Spika, sehemu hiyo ya Kijini watu wengi wamekuwa masikini kwa ukosefu wa barabara, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwa kipindi cha bajeti ya mwaka huu aitizame Kijini ina ukosefu wa barabara na wananchi wake wote wamekuwa masikini kwa kukosa maendeleo hata ule uchuzaji wa samaki unawashinda. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namkumbusha aionee huruma Kijini kwa kuipelekea barabara.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu maji katika jimbo langu ni kwamba lina ukosefu wa maji. Hivyo basi namuomba Mhe. Waziri alione hilo ili na sisi tupate maji safi na salama huko katika kijiji cha Matemwe.

Mhe. Spika, sasa nije katika suala zima la ajira ni kwamba kuna vijana wengi sana sasa hivi wanakosa ajira na hali ya kuwa kuna mahoteli mengi sana lakini ajira hazipatikana katika hoteli hizo kwa kisingizio cha elimu.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, tunakwenda katika miundombinu ya ajira. Jimbo langu la Matemwe lina vijana wengi sana wanakosa ajira na hali kuna mahoteli mengi sana kwa kisingizio kwamba wanaambiwa vijana wale hawana elimu ya kutosha. Lakini sasa sijui wawe na elimu gani hata waajiriwe pale kwenye mahoteli, hivyo kweli kutandika kitanda kunataka *degree*?

Mhe. Spika, jambo hili lazima tulitizame kwamba mahoteli yanadhoofisha vijana wetu kwa kuwakosesha ajira kwa kisingizio cha kusoma. Lakini pale pale anakuja mtu kutoka jirani aidha Tanzania Baraza au Kenya ana cheti cha kughushi tu lakini anapatiwa kazi, lakini kijana aliyekuwa mzaliwa wa pale anaambiwa hakusoma. Sasa niiombe Wizara ya Utalii au serikali ituhakikishie hoteli zetu hizi mtu awe na kiwango gani cha elimu hata mwananchi wa Zanzibar aweze kupata kazi.

Nikizungumzia juu ya miundombinu, moja katika miundombinu ni kwamba wananchi wetu wapatiwe ajira hususan kule kwetu Matemwe kwa sababu kuna mahoteli mengi ambayo wananchi wameuza mali zao kwa umasikini ili watoto wao wapate ajira lakini hawapatiwi kwa sababu wanaambiwa hawana elimu.

Mhe. Spika, tunakwenda katika sehemu ya elimu. Hivi sasa vijana wetu wengi katika skuli kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza kuwa watoto wetu wanakosa madawati, inabidi wakae chini na mtoto akiwa yuko chini hata kule kuandika kutakuwa kwa tabu. Kwa hivyo, ningeiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ijitahidi pamoja na serikali yetu iwapatie watoto wetu madawati ya kusomea katika skuli zao.

Mhe. Spika, kwa kujumlisha hotuba ya Mhe.Rais ambayo inatufanya sisi sasa hivi tufanye kazi ya kikweli kweli na tuwe na imani na wananchi. Kwa kumalizia kwa sababu sitaki kuchukua muda mrefu sana kwa vile bado ni mgeni naogopa kuja kuzungumza mengi nikaja nikapotea, lakini nizungumze kidogo tu kwa leo.

Mheshimiwa sasa hivi nitaogelea kidogo katika biashara. Hivi sasa kusema kweli Zanzibar imefurutu ada vitu kupandishwa bei, ukilinganisha uchumi na hali yetu hivi sasa. Huu mchele ambao tunakula sisi wanyonge yaani mapembe umeshapanda bei. Kwa hivyo, namuomba Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko aangalie sana mapembe ambayo ndio tunayoyategemea sisi yamepanda sana sana.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza wakati nauheshimu wakati wako lakini nimalizie kwa kusema kwamba, wizara zote hivi sasa naziomba ziangalie wananchi wanavyopata tabu katika sehemu za afya, biashara, maji, barabara, ajira na elimu. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa heshima yako namalizia hapa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwepo hapa katika Baraza lako tukufu na mimi naunga mkono hoja juu ya Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pili, nakushukuru wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako kwa mara nyengine tena kulishikilia jahazi hili la kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi jipya lenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Pia Mhe. Spika, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chambani kwa makusudi bila ya kufanya ajizi kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao wa jimbo hilo kwa ajili ya kuwatumikia. Vile vile nawapongeza wawakilishi wenzangu wote wa Baraza hili jipya la Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, pamoja na hayo, nachukua nafasi ya kumpongeza Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar kwa hotuba yake nzuri, mahiri, hotuba iliyojaa nyama na ambayo isingefaa hata kidogo kuiongeza hili na lile. Lakini kwa sababu tupo kazini ni lazima na sisi tuoneshe mshikamano wetu baina yetu na yeye Rais wetu wa Zanzibar.

Mimi nitazungumza machache sana kwa sababu ya upya wangu na vile vile kuchunga muda, nitazungumzia kuhusu suala la wazee. Mhe. Rais alizungumzia suala la wazee naomba kunukuu, alisema kwamba, “Wazee ni hazina yetu na chemchem ya busara katika jamii yetu”.

Mhe. Spika, maneno haya ni ya hekima na ni maneno ya busara, kwa sababu wazee ndio uti wa mgongo wa maisha ya maendeleo yetu ya kila siku. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa hili naiomba Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliangalie sana suala la wazee na wale wazee ambao wamepatiwa makaazi basi waendelezwe kuenziwa na wale wengine ambao hawakupatiwa makaazi walioko vijijini waangaliwe vyema. Vile vile wazee wanaopewa posho basi posho hili liongezwe kwa wazee hawa na wale ambao hawajapewa posho naiomba serikali ifanye uhakiki wa kutosha wazee wale nao waingizwe katika mkumbo wa kusaidiwa. Kwa sababu tuna wazee wengi ambao wanastahiki kusaidiwa na hivi sasa nafikiri wengine wamekosa kusaidiwa kwa kutojulikana.

Kwa hivyo, waziri anayehusika afanye kazi ya ziada kuwatafuta wazee hao kupitia shehia zao ili na wao waingie katika mkumbo huu wa kusaidiwa na serikali yao hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza masuala ya wazee sasa kidogo niende katika suala la wafanyakazi. Mhe. Spika, wafanyakazi wetu wa Zanzibar kwa kweli wanaishi katika hali ya maisha magumu hasa wafanyakazi waliyopo

vijijini. Mishahara yao haitoshelezi kukidhi haja zao za kila siku pia huduma nyengine ambazo zingekuwa ni vitendea kazi kwa ajili ya kazi zao hawana. Hivyo namuomba waziri anayehusika na Mfuko wa *ZSSF* awaandae maafisa wa *ZSSF* watayarishe mpango maalum wa kuwakopesha wafanyakazi hawa angalau waweze kukopa kwa masharti nafuu ili wakidhi mahitaji yao ya lazima. Wafanyakazi wetu wengi wanafanya kazi maeneo ya mbali hawana hata vipando vya baskeli kwa sababu ya hali ngumu ya maisha. Sasa watapopata mkopo ambao utakuwa na masharti nafuu inawezekana kununua hata vespa, sitaji gari ambayo gharama yake kubwa, lakini angalau vespa ya kumfikisha katika eneo lake la kazi na kufanya kazi yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, katika wafanyakazi nizungumzie kidogo kuhusu suala la umri wa kustaafu. Nafikiria kwamba umri wa lazima wa kustaafu katika serikali yetu ya Zanzibar wanaume ni miaka 60. kwa kweli miaka 60 ya kuzaliwa katika maisha yetu mtu anakuwa keshakuwa mzee sana hasa vijijini kutokana na hali ngumu ya maisha. Lakini hapa naishauri serikali labda ingeweka miaka 55 ya hiyari na miaka 60 ya lazima. Kwa sababu kuna wafanyakazi wanapofika umri wa miaka 50 au 55 kwa hiari yao wanaweza kuomba kustaafu, lakini kwa sababu ya ulazima wa serikali hujilazimisha mpaka kufika umri wa miaka 60 hivyo hivyo kwa tabu.

Kwa hivyo, ningemuomba waziri anayehusika angewahiarisha wafanyakazi wanapofika umri wa miaka 55 ambaye kwa hiari yake anataka kustaafu astaafishwe na kupewa haki zake na atapofikia umri wa miaka 60 basi hapa astaafishwe kwa ulazima. Hili litasaidia pia punguzo la vijana wetu ambao wamemaliza masomo hawajaajiriwa kwa kuwa hawa watu wa miaka 55 watakapoamua kustaafu watapata nafasi wale ambao hawajaajiriwa kuajiriwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo nataka nizungumzie kimuhtasari kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Rais katika hotuba yake alizungumza kwa ufasaha sana suala la ufugaji. Kwa kweli suala la ufugaji katika nchi yetu tunalo kubwa sana lakini mimi nataka nizungumzie ufugaji katika nyanja moja tu, hili litamhusu zaidi Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri nataka ukubaliane nami kwamba kuna wafugaji wengine wanakosa kuwahurumia wanyama na wanyama hawa hawana Baraza la Wawakilishi linalowatetea. Ingelikuwa kuna Baraza la Wawakilishi la Wanyama basi hapana shaka ng'ombe na punda wanaotumwa vibaya hapa Zanzibar wangelikuwa wakipiga kelele katika Baraza lao. Kwa hivyo, kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa watu wa Zanzibar na mali zao miongoni mwa mali zao ni hawa wanyama. Namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi wizara yake iwaonee huruma wale wanyama wanaotumwa kistilhali. Nafikiri tukitembea katika maeneo ya Mwembemakumbi, Daraja bovu, Mtoni, tunawakuta

ng'ombe na punda wamebebeshwa mizigo na vigongo mgongoni. Mimi ni miongoni mwa wafugaji kwa kweli nakuwa naona huruma sana.

Kwa hivyo, kwa kupitia Serikali ya Umoja wa Kitaifa nahisi kwamba, wale askari wanaokaa njiani kwa kusubiri daladala tu, basi na wao pia tungewapangia kuhusiana na suala hili la kuwahurumia wanyama ambao wanateswa vibaya kabisa.

Mhe. Spika, mwisho nataka nitoe nasaha. Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mhe. Spika, alimwita Maulana na baada ya kuzungumza hotuba yake alisema hii ndio maana hasa ya kumwita Maulana kwa sababu alitupa nasaha nyingi sana katika umoja wa Uzanzibari na Umoja wa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa. Jamani mimi nataka nitoe kisa kimoja kidogo. Kwa sababu sote tumeapa kwa kutumia msahafu katika Baraza hili nataka nitoe kisa kinachohusiana na dini kidogo.

Mtume (S.A.W) alipokwenda Madina aliikuta jamii ya Madina imechafuka chafuka watu wanagomba na kufanya kila kitu. Lakini kwa sababu ya busara zake aliwaunganisha na wakawa kitu kimoja. Nafikiri kuna kasida watoto wetu wanaimba kwamba, "aliwaunganisha Answari na Muhajirina akaing'arisha Madina" ina maana Wazanzibari hivi sasa tumeshaunganishwa Wapemba na Waunguja, *CUF* na CCM tumekuwa kitu kimoja, tuing'arishseni Zanzibar. Ili Zanzibar ing'are basi sote ni kuwa na nia moja tukawa na serikali moja ya umoja wa kitaifa kama ilivyotangazwa na kama tulivyo watumishi wa umma tuwatumikie wananchi wetu kwa nia moja ili Zanzibar iwe moja katika ulimwengu huu wa dunia hii ambayo inahitaji maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hayo machache sitaki nipoteze muda mkubwa kwa sababu kuna mengi ambayo labda yataendelea. Mwisho nasema kwamba naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nakushukuruni kwa kunisikiliza Assalamu Alaykum.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Mohammed Mbwana kwa mchango wako huo na kuunga mkono hoja. Waheshimiwa Wajumbe nawakumbusha wale wajumbe wa kamati tuliowatangaza kabla kwamba ule mkutano wao na makatibu wao utakuwa katika chumba nambari mbili wasisahau kufika huko. Muda uliobaki ni mchache hatuwezi tukaendelea tusitishe shughuli zetu kwa hapa tulipofikia.
Lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kushirikiana katika shughuli zetu za Baraza. Na baada ya hapo sasa niahirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 21 siku ya Ijumaa saa tatu asubuhi.

(Saa 1:41 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 21/01/2011 saa 3:00 asubuhi)